# HOTUBA ZA KIISLAMU JUU YA HAKI ZA BINADAMU

الخطاب الإسلامي و حقوق الإنسان

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

ترجمة

# الخطاب الإسلامي و حقوق الإنسان

تأليف

الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 – 9987 – 17 – 100 – 2

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarujumiwa na:**
Muhammad A. Bahsan

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba
Na
AlHaji Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Mubarak A Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Mei, 2015
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 4 1/7/2015 11:52:44 AM

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji .................................................................... 2
Utangulizi............................................................................................. 4

Mwanadamu kati ya maandiko na hotuba za kidini...................... 10

Janga la kibinadamu..................................................................... 12

Hadhi ya binadamu ...................................................................... 14

Sherehe ya mwenyezi mungu ya kumtukuza binadamu.......... ….19

Utukufu wa binadamu na hotuba za kidini ................................... 23

Kuasisi heshima ya binadamu....................................................... 26

Je heshima ya binadamu inagawanyika? ...................................... 29

Ni ipi nafasi ya fatwa katika ubinadamu?..................................... 33

Heshima ya binadamu ni jambo la kiasili na kikanuni ................. 37

Hotuba za kidini na kujishughulisha na binadamu ....................... 39

Haki ya mwenyezi mungu na haki za binadamu .......................... 45

Kuvumilia unyonge au kudhalilika? ............................................. 49

Uboreshaji wa hotuba kwa ajili ya binadamu ............................... 50

Wanaharakati wa kiislamu na haki za binadamu .......................... 52

Ukweli juu ya kujishughulisha na haki za binadamu.................... 55

Kwa nini unafumbiwa machouvunjwaji wa
haki za binadamu?........................................................................ 59

Mtazamo wa kujishughulisha zaidi na haki za binadamu............. 64

Jumuiya ya kitaifa ya haki za binadamu ...................................... 66

Wajibu wa kutetea haki za binadamu........................................... 68
Kutetea haki ......................................................................... 71
Elimu ya haki za binadamu na hatua za kutekeleza...................... 76
Kutenda kwa ajili ya haki za binadamu ........................................ 80
Kati ya haki na wajibu .............................................................. 84
Haki sawa.............................................................................. 86
Wajibu kwanza....................................................................... 88
Ubinafsi .............................................................................. 90
Kuzingatia utekelezaji haki.......................................................... 92
Utukufu wa maisha na tabia ya dhulma........................................ 94
Damu ni mstari mwekundu.......................................................... 97
Mafunzo yaliyopotea ................................................................ 100
Harakati za kigaidi .................................................................. 102
Dhulma juu ya uhai................................................................... 104
Kukataza maovu kwa upole na kwa ajili ya kuleta manufaa...... 107
Tangazo la kimataifa la haki za binadamu.................................. 118
Tangazo la haki za mtoto .......................................................... 128
Waraka wa haki za binadamu katika uislamu ............................. 132
Vitabu vya marejeo .................................................................. 143

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

## KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

Kila sifa njema inamstahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote. Ewe Mola mfikishie Rehema Muhammad na kizazi cha Muhammad, kama ulivyomrehemu Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, na mbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, hakika Wewe ni Mwingi wa kuhimidiwa na kutukuzwa.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 1 1/7/2015 11:52:44 AM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni kitabu ambacho asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la: *al-Khitwabul-Islamiy Wahuququl-Insan* Kilichoandikwa na Sheikh Hassan Musa al-Saffar**.** Na sisi tumekiita: "**Haki za Binadamu"** kwa Kiswahili

Haki za binadamu ni suala ambalo limepigiwa kelele sana na wapenda haki na amani duniani, na hii imetokana na haki hii kuvunjwa kwa makusudi na watu madhalimu na na tawala kandamizi duniani. Aidha, Uislamu ni wa kwanza katika kuainisha haki hizo za binadamu na kuzisimamia kikamilifu. Hapa lazima ieleweke kwamba nazungumzia Uislamu na sio Waislamu, kwa sababu kuna baadhi ya Waislamu na serikali zinazojiita za Kiislamu ambazo ziko juu katika kuvunja haki za binadamu. Uislamu uko mbali na watu hao na serikali hizo.

Hivyo msimamo na mafunzo ya Uislamu huhakikisha kwamba haki za binadamu zinalindwa na kutekelezwa kama ilivyo. Na humkemea na kumlaumu kila mwenye kuzivunja haki hizo bila kujali kama yeye ni Mwislamu au la.

Mwandishi wa kitabu hiki anatumia kalamu yake kuelezea utukufu wa binadamu na maisha yake na jinsi ya kusimamia haki zake za msingi na kuzitekeleza

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu ambapo ulimwengu umejaa dhulma na uonevu unaofanyiwa ubinadamu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 2 1/7/2015 11:52:44 AM

Kwa hiyo, taasisi yetu ya Al-Itra imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Muhammad A. Bahsan kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukileta kitabu hiki kutoka lugha yake ya asili ya Kiarabu kuja katika lugha ya Kiswahili. pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hi. Allah awalipe wote malipo mema hapa Duniani na kesho Akhera – Amin kisha amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 3 1/7/2015 11:52:44 AM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# UTANGULIZI

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu**
**Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.**

Haki za binadamu ni jambo tukufu mno linalostahiki kupiganiwa, na kwa kweli ni jambo muhimu linalojumuisha kila jambo la kiadilifu la kibinadamu. Na lengo la msingi wa sheria za Mwenyezi Mungu ni kuhakikisha haki za binadamu zinapatikana, na kuzikomboa fikra zake dhidi ya ukoloni wa kidhalimu, ili binadamu huyu amnyenyekee Mola Wake peke Yake kwa kujaza uhuru wake na matakwa yake. Mitume ya Mwenyezi Mungu walikuwa ni viongozi wa harakati za utetezi wa haki za binadamu katika maisha yao yote, kutokana na ulinganio wao wa kuwataka watu kukataa maovu na kupambana dhidi ya dhulma na ufisadi. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Mwabuduni Mwenyezi Mungu, na mwepukeni Shetani." (Qur'ani; 16:36)**.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 4 1/7/2015 11:52:44 AM

Na katika Aya nyingine, Qur'ani imeifanya hali ya kumkataa Shetani kuwa ni hali ya kuingiwa na imani ya kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, inasema:

فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انْفِصَامَ لَهَا

**"Basi anayemkataa Shetani na akamwamini Mwenyezi Mungu, bila ya shaka atakuwa amekamata kishikio madhubuti kisichovunjika." (Qur'ani, 2:256)**.

Kwa hakika harakati za kutetea haki za binadamu zimethibiti na kukamilisha ratiba yake katika Ujumbe wa Kiislamu, kwani Qur'ani Tukufu imeliasisi jambo hili la kutetea haki za binadamu kwa kulifanya kuwa ni miongoni mwa nadharia za kifalsafa, kwa hivyo limekuwa ni jambo muhimu katika itikadi ya Kidini, na kuwa ni jiwe la msingi katika mfumo wa fikra za Uislamu, kama ilivyo kwa fikra ya ukhalifa wa mwanadamu katika ulimwengu, na hali ya kurahisishiwa viumbe vingine ili vimtumikie yeye, na fikra ya kuwa yeye ni mwenye kutukuzwa, na kwamba yeye ni mtu huru na mwenye maamuzi katika maisha.

Kama ambavyo Sheria ya Kiislamu ilivyochukua jukumu la kuweka utaratibu wa wazi wenye kubainisha haki za binadamu, na kuzichunga haki hizo katika nyanja mbalimbali. Na kama ambavyo maisha ya Mtume (s.a.w.w.) pamoja na maisha ya Maimamu Waongofu waliokuja baada yake yanavyotuonesha mfano bora na kigezo chema katika kuchunga haki za binadamu.

Lakini kwa masikitiko, ni kwamba siasa ya kidhalimu iliyotawala umma imeuweka utelekezaji wa Ujumbe wa Kiislamu katika



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 5 1/7/2015 11:52:44 AM

kuheshimu haki za binadamu katika hali hasi, na hapo mwanadamu akawa ni mwenye kutendewa maovu ya hali ya juu, kunyang'anywa uhuru wake na kukandamizwa haki zake katika miongo mingi ya historia ya mwanadamu. Lakini la kusikitisha zaidi kuliko hayo, ni kuwepo watu wenye kuutetea ukandamizaji huo, kama vile wasemaji wa watawala, washairi na waandishi wao. Utamaduni huo wa kuwatetea madhalimu, ulichukua sura ya kidini na kifani, huku ukipewa nguvu na utawala na uwezo wao wa kimali, sanjari na kupambana dhidi ya rai nyingine na fikra yenye kuleta mwamko.

Kutokana na hali hiyo, maandiko ya kidini yenye kulingania uadilifu, wema, kuheshimu mawazo ya watu na kuheshimu haki za binadamu, ni mambo ambayo yaliachwa, kwa kuachwa makusudi au kwa kuyatolea maana isiyo sahihi, inayokwenda sambamba na matakwa ya madikteta na madhalimu. Kama ambavyo kinyume chake, walizua na kutengeneza maandiko yanayolingania kwenye udhalili, kusalimu amri na kuishi katika hali ya kukubaliana na ukandamizaji na udhalili. Pamoja na hayo, katika historia ya wanadamu kumejitokeza mwanga wa nuru, na kumekuwa na wanachuoni walio huru, na wanafikra walio wema, na washairi wanamapinduzi, na makundi ya upinzani yaliyotetea haki za binadamu, lakini kutokana na mwenendo wa walio wengi haikuwezekana kukubaliana na fikra ya haki za binadamu, ambazo Mitume walizipigania na kuletwa na Sheria ya Kiislamu.

Na wakati ambao, umma wetu wa Kiislamu ukitumbukia katika handaki la ukandamizwaji na kudhulumiwa, katika nchi za Ulaya pamoja na Amerika kumeibuka harakati kubwa za kutetea haki za binadamu tokea karne ya kumi na nane, kwa ajili ya kuhakikisha kunapatikana haki za binadamu na kutetea uhuru wake na utu wake. Harakati hizo za raia zimeweza kuleta ushindi wa hali ya juu. Harakati hizo hazikuishia katika nchi zao tu kwa kusimamisha mfumo wa kisiasa wa kidemokrasia, bali ni jambo lililoenea na kuwa la kima-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 6 1/7/2015 11:52:44 AM

taifa, na kufanywa kuwa ni mkataba maalumu wa haki za binadamu ulimwenguni kote.

Walinganiaji wa Kiislamu wa zama hizi, badala ya kuitumia fursa hii adhimu na kujiunga na harakati hizi za kibinadamu, ili kuonesha kwamba malengo yake yanakwenda sambamba na mafunzo ya Kiislamu, na ili wawe mstari wa mbele katika kutetea haki za binadamu katika jamii zao zenye kukandamizwa, bali katika kiwango cha kimataifa, badala ya yote hayo, wengi wao wameshika msimamo wa shaka na woga, kwa kuogopa kuhamisha harakati hizi kutoka katika jamii nyingine, na kwa kuwepo baadhi ya nukta zenye kuleta ikhtilafu katika baadhi ya maelezo yanayohusiana na haki za binadamu. Mwisho ikawa kwa walinganiaji hawa ni kukubali kwamba, harakati za kutetea haki za binadamu zinaashiria hatari kwa Uislamu na Waislamu!!

Kutokana na hayo, ukandamizaji umechukua nafasi katika nchi za Waislamu, na kujihami kutokana na hatari ya kung'olewa. Na mwisho baadhi ya wanaharakati wa Kiislamu wamezinduka na kutambua kosa walilolifanya, na kuwaingiza kwenye kosa hilo watu wao kutokana na ujinga waliokuwa nao kuhusu suala la haki za binadamu, na kutolitilia maanani sana. Kwa hakika katika nchi nyingi za Waislamu ukandamizaji na dhulma vimeshika hatamu. Na ukandamizaji wa haki za binadamu na kunyang'anywa uhuru imekuwa ni jambo linalofanywa kiufundi na taasisi za ukandamizaji na za kijasusi, ambazo zimekuwa zikiwachunguza watu na kuwahukumu kwa mujibu wa rai zao na fikra zao. Na wanaharakati wa Kiislamu ndio ambao wamekuwa waathirika na wenye kudhurika zaidi, mpaka baadhi yao wakawa wakimbizi, na makimbilio yao makubwa ni katika nchi za Ulaya ambako wanapata usalama wa nafsi zao, na wananufaika na uhuru wao, na wanafanya harakati zao za Kiislamu chini ya mfumo wa kanuni zinazolazimisha kuheshimu haki za bin-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 7 1/7/2015 11:52:44 AM

adamu. Mwisho kumedhihiri asasi na vyama vya Kiislamu vinavyotetea haki za binadamu kwa sababu ya ukandamizaji wanaofanyiwa, na kwa ajili ya kunufaika na kaulimbiu hii ya kisiasa. Lakini kazi inayotakiwa kutoka kwa wanaharakati wa Kiislamu katika utetezi wa haki za binadamu ni kubwa zaidi ya hii wanayoifanya sasa, yanayotakiwa ni haya:

**Kwanza:** Kusisitiza haki za binadamu katika fikra na utamaduni wa kidini wa kisasa, na kutatua baadhi ya mambo yaliyopo katika tamaduni na sheria za Kiisalamu ambazo huenda zikawa zinaonekana zinakinzana na baadhi ya misingi ya haki za binadamu ambayo imethibitishwa na mikataba ya haki za binadamu ya kimataifa. Na kwa hakika sisi hatulazimiki kuachana na yale yaliyothibiti katika Dini yetu, lakini ni juu yetu kuhakikisha kunakuwepo mafungamano kati ya kila kitu au fikra na Dini, inawezekana kwamba baadhi ya rai au maoni yakawa yanafahamika kwa mujibu wa mazingira fulani ambayo inawezekana kuyaangalia upya. Kama ambavyo inatupasa kupambanua kati ya mambo yasiyobadilika na yale yanayobadilika, ni kwamba yale yenye kubadilika hutengeneza anuani mpya katika baadhi ya mambo, kiasi cha kuwepo athari wakati wa kuyatolea hukumu ya kisheria.

**Pili:** Inapasa kukubaliana na hali ya maendeleo ya fikra za kibinadamu na maendeleo ya harakati za utetezi wa haki za binadamu za kimataifa, kwa lengo la kuleta uwiano wa utambuzi na uelewa. Kwa kufanya hivyo tutaweza kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine, na pia kuweza kuwanufaisha kwa kile tulichonacho miongoni mwa urithi wetu na utamaduni wetu wa Kiislamu, miongoni mwa mafunzo na sheria na vipengele vyenye kumhudumia binadamu na kutetea haki zake na heshima yake.

**Tatu:** Hakuna budi kuzidisha harakati za kutetea haki za binadamu, ndani ya jamii zetu na nchi zetu, na liwe ni jambo lenye



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 8 1/7/2015 11:52:44 AM

kupewa kipaumbele, na la kulitolea juhudi zetu zote. Kwani mambo mengine ambayo tunayojishughulisha nayo katika ratiba yetu ya mambo ya kidini na huduma za kijamii, hayana umuhimu mkubwa kuliko kujishughulisha na utetezi wa haki za binadamu, bali kukubalika haki za binadamu katika jamii yeyote ile, kunafungua milango na kutanua wigo wa shughuli mbalimbali, na huondosha vikwazo vinavyokwaza maendeleo. Baada ya hayo: Hakika kurasa hizi chache zilizomo mikononi mwako ewe ndugu msomaji mpendwa, zinazungumzia juu ya msimamo wa hotuba za Kiislamu katika zama hizi katika suala la haki za binadamu, na pia kuelezea baadhi ya fikra na kimsingi zenye kuonesha umuhimu wa jambo hili katika uwanja wa Kidini na kwa mtazamo wa wananchi. Natarajia kwamba baadhi ya kurasa hizi zitasambazwa na kusaidia katika kuhimiza utamaduni wa kutetea haki za binadamu katika jamii yetu ya Kiislamu. – **Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa kuwezesha.**

**Hasan Safar**
**11 Muharram 1426 A.H.**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 9 1/7/2015 11:52:44 AM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# MWANADAMU KATI YA MAANDIKO NA HOTUBA ZA KIDINI

Ni juu yetu kutofautisha kati ya hotuba za kidini na maandiko ya kidini, kwani maandiko ya kidini ni kila kilichothibiti kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kutoka kwa Mtume Wake, Muhammad (s.a.w.w.), kwa maana Kitabu (Qur'ani) na Sunnah. Kwani Qur'ani Tukufu haina shaka kwamba yote ni Kitabu Kitukufu kilichosalimika kutokana na kuzidishwa na kupunguzwa. Ama Sunnah Tukufu ni zile zilizothibiti usahihi wa mapokezi yake kama ilivyoelezwa na wanachuoni wa umma. Na maandiko haya ya kidini (Qur'ani na Sunnah) yako juu ya kanuni ya kuhukumiwa na kutuhumiwa. Ni kwamba maandiko hayo yanazungumza kwa niaba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ni Wahyi kutoka Kwake, na ni vyanzo vinavyotokana na Maasum (Wasiokosea), na wala haiwezekani ikaingia chembe ndogo ya shaka katika moyo wa Mwislamu juu ya ukweli wake na utukufu wake.

Ama hotuba ya kidini ni ile anayoifahamu mwanachuoni, msomi na mwanafikra kutokana na maandiko ya kidini au kutoka katika vyanzo vya ijtihadi vyenye kutegemewa. Hotuba za kidini hupatikana katika fatwa za wanachuoni, maandishi yao, mazungumzo ya wenye kuhutubu na rai, msimamo na muongozo wa kidini. Kwenye hotuba za kidini hakuna utukufu wala kanuni ya kusalimika na makosa, kwani mwenye kujitahidi hupatia na kukosea. Kwani huelezea kiwango cha ufahamu wake na uelewa wake, na mara nyingine huenda akaathirika na vishawishi tofauti vya kinafsi na kijamii ambavyo



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 10 1/7/2015 11:52:44 AM

huakisi rai yake na taswira yake. Kama ambavyo sehemu kubwa ya hotuba za kidini katika zama zetu hazitolewi na wanachuoni waliofikia daraja ya ijtihadi, bali hutolewa na watoaji mawaidha na mahatibu ambao wamefanya hotuba hizo kuwa ni kazi yao, na pia kutoka katika vikundi ambavyo vinajishughulisha na shughuli za kidini bila ya kuzingatia uwezo wa kielimu na usahihi. Kwa hivyo hotuba za kidini zinaweza kukosolewa na kusahihishwa, kwa sababu zinatokana na wanadamu. Ama maandiko ya kidini ni Wahyi wa Mwenyezi Mungu au maelezo kutoka Kwake.

Ni kweli kwamba hotuba za kidini zinategemea maandiko ya kidini, lakini jambo hili linategemea ufahamu na tafsiri ya maandiko, ufahamu huu na tafsiri unaweza kukosolewa na kusahihishwa. Kwani kuna baadhi ya tafsiri za baadhi ya maandiko ya kidini zinakuwa hazina ukweli, au kuelezwa nusu nusu, au kusomwa nje ya vile ilivyokusudiwa. Kama vile ambavyo baadhi ya maandishi yanayosemwa na kutolewa dalili, yanahitaji uhakika na uthibiti wa usahihi wa mapokezi yake.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 11 1/7/2015 11:52:44 AM

## JANGA LA KIBINADAMU:

Miongoni mwa mambo ya wazi ya aibu na kushindwa katika jamii zetu ni kudharauliwa kwa nafasi ya binadamu, na kupungua kiwango cha kushughulikia thamani yake na haki yake na kutetea heshima yake, mpaka umma wetu umekuwa ni wenye kushika nafasi za juu katika ukandamizaji wa haki za binadamu katika ngazi za kimataifa. Ukandamizaji huu si katika upande wa watawala wa kisiasa tu, bali ni katika kiwango cha jamii kwa ujumla. Kwani kuna ugaidi wa kifikra ambao unazuia uhuru wa mtu kueleza mawazo yake, ubaguzi dhidi ya mwanamke na kumuweka daraja ya pili, ukali dhidi ya watoto ambao hukandamizwa utu wao, na uoni mwingine wowote ambao husababisha kuwepo na tofauti.

Kutokana na hali hii, kumesababisha kuwepo na mitizamo ya kigaidi inayotekeleza unyama, kuuwa watu, kukata watu vichwa, kuwateka watu wasio na makosa na kuwalenga raia wa kawaleta katika mapambano. Yote haya yanafanywa kwa jina la Dini na chini ya nembo ya Uislamu, na kwa anuani ya kutetea vitu vitukufu vya umma.

Matendo haya ni uvunjifu wa wazi wa haki za binadamu katika jamii ya Kiislamu, na huu ni ukataaji wa wazi wa heshima ya binadamu na hadhi yake, huku kila mmoja akiyanasibisha matendo hayo na Dini. Kutokana na hali hii ni wazi kwamba hotuba za Kidini zitakuwa ni zenye kutuhumiwa.

Kwa hakika hakuna shaka juu ya usafi wa Dini na kuwa kwake mbali na haya yanayofanywa kwa jina lake, kwani maandiko sahihi ya Dini yanaonesha wazi namna yanavyojishughulisha mno na ubinadamu wa binadamu, na heshima ya hali ya juu ya utukufu wake na haki zake ambazo hazina mfano wake katika imani yoyote au utamaduni wowote. Kwa hivyo, inawezekana kuzikosoa hotuba za



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 12 1/7/2015 11:52:45 AM

Kidini za zama zetu hizi na kuzirekebisha kwa kutumia maandiko sahihi ya Dini, lakini ikimili zaidi katika misingi ya Dini ya Mwenyezi Mungu na malengo ya Sheria, na kuwafikiana na heshima ya binadamu na vipimo vya kiakili.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo tunaona kuwa ni mapungufu katika hotuba za Kiislamu katika zama zetu hizi, katika upande wa kujishughulisha na heshima ya mwanadamu na haki zake.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 13 1/7/2015 11:52:45 AM

# HADHI YA BINADAMU:

Katika karne ya kati, nchi za Ulaya ziliteseka kutokana na kanisa kupinga hadhi ya binadamu na heshima yake, na likasisitiza zaidi katika upande wa kumtukuza Mungu. Jambo hili lilipelekea ulipizaji wa kisasi katika jamii hiyo, wakawa wanapinga juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuinyanyua hadhi ya binadamu. Kutokana na hali hii baadhi ya madhehebu (mirengo) za kibinadamu zimeeleza majanga ya kibinadamu zikidhihirisha mwelekeo huu, kama ilivyoelezwa na (Walter Liebman, 1929). Anaeleza kama kwamba tabia za kibinadamu zinagongana na mafunzo ya Kiungu, anasema: "Ni kwamba ikiwa watu wataendelea kuamini ufalme wa mbinguni, basi wao wanahitaji kupata kheri zote katika uzoefu wa kibinadamu. Wana wajibu wa kuishi katika imani, kwamba wajibu wa binadamu ni kuyafanya matakwa yake yawe yanakubaliana na maumbile yake, na sio kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, bali ni kufanya kilicho bora zaidi katika kutambua furaha ya kibinadamu."[1]

Hotuba za Kiislamu nazo zimeathiriwa na ugonjwa huu wa kanisa la Kikiristo, kwani katika hotuba zake kumepindukia mipaka katika kutoa maelezo juu ya dhati ya Mwenyezi Mungu na sifa Zake, huku ikipuuziwa nafasi ya binadamu ambaye kuwepo kwake kunabainisha dalili za Mwenyezi Mungu na utukufu Wake, na ni mfano bora wa uwezo Wake Mwenyezi Mungu na ni sehemu ya utukufu Wake. Watu wa mrengo huu wamekuwa wakizamia katika kufanya tafiti juu ya dhati ya Mwenyezi Mungu na sifa Zake, na kujishughulisha katika mizozo itokanayo na maudhui haya, na ambayo mara nyingi imepelekea katika mgawanyiko na mapambano yenye kusikitisha.

[1] Lanland: Andaria, *Mausuatu Landaria al-Falsafiya*, Jz. 2, Uk. 568.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 14 1/7/2015 11:52:45 AM

Kwa upande mmoja kuna Shia na Mu'tazila, na upande wa pili kuna Ashaira, wakitofautiana juu ya kuungana na kuwa kitu kimoja kati ya dhati ya Mwenyezi Mungu na sifa za dhati. Au kauli ya Ashaira, inayosema kwamba, kuna sifa za ukamilifu zilizozidi katika dhati, katika hali ya nadharia na kivitendo. Au tofauti juu ya kuonekana kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama, au kuhusu utangulizi wa Qur'ani na kuumbwa kwake.

Licha ya kwamba utaratibu wa Qur'ani Tukufu ni maelezo ya mara kwa mara juu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kufikiri utukufu wa Mwenyezi Mungu kwa kupitia viumbe hivyo, na kufikiria juu ya uzuri wa ulimwengu na mpangilio wake wenye ufanisi, na kutafiti juu ya utajiri mkubwa uliomo, na pia kufikiri juu ya mpangilio madhubuti unaoendesha maisha humo (katika ulimwengu). Mwenyezi Mungu anasema:

وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

**"…na wanafikiria umbo la mbingu na ardhi…"**
**(Qur'ani, 3:191).**

قُلِ انْظُرُوا مَاذَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

**Sema, tazameni ni yapi yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini!**
**(Qur'ani, 10:101).**

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِلْمُوقِنِينَ وَفِي أَنْفُسِكُمْ أَفَلَا
تُبْصِرُونَ



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 15 1/7/2015 11:52:45 AM

**“Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini. Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamwoni?” (Qur’ani, 51: 20-21).**

Ama kufikiri kuhusu dhati ya Mwenyezi Mungu si jambo lililoamrishwa, bali ni kinyume chake, kwani kuna Hadithi na Riwaya zinazokataza kujishughulisha kufikiri katika dhati ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) ya kwamba amesema: “Fikirini katika maumbile ya Mwenyezi Mungu, na wala msifikiri juu ya Mwenyezi Mungu, mtaangamia.”[2] “Fikirini katika maumbile, na wala msifikiri katika Muumba.”[3] “Fikirini katika neema za Mwenyezi Mungu, na wala msifikiri juu ya Mwenyezi Mungu.”[4] Na imepokewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) akisema: “Tahadharini dhidi ya kufikiri juu ya Mwenyezi Mungu, kwani kufikiri huko hakukuzidishieni isipokuwa kupotea.”[5] “Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: ‘Na kwamba kwao Mola Wako ndio mwisho.’ Basi atakapomaliza maneno, jizuieni.”[6]

Hotuba za kidini na uzungumziaji kuhusiana na Mwenyezi Mungu umekuwa mkubwa, huku uzungumziaji juu ya hadhi ya binadamu umepewa nafasi ndogo sana, hailingani na kiwango kikubwa kilichoelezwa ndani ya Qur’ani Tukufu juu ya hadhi yake, nafasi yake na sifa za kipekee alizopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kumueleza kwamba ni mbora wa viumbe.

Kwani kwa hakika Qur’ani Tukufu imeanza na *Bismillahi* (**Kwa jina la Mwenyezi Mungu**), na mwisho wake imemalizia neno *‘Annasu’* (watu). Neno *‘Annasu’* limetajwa takribani mara 234, na neno *‘Insaanu’* (binadamu) mara 90, *‘Ibadu’* (waja) zaidi

---

[2] Al-Muttaqiy al-Hundiy, Ali, *Kanzul Ummal*: Hadithi Na. 5705.
[3] Kitabu kilichotangulia: Hadithi Na. 5706.
[4] Kitabu kilichotangulia: Hadithi Na. 5707.
[5] Al-Majlisiy, Muhammada Baqir, *Biharul An-wari*: Jz. 3, Uk. 259.
[6] Kitabu kilichotangulia.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 16 1/7/2015 11:52:45 AM

ya mara 100, *'Basharu'* (binadamu) mara 37 na *'Bani Adam'* (wanadamu) mara 8.

Na Aya mbali mbali za Qur'ani zinaelezea nafasi aliyonayo binadamu na namna alivyokuwa ni kiumbe wa kipekee, kama kauli yake Mwenyezi Mungu:

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلا

**"Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba." (Qur'ani, 17:70).**

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ

**"Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa." (Qur'ani, 95:4).**

وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ

**"Na akakutieni sura, na akazifanya nzuri sura zenu…" (Qur'ani, 40:64).**

Ni sahihi kwamba baadhi ya Aya za Qur'ani zinazungumzia vipengele dhaifu na hasi katika shakhsia ya binadamu, lakini ni kwam-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 17 1/7/2015 11:52:45 AM

ba Aya hizo zimekuja kumuelekeza ili kujitenga nazo na kuelekea katika daraja za ukamilifu. Kwa kweli ni Aya ambazo zinamzungumzia binadamu kutoka katika mughafala alionao, na wala Aya hizo hazimuondolei uwezekano wa kuwa mkamilifu na kuwa na daraja ya heshima. Na mara nyingi hotuba za Kiislamu zinakita katika hali hii, kumuonesha binadamu kuwa yuko katika hali ya udhaifu na mughafala, kama kwamba ndio namna ambayo Qur'ani imetaka kumueleza binadamu, kama vile kwamba binadamu ameficha kasoro ambazo zina matokeo mabaya na kuamiliana naye katika mawanda ya kidini.

Kwa hakika lau kama tunaangalia mifano ya kibinadamu ambayo imeelezwa na Qur'ani Tukufu kwa kupitia Aya Takatifu, tutaona kwamba idadi kubwa ya mifano hiyo ni kuhusu Mitume, Mawalii na watu wema, katika hali ambayo mifano ya watu mafisadi kama vile madhalimu, matwaghuti na waovu ni michache. Hiki ni kwa mujibu wa kiwango cha mifano, na huenda hali hiyo ikatueleza namna Qur'ani ilivyomweleza binadamu katika sura yake ya heshima ya hali ya juu, pamoja na kuzingatia hali iliyoelezwa na Qur'ani Tukufu juu ya kuenea hali ya mughafala na udhaifu katika anga ya wanadamu.

# SHEREHE YA MWENYEZI MUNGU YA KUMTUKUZA BINADAMU:

Maelezo ya Qur'ani juu ya kuumbwa kwa binadamu yanadhihirisha wazi nafasi ya kipekee ya binadamu aliyowekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika kuieleza nafasi hiyo tuzingatie vipengele vifuatavyo:

Katika Qur'ani hakuna maelezo ya kina juu ya uumbwaji wa viumbe vyote kama vile mbingu, ardhi, Malaika na viumbe vingine kama ilivyoelezea kuumbwa kwa binadamu. Wahyi wa Mwenyezi Mungu ulianza na maelezo ya uumbaji na kumtaja binadamu miongoni mwa viumbe vyote, kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ

**"Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliyeumba. Amemuumba binaadamu kwa tone la damu." (Qur'ani, 96:1-2).**

Mwenyezi Mungu ameumba viumbe vyote kwa uwezo Wake, lakini Mwenyezi Mungu amesimamia uumbaji wa binadamu kwa uangalizi Wake na kuwa katika namna ya kipekee, anasema:

قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**Akasema: Ewe Iblisi! Kipi kilichokuzuia kumsujudia yule niliyemuumba kwa Mikono Yangu? (Qur'ani, 38:75)**

Jambo kubwa lenye shari halifanywi na mikono Yake, isipokuwa jambo lenye uzito na kuwa na thamani ya hali ya juu, na kwa vile



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 19 1/7/2015 11:52:45 AM

Mwenyezi Mungu hana viungo (hatendi kwa kutumia viungo), basi makusudio ya Aya ni kwamba amemuumba binadamu kwa uangalizi maalumu. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu alivyoeleza kwamba alimpulizia binadamu roho Yake, anasema:

فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ

**Na nitakapomkamilisha na nikampulizia roho Yangu, basi mwangukieni kwa kusujudu. (Qur'ani, 38:72).**

Hii haina maana kwamba sehemu fulani ya Mwenyezi Mungu imeingia katika kiwiliwili cha binadamu, kama wanavyodai baadhi ya watu wenye itikadi kama hiyo, lakini ni kwamba Aya hii inadhihirisha utukufu na heshima aliyonayo kwa kupitia tamko la 'Kumpulizia roho.' Na kwa kweli Mwenyezi Mungu amewaeleza Malaika wake juu ya matakwa Yake ya kutaka kumuumba binadamu, kama alivyowaeleza juu ya jambo kubwa ambalo anataka kulifanya, anasema Mwenyezi Mungu:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً

**Na Mola wako alipowaambia Malaika: Mimi nitaweka khalifa katika ardhi. (Qur'ani 2:30).**

Na wakati Mwenyezi Mungu alipomuumba binadamu, aliweka sherehe ya kilimwengu ya kusherehekea kuwepo kwake, na akawaamrisha Malaika wafanye sherehe ya kumpongeza na kumtukuza kwa kumsujudia, kama anavyosema:



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 20 1/7/2015 11:52:45 AM

فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ فَسَجَدَ الْمَلَائِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ

**Na nitakapomkamilisha na nikampulizia roho Yangu, basi mwangukieni kwa kusujudu. Wakasujudu Malaika wote pamoja. (Qur'ani 38: 72-73).**

Huenda Aya hizi zikawa zinaashiria namna Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyoufanya ulimwengu umtumikie binadamu, kama anavyosema:

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

**"Kwani hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na kwenye ardhi." (Qur'ani 31:20).**

Baadhi ya watu wanaonelea kwamba sijda iliyofanywa na Malaika ilikuwa inamhusisha Adam kwa kuzingatiwa kwamba alikuwa Mtume, na wala haihusiani na jinsia ya kibinadamu, lakini kwa mujibu wa mtiritiko wa Aya za Qur'ani inapingana na kauli hii, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ يَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 21 1/7/2015 11:52:45 AM

**Na hakika tuliwaumba, kisha tukawatia sura, kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu wote isipokuwa Iblisi hakuwa miongoni mwa waliosujudu. (Qur'ani, 7:11)**

Kwa hakika Aya hii inazungumzia wanadamu kama wanadamu na neema ya kuumbwa kwao, kisha kutiwa sura, kisha kusujudiwa na Malaika wakiwa ni wenye kutekeleza kile walichomfanyia baba yao wa mwanzo, Adam. Allamah Tabatabai anasema: "Sijda ya Malaika ilikuwa ni wana wa Adamu wote, kwa sababu ndio chanzo cha ubinadamu, licha ya kwamba Adamu (a.s.) ndiye aliyeelekewa wakati wa sijda, wakati ilipotolewa amri ya sijda alielekewa yeye akiwa anauwakilisha ubinadamu kwa niaba ya binadamu wote, na sio kuhusishwa yeye kama yeye."[7]

Hivi ndivyo ambavyo maandiko ya Qur'ani yanavyosema kuhusiana na nafasi ya binadamu, katika hali ambayo hotuba za Kiislamu hazizungumzii daraja ya kipekee ya thamani ya binadamu. Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Hakuna kitu kilicho kitukufu mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko binadamu."[8]

[7] Tabatabai: Sayed Muhammad Husein, *al-Mizan fii Tafsiril Qur'ani*, Jz. 8, Uk. 21.
[8] Al-Muttaqul Hindiy: Ali, *Kanzul Ummal*, hadithi Na. 34621.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 22 1/7/2015 11:52:45 AM

# UTUKUFU WA BINADAMU NA HOTUBA ZA KIDINI

Ushirikiano wowote wa baadhi ya watu kwa misingi ya kimada au kiroho unahusiana na kiwango maalumu cha mahusiano kati yao, kwa mfano ikiwa mahusiano yao yanatokana na ukoo mmoja, basi hisia zao zitakuwa ni juu ya kushirikiana katika mambo maalumu, au wakiwa ni watu wa dini moja, basi mafungamano yao kati yao yatakuwa ni ya hali ya juu, na kuheshimiana kutakuwa ni kukubwa mno. Jambo hili ni la kimaumbile na lililo maarufu, lakini je mahusiano kati yao ndio itakuwa ni sababu ya kuwadharau wale walio nje ya umoja wao miongoni mwa wanadamu? Na je hiyo inamaanisha kwamba kutukuzana na kuheshimiana inabakia katika wigo wa watu walioungana nao tu, ama wengine ni wanadamu wa daraja la pili?

Kwa hakika sisi tunakuta katika maandiko ya Kiislamu yakisisitiza ubora na utukufu kwa misingi ya Uislamu na Imani, na kuwa ndivyo vinavyomkamilisha binadamu, na kunyanyua hadhi yake na kuheshimu haki zake. Yote haya ni kwa mujibu wa mafungamano yaliyomo katika mfumo wa itikadi juu ya haki ya Dini na misingi yake, na katika misingi ya kushikamana kati ya wafuasi wake. Lakini, je hii inamaanisha kupinga na kukataa heshima ya binadamu aliye nje ya Uislamu? Na je, inatoa nafasi ya kuwadharau wanadamu wasiokuwa Waislamu? Au ndio inakuwa sababu ya kuwavunjia heshima zao na kuwanyima haki zao za kimada na kiroho?

Kwa hakika wanadamu wamesibiwa na ugonjwa wa kuenea fikra hizi katika karne nyingi, ambapo baadhi ya makundi ya watu yamenyimwa heshima yao na watu wasiokuwa wao, jambo lililopelekea kuasisiwa visingizio vya kufanyiwa uadui na kuvunjiwa heshima na kunyimwa haki zao. Kwa mfano, harakati za kinazi zilizokuwa ziki-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 23 1/7/2015 11:52:45 AM

ongozwa na Hitler, zililenga katika kuwatukuza na kuwafadhilisha ukoo wa Maariy, na kwamba Mayahudi, Masalifiin na watu wa jamii za wachache wakiwekwa daraja la chini, na ikawa wale wasiokuwa Maariy wakitengwa na ajira za serikali, na kuzuiwa kuingia katika sehemu za mikusanyiko, na kupigwa vita kila ukoo ambao haukuwa wa Kiariy.[9]

Mayahudi na Manaswara nao walikuwa wakieneza fikra katika jamii zao kwamba wao ni taifa teule lililoteuliwa na Mwenyezi Mungu, kiasi cha kupelekea kuwadharau watu wa mataifa mengine na kuwanyima haki zao, kama inavyosema Qur'ani:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ وَالنَّصَارَىٰ نَحْنُ أَبْنَاءُ اللَّهِ وَأَحِبَّاؤُهُ
قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوبِكُمْ بَلْ أَنْتُمْ بَشَرٌ مِمَّنْ خَلَقَ

**"Na Mayahudi na Manaswara wanasema: Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Sema: Basi kwa nini anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu (tu) katika aliowaumba. (Qur'ani 5:18).**

Haya ndio matamshi ya Mwenyezi Mungu ambayo yanathibitisha juu ya kuwepo usawa kati ya wanadamu katika ubinadamu wao, amesema: **"Bali nyinyi ni watu tu kama wale wengine aliowaumba."** Kwa hivyo haimaanishi kuwepo kwa mahusiano ya kiukoo au kidini kuwa ni sababu ya kuwadharau wengine au kuwanyima haki zao, kama walivyokuwa wakifanya Mayahudi ambao walikuwa hawaiheshimu mali ya mwingine asiyekuwa Myahudi, kwa kuwazingatia kwamba ni wapumbavu, na wao Wayahudi hawana kosa lolote katika kuwapora haki zao, kama anavyoielezea hali hiyo Mwenyezi Mungu pale aliposema:

[9] Kayaliy: Abdul Wahhab, *Mausuatus Siyasiya*, Jz. 6, Uk. 546.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيِّينَ سَبِيلٌ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

**"Hayo ni kwa kuwa walisema: Hatuna lawama kwa wasiojua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na hali wanajua." (Qur'ani: 3:75)**

Kwa hakika wao wanamsingizia Mwenyezi Mungu kwa kudai kwamba sheria walizoteremshiwa zinaruhusu kupora mali ya wengine wasiokuwa wafuasi wa dini yao, **"Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma."** Lakini Mwenyezi Mungu amewajibu jawabu lenye kukata ngebe zao, ya kwamba hayo wanayoyasema ni uongo mtupu, na haiwezekani Mwenyezi Mungu akawawekea sheria yenye kukandamiza haki za watu wengine, anasema: **"Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua."**

Na bila ya Qur'ani Tukufu kuja kukataza mtindo huu na fikra hizi na kuzijibu ingekuwaje, na haikuwa tu kwa sababu ya kuenea kwake kwa Mayahudi na Manaswara, bali jambo lililo muhimu zaidi ya hilo ni kutahadharishwa umma wa Kiislamu dhidi ya kufuata mwenendo kama huo, kwani kile kinachoendelea katika jamii ya Waislamu ni fikra juu ya kuwadharau wengine, zinazopelekea kuwanyima haki zao. Kwa hakika lengo la Qur'ani Tukufu, kwanza na kabla ya jambo jingine ni kuasisi heshima ya binadamu kwa sababu ya ubinadamu wake, akiwa katika kabila lolote lile, na akiwa mfuasi wa dini au itikadi yoyote anayoifuata, kwani yeye ni binadamu anastahiki kuheshimiwa.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 25 1/7/2015 11:52:45 AM

# KUASISI HESHIMA YA BINADAMU:

Sayyid Muhammad Husein Fadhlullahi ametanabahisha ukweli huu, na akasisitiza jambo hili katika kuitafsiri Aya ya sabini na tano ya Suratul-Imran, kama alivyosema:

"Huenda ikawa tunajifunza kutokana na makemeo ya Mwenyezi Mungu kuwakemea Mayahudi juu ya nadharia yao kwa wengine, na kutowajibika kwao juu ya mali ya wengine, wakijipa haki ya kuichukua kwa dhulma. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu hawataki Waislamu kufuata nadharia hii katika kuamiliana kwao na wasiokuwa Waislamu, wakawa wanajihalalishia wenyewe kuwapora mali zao na kuziiba, kwa hoja kwamba hakuna kumheshimu kafiri, katika nafsi yake na mali yake, isipokuwa dhimmi au aliyeweka ahadi ya kuishi na Waislamu kwa salama na amani. Hii ni hukumu waliyoipitisha baadhi ya wanachuoni ambao hawaoni kwamba asili ya anuani ya kivita ni kuhalalisha mali ya makafiri kwa Waislamu, bali wanaona kwamba asili yake ni kutowahishimu isipokwa dhimmiy au aliyeweka ahadi ya kuishi salama na amani katika nchi ya Waislamu. Hukumu hii wameitoa kutoka katika maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yasemayo: "Mwenye kusema hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa kauli hii mali yake italindwa na damu yake na utu wake," na mfano wa Hadithi ambazo zinazungumzia heshima inayoambatana na Uislamu, ambapo kafiri hana haki ya kuheshimiwa kutokana na ukafiri wake, lakini tumesema katika tafiti zetu, kwamba maneno haya hayakuja kuelezea hukumu hii katika hali zote, lakini imekuja kutoa ruhusa kwa Uislamu kutoiheshimu mali ya kafiri na nafsi yake na utu wake wakati wa vita tu, na huenda kauli yetu hii ikakubaliana na maneno ya Mwenyezi Mungu yasemayo:



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 26 1/7/2015 11:52:45 AM

لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ
وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا
إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ
الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ
وَظَاهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

**"Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga vita, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu anawakataza kufanya urafiki na wale tu waliowapiga vita, na wakawatoa makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanaowafanya hao marafiki basi hao ndio madhalimu."**
**(Qur'ani, 60:7-9).**

Kwa hakika dhahiri ya Aya hizi mbili ni kwamba kafiri ambaye hajatangaza vita dhidi ya Waislamu na wala hajawatoa kutoka nyumbani kwao, bali ikawa msimamo wake ni wa kutopambana dhidi ya utawala wa Kiislamu ambapo katika hali ya kawaida watu wanaishi ndani yake kwa kuelewana (bila ya kuwa ni dhimmiy au mwenye kusaini mkataba wa kuishi kwa amani katika nchi ya Waislamu), basi inastahili kuamiliana naye kwa wema kwa kupewa kila jambo lenye maslahi naye, na pia kuamiliana naye kwa uadilifu kwa maana ya ujumla, ambao unampa haki ya kuheshimiwa mali yake, nafsi yake na utu wake, na kutofanyiwa uadui isipokuwa kwa njia ya haki, na kwa mantiki hii ni kwamba, ukafiri si sawasawa na kutokuwa na heshima, bali vita ndivyo ambavyo vinapelekea hilo (kutowaheshimu wapiganaji wanaopigana dhidi ya Uislamu).

Na pia Aya hii inatufunza kwamba, kuwepo kwa tofauti katika Dini, hakutoi ruhusa ya kuvunja heshima ya wengine, kwani Mwenyezi Mungu amewalaumu Mayahudi kwa sababu ya kuwa na mwenendo huo. Na huenda baadhi ya wanachuoni wanaona kwamba, Aya hii haimaanishi zaidi ya wajibu wa kutekeleza amana na sio wajibu wa kuiheshimu mali, na sisi tunaona kwamba wajibu wa kutekeleza amana ni wa kufuata, kwa vile wajibu wa kutekeleza amana unahusiana na mambo ya kiitikadi, kwa mtu kurejesha amana kwa aliyempa amana, jambo hili linahusiana na ulazima wa kiitikadi, kwa hivyo sisi hatuoni kuwa kuna mafungamano kati ya maudhui ya Aya na kuacha kuiheshimu mali ya kafiri.

Na jawabu juu ya hilo, ni kwamba suala la amana halikutajwa katika Aya, kwa vile linahusiana na masuala ya kiitikadi, bali Aya imelenga katika kutaja tabia ya Mayahudi ambao si wenye kuheshimu mali ya watu wengine wasiokuwa Mayahudi, kwa mujibu wa kauli yake Mwenyezi Mungu: **"Haya ni kwa sababu walikuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma."** Kwa hakika hao Mayahudi wanaifanyia khiyana amana kwa misingi ya kutoiheshimu mali ya wengine, na sio kwa misingi kwamba wao hawajilazimishi kutekeleza amana kwa misingi ya kiitikadi. Iwapo Waislamu watafanya kama hivyo walivyokuwa wakifanya Mayahudi, nao watastahiki lawama, na huenda tukazingatia katika maudhui haya, kwamba kuna mafungamano ya kibinadamu kati ya watu werevu ya kutotumia mali ya mwingine pasi na haki, kwani suala la kuheshimu mali ni jambo takatifu kati yao, ambalo linajenga mahusiano yao kwa ujumla, ndio maana tukawaona wanawalaumu wale wanaokula mali za wengine kwa njia za dhulma na kuwaadhibu wezi, na wala hawaachi mwenendo huu, isipokuwa katika hali ya vita, bila ya kuwepo tofauti kati ya watu ambao wanafuata dini moja au dini nyingine.[10]

[10] Fadhlullahi: Muhammad Husein, Tafsir Min Wahyil Qur'ani, Jz.6, Uk.110.

# JE HESHIMA YA BINADAMU INAGAWANYIKA?

Miongoni mwa maneno yenye kasoro kubwa katika sehemu kubwa ya hotuba za Kiislamu, ni kusemwa kwamba heshima ya binadamu inagawanyika, na utukufu huo unawahusu Waislamu peke yao, asiyekuwa Mwislamu hastahiki kuheshimiwa, na haki hii hufinywa zaidi kwa madai kuwa haki hii anastahiki kupewa Muumini peke yake, na asiyekuwa yeye miongoni mwa watu wa madhehebu mengine na wazushi, hawastahiki kutukuzwa na kuheshimiwa, na ni halali kutokupewa baadhi ya haki za kimada na za kiroho. Licha ya kwamba Qur'ani imeeleza kwamba Mwenyezi Mungu amewapa heshima wanadamu wote, kama anavyosema:

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ
وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِمَّنْ
خَلَقْنَا تَفْضِيلًا

**"Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba." (Qur'ani, 17:70).**

Aya hii Tukufu iko ikielezea kutukuzwa kwa wanadamu wote na Mwenyezi Mungu, na haya ndio waliyoyasisitiza baadhi ya wafasiri walipoifasiri Aya hii Tukufu. Sayyid Muhammad Husein Tabatabai anasema: "Inadhihiri kwamba makusudio ya Aya ni kubainisha hali

ya wanadamu wote, na kufumbia macho ule utukufu wa Kiungu unaowahusu baadhi ya watu, jambo hili linawahusu wanadamu wote, washirikina, makafiri na mafasiki."[11]

Naye al-Alusiy Baghdadiy amesema: "**Tumemtukuza binadamu**: Maana yake ni kwamba, tumewafanya wote kuwa ni watu wa kutukuzwa, mwema wao na muovu wao, kwa maana utukufu na wema unawahusu wote bila ya kuwa na kikomo cha watu maalumu."[12]

Maelezo haya yaliyo wazi, yalikuwa iwe ndio msingi wa kufahamu baadhi ya maandiko, na kutolea fatwa baadhi ya hukumu za kisheria zinazohusiana na mafungamano juu ya watu wasio wa dini moja au madhehebu moja, na namna ya kuamiliana nao. Kwa kweli kauli iliyo mashuhuri ya wanachuoni ya kuhalalisha jihadi ya kuanza kuwapiga makafiri kwa sababu ya ukafiri wao, na si kwa sababu ya kuwafanyia uadui Waislamu, na kuwapa chaguo moja kati ya mambo mawili: Ama kusilimu au kuuwawa, isipokuwa kwa watu wa Kitabu, ambao wao wana chaguo la tatu, ambalo ni kutoa *jizya* (kodi), kauli hii inahitaji kufanyiwa tena utafiti.

Baadhi ya wanachuoni wamefanya utafiti mzuri juu ya maudhui haya, miongoni mwao ni Sheikh Muhammad Mahdiy Shamsuddin, katika kitabu chake kiitwacho *'Jihadul Umma*.' Katika utafiti wake huo amekuja na hitimisho la kwamba kisheria haifai kuanzisha jihadi. Natija hii imetokana na kuzijadili na kuzivunja dalili ambazo wanazitegemea wanachuoni mashuhuri.[13]

Pia maudhui yanayohusiana na unajisi wa mtu kafiri, ni jambo ambalo wanashikamana nalo wanachuoni wa madhehebu ya Kishia, na baadhi yao huwatoa Ahlul Kitabi (wanasema: Wao si najisi). Ama

[11] Tabatabai: Sayed Muhammad Husein, *al-Mizan fii Tafsiril Qur'ani*, Jz. 13, Uk. 152.

[12] Al-Alusiy Baghdadiy: Sayyid Muhammad Shukriy, *Ruhul-Maaniy fii Tafsiril Qur'ani*, Jz. 15, Uk. 117.

[13] Shamsuddin: Muhammad Mahdiy, *Jihadul Umma*.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 30 1/7/2015 11:52:45 AM

kuhusiana na wanachuoni wa Kisunni wao wanasema kwamba: "Hakika kafiri aliye hai ni tohara kwa sababu yeye ni binadamu, na binadamu ni tohara, ni sawa akiwa Mwislamu au kafiri, hii ni kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Kwa hakika tumemtukuza binadamu."** Na kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo: **"Hakika washirikina ni najisi,"** haina maana kwamba miili yao ni najisi, bali makusudio yake ni kwamba yaliyo najisi ni yale wanayoyaitakidi, na Mtume (s.a.w.w.) aliwahi kuwafunga mateka katika msikiti."[14]

Na baadhi ya wanachuoni wa Kishia wa zama hizi wanakubaliana na rai hii, kwa kusema kwamba kafiri yeyote si najisi, miongoni mwao ni kama vile Sayyid Fadhlullahi na Sheikh Makarimu Shiraziy, pale aliposema katika kusherehesha kitabu kijulikanacho kwa jina la '*al-Ur-watul Wuthqaa'*: "Hakuna dalili juu ya unajisi wa makafiri, ama Ahlul Kitabi kwa mujibu wa riwaya nyingi zenye kukubalika ni watu tohara, na najisi yao ni pale wanaponajisika kwa najisi najisi za kawaida, na pia utohara wao umethibitishwa na baadhi ya Aya za Qur'ani. Na baadhi ya riwaya zinaonelea vyema kujiepusha na vile vilivyomo mikononi mwao kwa vile mara nyingi huwa ni vyenye kunajisika kwa najisi ya kimada. Kwa mujibu wa maandiko haya, kuna yale yanayoelezea juu ya utohara wao na yale yanayodhihirisha unajisi na yale yanayoelezea wajibu wa kujiepusha nao. Ama asiye Ahlul Kitabi, bila ya kuwepo ikhtilafu kati ya vigawanyo vyake, pia hakuna dalili juu ya unajisi wake, licha ya kuwepo dalili inayothibitisha utohara wake kwa mujibu wa mtirirko wa riwaya, basi itachukuliwa kwamba asili yao ni watu tohara."[15]

Na miongoni mwa maudhui ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti upya, ni suala la kuhalalisha kumsengenya Mwislamu asiyekuwa Mshia, kama lilivyo mashuhuri kati ya wanachuoni, kwani jambo

---

[14] Wizaratul Auqafi washuunil Islamiyya - Kuweit: *Al-Mausuatul Fiqhiyyah*, Jz. 35, Uk. 23.
[15] Shirziy: Nasir Makarim, *Taaliqatu Alaal- Ur-watul- Uthqaa*, Uk. 27.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 31 1/7/2015 11:52:45 AM

hili ni kuvunja haki ya kiroho. Kuna baadhi ya wanachuoni walioharamisha kusengenya Mwislamu hata kama si mfuasi wa madhehebu ya Kishia, miongoni mwao ni Mtafiti, Ardabiliy na Sheikh Akhundiy al-Khurasaniy katika kitabu kijulikanacho kwa jina la '*Kifayatul Usuli*.' Na Sheikh Muhammad Aswf al-Muhsiniy anasema: "Hakiki dhahiri ya riwaya zimeharamisha kumsengenya Muumini (Mshia) na kuruhusu kumsengenya asiyekuwa Mshia. Mimi ninasema: "Dhahiri ya Aya hii isemayo: **"Wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi,"** hukumu hii inawahusu wote, kwani mustalahi wa neno 'Muumini' wakati iliposhuka Qur'ani, ulikuwa na maana pana zaidi ikilinganishwa na ilivyo leo, na udugu uliotajwa katika Aya, hauwahusishi Waislamu maalumu, kwani maana ya ndugu, pia inamhusisha asiyekuwa Mshia, na kwa hakika imewajibishwa kujitenga dhidi ya watu wa bidaa, kwa sababu ya uzushi wao.

Na katika kitabu '*Jawahiru*' na vinginevyo, kuna dalili ya kuruhusu kumsengenya mwenye kudhihirisha maovu, eti kwa sababu asiyekuwa Mshia amedhihirisha uovu ulio mkubwa. Kwa kweli hii ni dalili ya kushangaza sana, kwani wasiokuwa Mashia hawaoni kwamba itikadi yao na matendo yao ni batili, mpaka ionekane kwamba ni wenye kuyadhihirisha hayo. Basi je, wanachuoni hawa watukufu wanatoa fatwa ya kuruhusu kusengenywa Muumini (Mshia) mwenye kukosea katika baadhi ya itikadi zake au matendo yake katika hali ya kujitahidi au kukalidi (kufuata fat-wa za Mujtahidi)? Na mwenye kudhihirisha madhambi ni yule mwenye kuyadhihirisha huku akijua kwamba anafanya maasi, na kwa ujumla, hakuna dalili ya matamshi inayoruhusu kumsengenya Mwislamu asiyekuwa Mshia.[16] Mfano wa hayo, ni ile fatwa inayoelezwa na wanachuoni juu ya kuruhusu kuwadhikisha madhimmiy na Ahlul-Kitabi wanaoishi katika dola ya Kiislamu, na kuwabinya zaidi, na mengi mengineyo

[16] Al-Muhsiniy: Muhammad Aswif, *Hududu Sharriati- al-Muharramatu*, Jz. 2, Uk. 77.

waliyoyaeleza kuhusiana na hukumu za kuamiliana na madhimmiy.

## NI IPI NAFASI YA FATWA KATIKA UBINADAMU?

Mmoja kati ya wanachuoni wa zama hizi aliulizwa kuhusiana na uhalali wa kuwasaidia wasiokuwa Waislamu, na wale wasiokuwa wafuasi wa madhehebu yake miongoni mwa Waislamu wakati wa majanga. Jawabu lake lilikuwa ni kukataa. Ibara kama hizi zinapelekea chuki na dharau kwa wasiokuwa Waislamu na watu wenye kutofautiana madhehebu. Yafuatayo ni maswali na majibu yalivyokuwa:

**Swali:** Mara nyingi hutokea majanga, na huwa vigumu kupambanua kati ya watu au kuwafahamu ya kwamba huyu ni Mwislamu au sio Mwislamu, basi je, inafaa kwa shirika la misaada kuwasaidia bila ya kuzingatia taarifa zao?

**Jawabu:** Tunaona kwamba, ni juu ya shirika la misaada kuwapa misaada Waislamu tu na kuwatatulia shida zao, na kutowapa misaada wasiokuwa Waislamu, ambao wao ni maadui wa Dini, hata kama watakufa njaa, au watakufa kwa sababu ya baridi au joto au mafuriko au kuangukiwa na kitu, kwani hiyo inazingatiwa kwamba ni adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya ukafiri wao na uzushi wao, kama ambavyo makafiri katika madola makubwa huwasaidia wale walio katika Dini yao, na kuwahusisha wale walio katika madhehebu yao na njia yao, na wala hawawapi Waislamu, ila pale wanapokuwa na tamaa kwamba wataachana na Dini zao, kama wanavyofanya Mashia na Manaswara. Ama itakapokuwa kuna uzito wa kuwatambua Waislamu, kama vile kukiwa na njaa kali, inafaa



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 33 1/7/2015 11:52:45 AM

asiyekuwa Mwislamu kula pamoja na Mwislamu au kupewa chakula pamoja nao au kupewa kitu kingine, ikiwa haitojulikana hali yake.

**Swali:** Itakapokuwa wengi wao si Waislamu, je inafaa kuwasaidia kwa sababu ya kuwepo Waislamu wachache?

**Jawabu:** Haifai kumsaidia asiyekuwa Mwislamu, si kwa sababu ya njaa au mafuriko au tetemeko, wala kumsaidia katika matibabu au mfano wake, bali msaada unawahusu Waislamu tu pindi watakapotambulikana, pindi patakapokuwa na mchanganyiko na kutojulikana, itafaa kumsaidia asiyekuwa Mwislamu pindi itakapokuwa haijulikani hali yake na akawa amechanganyikana na Waislamu, na kukawa na ugumu wa kuweza kuwapambanua.

**Swali:** Pindi waathirika watakapokuwa wengi wao ni watu wafanyao bidaa (wazushi), je inafaa kwa shirika la misaada la Kiislamu kuwasaidia?

**Jawabu:** Haifai kwa Waislamu kuwasaidia wasiokuwa Waislamu, kama vile Mashia, watu wanaozuru makaburi na watu wa dini za uzushi kama vile manaswara, maduruzi, makadiani, masikhi, maberelali, mabaathi na mfano wao. Ni kwa sababu watu hawa wanawapiga vita Ahlusunna na wanawatakia yale yanayowadhuru. Basi wakiwa katika hali hiyo, watakuwa si watu wanaostahiki kupewa msaada, na inazingatiwa yale yaliyowasibu miongoni mwa misiba au ukame au ugonjwa, kuwa hayo ni adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi haifai kuwasaidia, bali msaada uwahusishe wafuasi wa Ahlusunna waljamaa peke yao.

**Swali:** Je inafaa kuwapa Zaka watendao bidaa (uzushi), kwa lengo la kujikinga na shari zao au kwa ajili ya kuzizowesha nyoyo zao (ili wamili kwenye Uislamu)?

**Jawabu:** Ni wajibu kwa Mwislamu wa kiahlisunna kuwachukia

watendao bidaa na kuwadharau, kama vile Mashia, wasiofanya ibada, wenye kuzuru makaburi na maibaadhi, kama ilivyo wajibu kwa Mwislamu pindi hao wanapokuwa wengi katika nchi, kujitenga nao ili kusalimika na shari zao, ikiwa hatoweza au kupata namna yoyote ya kujitenga nao, hapo itafaa kujikurubisha kwao na kujikinga na shari zao kwa kuwapa sehemu fulani ya mali ya Zaka, hapo watazingatiwa kuwa wao ni wenye kuzoweshwa nyoyo zao.

**Swali:** Iwapo katika mji hakuna yeyote isipokuwa watenda bidaa, je hapo itafaa kuwasaidia?

**Jawabu:** Haifai kuwasaidia, kwani ndani yake kuna kuwatia nguvu katika imani zao na kudhihirisha uzushi wao, kwani watakapojiweza kihali, itakuwa ni fedheha kwa Ahlusunna, kwa hivyo ni juu ya Mwislamu wa kiahlusunna afanye kila awezalo ili kuwadhalilisha wazushi, na wala asiwaajiri na kuwatumikisha, na asitaamali nao kwa yale yenye kutia nguvu itikadi zao au kunyanyua vitegauchumi vyao, na wala wasinunue bidhaa zao, lakini wasipoweza kusalimika na shari zao, itafaa kuwapa kiasi ambacho kitawazuia maudhi yao.[17]

Kwa hakika mazungumzo kama haya ambayo ni mengi katika viwanja vya Waislamu, huja katika mfumo wa dua katika hotuba za Swala ya Ijumaa, ambapo Mayahudi wote, manaswara, makafiri na wale Waislamu wenye kutofautiana nao kimadhehebu, huombewa kuangamia, na wake zao kuombewa wabakie wajane na watoto wao wawe mayatima. Kwa kweli hotuba kama hizi ndizo zilizotengeneza mazingira ya ugaidi ambao umezisibu nchi za Kiislamu katika zama hizi na nchi nyinginezo katika ulimwengu, jambo ambalo limeichafua sura ya Uislamu na Waislamu.

Kwa hakika kuhalalisha damu ya wasiokuwa Waislamu na kuvifedhehesha viwiliwili vyao na kuvikata vichwa vyao, kisha kuji-

[17] *Hayghatul- Ighathatul- Islamiyyahul- Alamiyyah*, Maktabul Ahsai, 100 Suala wa Jawaba Fil Amalil Khayriy, Uk.7-12.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 35 1/7/2015 11:52:46 AM

fakharisha kwa kurikodi matendo hayo ya kinyama chini ya nembo ya Uislamu, na kuyasambaza katika vyombo vya habari vya kilimwengu, hayo ni matunda machungu yatokanayo na hotuba kama hizi. Katika matukio mengi ya kigaidi, ni kwamba magaidi huwauliza dini zao wale waliowakamata, ambaye ni Mwislamu, humuachia, na ambaye si Mwislamu huharakisha kumuua.

Na miongoni mwa mifano ya karibuni ya kigaidi, ni ile iliyoripotiwa na gazeti la *al-Hayat* la tarehe 7|12|2004, kuhusiana na kuvamiwa kituo cha utamaduni cha ubalozi wa Marekani katika mji wa Jiddah, mmoja wa wafanyakazi wake anayeitwa Abdul Qawiyy Abdul Muhsin alilielezea gazeti hilo namna alivyoishi katika hali ya wasiwasi, pale alipoulizwa na mmoja wa wavamizi, kuhusiana na dini yake, aliwaambia: "Mimi ni Mwislamu…, mimi ni Mwislamu." Basi mara wakamtaka asome Suratul Fatiha, aliweza kuisoma. Anasema hakuweza kuamini kwamba baada ya kuulizwa yeye, aliulizwa mtu aliyekuwa katika chumba huku wote wakiwa wamenyanyua mikono ya kusalimu amri, kisha ikaja zamu ya Mfilipino ambaye hakuwa Mwislamu, na mwenyewe alikiri kwamba si Mwislamu, basi mara wakamuua kwa risasi katika kichwa chake.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 36 1/7/2015 11:52:46 AM

# HESHIMA YA BINADAMU NI JAMBO LA KIASILI NA KIKANUNI:

Hakika katika kutafakari Aya isemayo: **"Kwa hakika tumemtukuza binadamu,"** inapasa kukubali kwamba kutukuzwa kwa binadamu ni jambo la msingi katika fikra na katika kanuni za kifiqhi, haifai kuziacha, isipokuwa kwa sababu maalumu ya kisheria na kwa dalili sahihi iliyo wazi.

Kutokana na asili ya jambo hili, mwanachuoni faqihi, Sheikh al-Muntadhiriy katika darasa zake za kifiqhi za ngazi za juu, (*Bahthul Khariji*) kuhusu heshima ya binadamu, amepinga kuhusisha hukumu hii kwa Muumini peke yake, na yaliyokuja katika darasa hiyo ni kama yafuatayo: "Hakika kuwadhulumu watu ni jambo lisilofaa kwa mujibu wa akili, na vilevile kwa mujibu wa Qur'ani na Sunna. Sisi tunaitakidi kwamba Qur'ani iliposema: **"Kwa hakika tumemtukuza binadamu,"** ni kwamba inakusudia wanadamu ni wenye kutukuzwa kwa sababu wao ni wanadamu. Basi panaposemwa kuhusu haki za binadamu, ni kwamba inakusudia kwamba binadamu ana utukufu wake na heshima yake kwa vile ni binadamu hata kama ni kafiri, kwani binadamu ni mwenye kuheshimiwa mbele ya Mwenyezi Mungu kutokana na dhati (asili) yake, na haya ndiyo yaliyobainishwa na Aya kwa uwazi. Na Imamu Ali (a.s.) anasema katika wasia wake aliomuandikia Malik al-Ashtar: "Watu wako wa aina mbili: Ima ni ndugu yako katika Dini au ni mfano wako katika maumbile." Basi kwa hivyo binadamu ana heshima yake kwa vile yeye ni binadamu.

Na katika kuharamishwa kutukanwa, vilevile inawezekana kutegemea Aya ifuatayo: Na wala msiitane kwa majina ya kejeli. **"Ni**

**uovu kutumia jina baya baada ya kwisha kuamini."** Haikuhusishwa kwa Mwislamu na Muumini. Mwenyezi Mungu anasema kwamba anachukia kuitana majina mabaya. Na anasema tena: **"Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao."** Haikuwekwa sharti la mtu kuwa Mwislamu, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaka kuwe na misingi ya kijamii iliyo salama, na wala watu fulani wasiwaite wengine kwa majina mabaya, hii vilevile ni hukumu inayowahusu wasiokuwa Waislamu, na kwa uchache inawahusu Waislamu wote, ni sawa wakiwa Waumini (Mashia) au wasio Waumini. Pindi mtakapoamini hamna haki ya kumvunjia heshima Muumini mwingine au kumvunjia heshima mtu asiyekuwa Muumini. Kinachopasa kwa imani ni mtu kuwa thabiti na wala asiseme maneno mabaya.

Kutukana ni jambo lenye kuchukiza katika nafsi ya Mwenyezi Mungu, ni sawa ikiwa aliyetukanwa ni Muumini au si Muumini. Kuna riwaya kutoka kwa Abu Basir inayosema: "Msiwatukane watu, kwani matokeo yake ni kuchuma uadui." Pia katika riawaya hii haihusishi Muumini au Mwislamu, bali inawahusisha watu wote. Inakataza kuwatukana watu wa aina zote, ila linaloweza kusemwa ni kwamba kumtukana Muumini ni jambo baya zaidi kuliko kumtukana asiyekuwa Muumini. Ni jambo maarufu, ambalo husemwa kwamba kumtukana Muumini na wale wenye kuheshimika, ni jambo baya zaidi kuliko watu wa kawaida wasio na tabia nzuri kwa mujibu wa mtazamo wa jamii."[18]

Tunaashiria hapa yale waliyoyaeleza wanachuoni juu ya kumwadhibu Mwislamu yeyote iwapo atamsingizia mtu uovu hata kama ni kafiri.[19] Na imepokewa ndani ya *Wasaili* kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) namna alivyomwadhibu yule aliyemsingizia mmoja kati ya madhimmiy.[20]

---

18 Baqii, Imadu Diin, *Taqriyratu darsi Ayatullahi Muntadhiriy, Biun-wani Huquqil Insaanil au Huquuqil Insanil Muumini? Annaz-atul Insaniyyatu wal Islaamu*.

19 Ibn Qudama, *al-Mughniy*, Jz. 12, Uk. 399.

20 *Al-Wasail*: Hadithi Na. 34560



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 38 1/7/2015 11:52:46 AM

# HOTUBA ZA KIDINI NA KUJISHUGHULISHA NA BINADAMU

Katika kuboresha mafungamano ya binadamu na Mola Wake, na kuhakikisha mwendelezo wake wa kumwabudu, na kwa ajili ya kujenga mambo ya kiroho katika nafsi ya binadamu, Uislamu umeweka sheria ya ratiba ya ibada, kama vile Swala, Funga, Hijja, Umra na alama nyingine za Kidini, kama kusoma Qur'ani, Dua, Dhikri na Tasbihi. Na wakati huo huo, mafunzo ya Uislamu yameelekeza katika kumtumikia binadamu na kuwanufaisha watu, kwa kuwalisha wenye njaa, kuwalea mayatima, kuwasaidia mafukara na wanyonge, kuwapa mahitaji wale wenye kuhitaji, kuwatembelea wagonjwa, kuwasaidia wenye kufikwa na majanga, na kila aina ya wema kuwafanyia wengine na kuwapatia huduma.

Na wakati tunaposoma maandiko ya Kidini, tunaona mahimizo yake yakiwa yanalingana kwenye pande hizi mbili, bali tunakuta katika maandiko mengi yanayoelezea ratiba ya ibada, kama vile Swala, Funga na mfano wake, ndani yake zinalenga kukuza misukumo ndani ya nafsi ya binadamu ya kuwatendea wema watu. Kama ambavyo baadhi ya ibada ni za kuwapa mali watu wengine, kama Zaka, Khumsi, Kafara na Dhahaya (Nyama iliyochinywa katika ibada ya Hijja). Hakika Qur'ani imeweka tofauti kati ya kufuata Dini kikweli na kuifuata kiuongo, tofauti hiyo ni namna binadamu anavyojishughulisha na kuwasaidia wanadamu wanyonge kama vile mayatima na masikini, na inazingatiwa kwamba kutekeleza ibada ya Swala bila kuwasaidia mayatima na mafukara, ni kufuata Dini kiuingo na kujionesha katika hali ya kujifedhehesha, Mwenyezi Mungu anasema:



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 39 1/7/2015 11:52:46 AM

أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالدِّينِ فَذَٰلِكَ الَّذِي يَدُعُّ الْيَتِيمَ وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ الْمِسْكِينِ فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونَ

**"Je! Umemuona anayekadhibisha Malipo? Huyo ni yule ambaye humsukuma yatima. Wala hahimizi kumlisha masikini. Basi, ole wao wanaoswali. Ambao wanapuuza Swala zao. Ambao wanajionesha. Na huku wanazuia msaada." (Qur'ani, 107: 1-7).**

Na pia kuhusiana na kuwajibishwa kwa ibada ya Hijja, Qur'ani inaashiria kwamba matendo ya ibada hii yanalenga kuwanufaisha watu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

لِيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ

**"Ili washuhudie manufaa yao." (Qur'ani 22:28).**

Na kuna riwaya zinazoashiria kipengele cha ubinadamu katika ibada ya Funga, ambacho ni kuwakumbuka wenye njaa na wenye mahitajio. Imamu Husein (a.s.) aliulizwa: Kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu amefaradhisha ibada ya Funga? Alijibu: "Ili tajiri apate hisia ya njaa, aweze kuwasaidia masikini."[21] Na kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq (a.s.) amesema: "Ama sababu ya kufaradhishwa kufunga, ni kwamba tajiri na fakiri wawe sawa, hiyo ni kwa sababu tajiri hapatwi na hisia ya njaa akaweza kumsaidia fakiri, kwa sababu tajiri kila anapotaka kitu hukipata. Basi Mwenyezi Mungu Mtukufu akataka kuweka sawa kati ya waja Wake, na amuonjeshe tajiri

[21] Al-Majlisiy: Muhammad al-Baqir, *Biharul An-wari*, Jz, 93, Uk. 375.

muonjo wa njaa na maumivu ili amhurumie mnyonge na mwenye njaa."[22]

Na Qur'ani Tukufu inaeleza kwamba kipimo cha wema sio tu kutekeleza nembo za ibada, huku ikisisitiza kwamba wema hupatikana katika imani na kuwapa msaada wengine pamoja na ratiba za kiibada, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ
وَالْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ
ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ
وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ
وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا

**"Sio wema kuelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi tu. Bali wema ni wa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali kwa kuipenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ukombozi wa watumwa, na akasimamisha Swala na akatoa Zaka, na wanaotimiza ahadi zao wanapoahidi." (Qur'ani 2:177).**

Hakika inalazimika kuikata Swala kwa ajili ya kuokoa maisha ya binadamu kutokana na hatari. Na inalazimika kwa mwanamke mjamzito kutokufunga ikiwa Funga yake itamsababishia madhara mtoto wake aliyeko tumboni, au kumsababishia shida mtoto anaye-

[22] Kitabu kilichotangulia.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 41 1/7/2015 11:52:46 AM

nyonya kwa kukosa maziwa ya kutosha. Na wala si wajibu kwa mtu kutekeleza ibada ya Hijja, pindi anapokuwa anadaiwa haki za watu za kimali, bali ibada yake hiyo haitokubaliwa ikiwa ataitekeleza huku akiwa na deni.

Na Hadithi mbalimbali zinaashiria juu ya umuhimu na ubora wa kutoa huduma kwa watu, kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema: "Viumbe ni familia ya Mwenyezi Mungu, basi mbora wa viumbe mbele ya Mwenyezi Mungu, ni yule mwenye kuinufaisha familia ya Mwenyezi Mungu."[23] Na Mtu mmoja alimwambia Mtume (s.a.w.w): "Napenda niwe mbora wa watu." Mtume (s.a.w.w.) akamwambia; "Mbora wa watu, ni yule mwenye kuwanufaisha watu, basi kuwa mnufaishaji wao."[24] Na pia kutoka kwake (s.a.w.w.) amesema: "Mambo mawili hayana kitu kilicho bora zaidi juu yake: Kumuamini Mwenyezi Mungu na kuwanufaisha waja wa Mwenyezi Mungu."[25]

Na imepokewa kutoka kwa Imamu Muhammad al-Baqir (a.s): "Kuihudumia nyumba ya watu walio Waislamu, kwa kuwalisha, kuwavisha na kuzizuia nyuso zao na watu (kuwawezesha ili wasiombe), jambo hili ni bora mno kwangu kuliko kufanya ibada ya Hijja kisha kufanya ibada ya Hijja na mfano wake na mfano wake mpaka zifikie kumi, na mfano wake na mfano wake mpaka zifikie sabini."[26]

Na kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq (a.s.) amesema: "Naapa kwa ambaye alimpeleka Muhammad kwa haki hali ya kuwa ni mbashiri na muonyaji, hakika kumtatulia shida Mwislamu na kumliwaza kutokana na msiba wake ni jambo bora zaidi kuliko kuhiji na kutufu na kuhiji na kutufu mpaka zikafikia kumi." Kisha Imamu (a.s.) aliu-

---

23 Al-Hindiy: Ali al-Muttaqiy, *Kanzul Ummal*, Hadithi Na. 16171.

24 Kitabu kilichotangulia, hadithi Na. 44154.

25 Al-Majlisiy: Muhammad Baqir, *Biharul An-war*, Jz. 74, Uk. 137.

26 Kitabu kilicotangulia, Jz. 71, Uk. 329.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 42 1/7/2015 11:52:46 AM

nyanyua mkono wake na akasema: "Mcheni Mwenyezi Mungu na wala msiache kutenda kheri na wala msiwe wavivu, kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake ni wenye kujitosheleza kutokana na nyinyi na kutokana na amali zenu, na nyinyi ni wahitaji mnaomhitajia Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaka hiyo iwe ni sababu ya kuwaingiza Peponi kutokana na huruma Yake."[27]

Msisitizo huu ambao tunaukuta katika maandiko ya Kidini yanayohimiza juu ya kuwatumikia watu na kuwanufaisha, hatuyaoni yakiakisi kama yalivyo katika hotuba za Kidini, Dini ambayo mara nyingi inasisitiza juu ya masuala ya wanadamu, huenda haya yakawa ni matokeo ya uchache wa kujishughulisha na kazi za misaada ya kibinadamu katika jamii zetu za Kiislamu ikilinganishwa na jamii nyingine, pia kutoliangalia jambo hili kwa mtazamo wa kina katika jamii zetu. Katika jamii za watu wengine kunaundwa mashirika yenye kufanya kazi za kuwasaidia watu, mashirika ambayo ni ya kilimwengu, kama vile shirika la haki za binadamu, ulinzi wa mazingira, madaktari wasio na mipaka, mashirika yenye kusaidia nchi zilizokumbwa na majanga, shirika la kuwalinda walemavu, na mashirika yenye kujishughulisha na magonjwa ya hatari, kama vile, ukimwi na saratani.

Kwa hakika hotuba zetu za Kidini, zinahitaji sana kujishughulisha na kadhia za kibinadamu, ili kukusanya nguvu kwa ajili ya kutatua shida na mahitajio ya maisha katika jamii zetu ambazo zinasibiwa na ujinga, ufakiri na ukosefu wa huduma. Hakika watu katika jamii zetu kuelekeza nguvu zao katika kujenga misikiti, hazilingani na ujenzi wa vyuo vikuu na maktaba. Na kwenda Hijja na Umra mara kwa mara, hakulingani na kuwalea mayatima na kuwasaidia walemavu. Na watu wengine kuharakia kwenda kwenye Swala ya

[27] Kitabu kilichopita, Jz. 71, uk. 329.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 43 1/7/2015 11:52:46 AM

jamaa, hakulingani na kuharakia katika kujishughulisha na mambo mengine.

Na kwa hakika tumeona namna jamii za Ulaya zilivyokabiliana na janga la Sunami, ambalo lilizikumba nchi za Asia ya Kusini mnamo mwaka 2005 A.D., ambapo maelfu ya watu walipoteza maisha, na mamilioni kukosa makazi, na kuangamiza maelfu ya vijiji na miji, basi watu wa Ulaya walikimbilia kwa haraka kuwasaidia. Kwanza walianza kuwasiliana na mashirika ya misaada ya kibinadamu, na kwa mfano msaada uliokusanywa ndani ya dakika moja katika nchi ya Uingereza ulifikia Paundi 15,000, hii ni kwa mujibu wa shirika la habari la Uingereza (B.B.C.), na kwa mujibu wa gazeti, ni kwamba kwa muda wa saa moja, palipatikana mchango wenye thamani ya Paundi 1,000,000, mbali ya msaada wa vitu, kama vile nguo, chakula na dawa. Na vituo vyote vya televisheni walianzisha akaunti maalumu kwa ajili ya kukusanya misaada, na mamia ya mitandao ya intaneti ilijitolea kutoa taarifa za watu waliopotea wa jinsia mbalimbali.

Katika wakati ambao jamii za Kiislamu zilikuwa zimetulia, na baya zaidi ya hilo, ni kutolewa baadhi ya hotuba kutoka kwa baadhi ya mirengo ya Kiislamu yenye kufurahia hali iliyowasibu watu wa mataifa hayo, kwa kusema kwamba, hayo yaliyowasibu ni adhabu inayotoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu ya uovu wa watu wa nchi hizo, hali hii inadhihirisha ugumu katika hisia za kibinadamu, basi hakuna budi kutolewa mafunzo ya Kiislamu ya kiasili ambayo yanaamsha hisia na msukumo wa kheri na mapenzi katika nafsi ya kila Mwislamu, bali kwa kila kiumbe hai, kama ilivyokuja katika Hadithi: "Kwa kila kiumbe chenye kiu (kunywesha maji kiumbe chochote) kuna malipo."[28]

[28] Ibn Hanbal: Imamu Ahmad, *Musnadul Imami Ahamd ibn Hanbal*, Hadithi Na. 17724.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 44 1/7/2015 11:52:46 AM

# HAKI YA MWENYEZI MUNGU NA HAKI ZA BINADAMU:

Ujumbe wa Mwenyezi Mungu umekuja kumuongoza binadamu katika kutekeleza haki za Muumba Wake, kwa kumtambua, kumuamini, kumuabudu na kumtii. Hili ni la kwanza, na jambo la pili ni kumuongoza katika kutekeleza haki za watu, kwa lengo la kupangilia maisha ya kijamii kati ya wanadamu. Baadhi ya Aya za Qur'ani Tukufu zinaangazia lengo hili, kama ndio msingi madhubuti wa Ujumbe wa Mitume, Mwenyezi Mungu anasema:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili za waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu." (Qur'ani 57:25).**

Kama ambavyo pia baadhi ya Hadithi zinaashiria ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anakasirishwa zaidi na uvunjwaji wa haki za watu kuliko kuvunjwa haki ya kuabudiwa Kwake na kutiiwa Kwake, isipokuwa katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, imepokewa kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema: "Dhulma iko ya aina tatu: Dhulma isiyosamehewa na Mwenyezi Mungu, na dhulma yenye kusamehewa na Mwenyezi Mungu, na dhulma asiyoiacha. Ama dhulma isiyosamehewa na Mwenyezi Mungu ni ushirikina, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: **"Haki-**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 45 1/7/2015 11:52:46 AM

**ka ushirikina ni dhulma iliyo kubwa mno."** Ama dhulma yenye kusamehewa na Mwenyezi Mungu ni dhuluma wanayojidhulumu waja wenyewe kati yao na Mola wao, na ama dhulma asiyoiacha Mwenyezi Mungu, ni waja kudhulumiana wenyewe kwa wenyewe, mpaka wao wenyewe watakapolipana."[29]

Na kama hivi imekuja kutoka kwa Imamu Ali (a.s.) katika kitabu cha *Nahjul Balaghah* akisema: "Tambueni kwamba dhuluma iko ya aina tatu: Kuna dhuluma isiosamehewa, na dhuluma isioachwa, na dhuluma yenye kusamehewa, isiyotakiwa. Ama dhuluma isiyosamehewa ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: **"Kwa hakika Mwenyezi Mungu hasamehe akishirikishwa."** Ama dhulma ambayo husamehewa ni dhulma ya mja kujidhulumu nafsi yake kwa kutenda baadhi ya maasi madogo madogo. Ama dhulma ambayo haiachwi, ni waja kudhulumiana wao kwa wao. Huko (Kiyama) kisasi ni cha nguvu sana, sio jeraha kwa kisu wala kipigo kwa mjeledi, lakini ni ngumu mno kwa kuwa vitu vyote hivi si chochote ukivilinganisha na (adhabu) ya huko." [30]

Kuna maandiko mengi ya Kidini yanayotahadharisha dhidi ya kutoziheshimu haki za wengine, kama kauli yake Mwenyezi Mungu: **"Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu." "Na wala msifanye uadui, hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kufanya uadui."** Na pia imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Iogopeni dhulma, kwani hiyo ni giza la Siku ya Kiyama."[31] Lakini tunachokishuhudia katika hotuba za Kidini, ni msisitizo juu ya haki za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kutokuwepo msisitizo juu ya haki za binadamu.

---

[29] Al-Hindiy: Ali Muttaqiy, *Kanzul Ummal*, Hadithi Na. 7588.

[30] Sharifu Radhiy: Nahjul Balaghah, Khutba Na. 176.

[31] Al-Hindiy: Ali Muttaqiy, *Kanzul Ummal*, Hadithi Na. 7598.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 46 1/7/2015 11:52:46 AM

Na pia utakuta katika tafiti za kifikra za kiitikati na kifiqhi za kiibada zikiwa zimejaa katika maktaba za Kiislamu, kama vile hukumu za Swala, Funga na Hijja, tafiti hizi ziko katika mijaladi (juzuu) mingi, na zikiwa katika milango mbalimbali na sura tofauti, hata kufikia katika sura za kudhania na kutarajia, lakini masuala ya haki za binadamu hayakuzungumziwa katika anuani maalumu katika mambo ya kifikra (kiitikadi) wala katika mambo ya kifiqhi, na wala hayakuzungumziwa isipokuwa juu juu tu ndani ya milango tofauti ya kifiqhi.

Na katika kiwango cha hotuba na kuelimisha, ni kwamba mara nyingi mahatibu huhimiza juu ya utekelezaji wa nguzo za ibada zilizo wajibu kisheria, na kutahadharisha dhidi ya kutenda dhambi na maasi yanayohusiana na upande wa mtu binafsi, kama vile kuzini, kunywa ulevi na wanawake kutovaa hijabu, lakini mazungumzo yanayohusiana na kuvunja haki za kisiasa, kijamii na kifikra ni kidogo sana.

Na pindi walinganiaji wa Kiislamu wanapoona watawala hawajishughulishi na mambo ya Kidini, kama vile Swala au Funga, au pindi wanapotenda baadhi ya maasi, kama vile kuzini, kutojisitiri na mengineo, hapo husimama Kiyama chao na wala hakitosita (kushambuliwa kwa maneno makali), lakini mahatibu hao hawalipi umuhimu suala la kuvunjwa kwa haki za wananchi, au kukosekana kwa uadilifu, au kudharauliwa maslahi ya watu na mahitajio yao.

Hakika wao hukasirika kwa kumuona mwanamke asiyejisitiri, lakini wanafumbia macho hali ya ufakiri na unyimwaji wa haki za watu, na hukasirishwa sana na wale wanaokula waziwazi katika mchana wa mwezi wa Ramadhani, lakini hunyamazia kimya hali ya kuenea kwa ufisadi wa kisiasa na kiuchumi. Na pindi wanapoanzisha kikundi cha kuamrisha mema na kukataza mabaya,



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 47 1/7/2015 11:52:46 AM

hakika mipaka ya mambo mema na mambo maovu kwao hayajumuishi mambo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, bali ni yale tu yanayohusiana na mambo ya kiibada na kukhalifu mambo ya kisheria yanamuhusu mtu binafsi.

Kasoro hii katika hotuba za Kidini, ni moja ya udhaifu wa wazi kuhusiana na mambo ya kibinadamu wakati wanapotoa hotuba za namna hii.

# KUVUMILIA UNYONGE AU KUDHALILIKA?

Katika mafungamano ya kiijamii, kuna yule ambaye yuko katika nafasi ya juu, na yule aliye katika hali ya chini, na mara nyingi hutokea kudhulumiwa yule aliye katika hali ya pili (mnyonge). Ndio maana mafunzo ya Kidini yakatahadharisha wale wenye nguvu dhidi ya kuwaonea wengine, kama vile mtawala asiwadhulumu raia wake, mume asimdhulumu mke wake, baba asiwadhulumu watoto wake, tajiri asimuonee fakiri, na mkuu wa kazi asiwadhulumu wafanyakazi wake.

Ni sahihi kwamba kuna kundi ambalo linatakiwa lifanye subira, lakini subira hiyo isifikie kiwango cha kuishusha heshima yake na utu wake. Kama ambavyo kwamba, kuna mafunzo na sheria zinazohimiza juu ya kupigania haki na kuyahami maslahi yaliyo katika sheria.

Na tunaloliona hapa katika hotuba za Kidini, ni kwamba mara nyingi zinaelekeza katika unyonge na kujidhalilisha kwa wenye nguvu, kwa kusisitiza kuwepo haki za mtawala juu ya raia wake, mke juu ya mume wake, baba juu ya watoto wake na mkuu wa kazi juu ya wafanyakazi wake, kama ambavo hotuba zao zinavyosisitiza kwa raia, mke, watoto na wafanyakazi kutozembea katika kutekeleza haki zao kwa upande wa pili.

Ama kutahadharishwa mtawala dhidi ya kuwadhulumu raia, na mume kumdhulumu mke wake, na baba kuzembea juu ya haki za watoto wake na mkuu wa kazi kuwadhulumu wafanyakazi wake, au pia kuwaelimisha watu juu ya haki zao, na kuwaelekeza njia bora ya kuzipata haki zao na kuzipigania, ni jambo la nadra kuzungumzwa katika hotuba za Kidini!



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 49 1/7/2015 11:52:46 AM

# UBORESHAJI WA HOTUBA KWA AJILI YA BINADAMU:

Hakika uboreshaji wa hotuba za Kidini kwa ajili ya maslahi ya binadamu, sio matakwa kwa ajili ya ukamilifu wake, na wala sio jambo la kijuu juu, bali ni jambo lenye umuhimu wa hali ya juu, jambo ambalo liko katikati ya mambo yanayowahusu watu na wanalolihitaji mno. Kwa kweli jambo hili ni njia inayothibitisha kupatikana mambo ya kimsingi, ambayo watu wamechelewa sana kuyapata, miongoni mwayo ambayo ni muhimu zaidi ni kama yafuatayo:

**Kwanza:** Kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo ya kibinadamu katika jamii zetu, kwani leo binadamu anaishi katika hali mbaya, akiwa anakosa mbinu ya kujenga maisha bora, na kukosa kustarehe na haki zake za kibinadamu kwa mujibu wa sheria.

**Pili:** Kuwa na mafungamano pamoja na wengine ndani ya umma na ndani ya nchi, na pia nje ya nchi pamoja na watu wengine na tamaduni mbalimbali, kwani jamii zetu zinasibiwa na tatizo la kuwepo mafungamano na vikundi vingine vya watu, kwani umma umeingizwa katika vita vyenye kulenga kuwazuia kuamiliana pamoja na tamaduni nyingine na mataifa mengine kwa sababu ya ugaidi.

**Tatu:** Kuchangia katika kuhudumia masuala ya kibinadamu katika kiwango cha ulimwengu, ili umma uwe sambamba na yale yanayolinganiwa na Uislamu, kama vile tabia njema, mafunzo na kaulimbiu za Ujumbe wake Mtukufu.

Hakika Qur'ani Tukufu inautangaza Uislamu kuwa ni Dini inayojishughulisha na mambo ya kibinadamu kwa ujumla, inasema:



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 50 1/7/2015 11:52:46 AM

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ

**"Na hatukukutuma ila kwa watu wote…" (Qur'ani 34:28).**

Na Ujumbe, rehema na amani ni kwa mataifa yote ulimwenguni, inasema:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

**"Na hatukukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu wote." (Qur'ani 21:107).**

Na umma wa Kiislamu unapaswa kuwa ndio muongozaji wa mambo mema katika jamii yote ya kibinadamu, kama Qur'ani inavyosema:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

**"Mmekuwa ni umma bora uliotolewa kwa watu…" (Qur'ani 3:110).**

Basi hakuna budi kutolewa hotuba zenye kuelekeza majukumu haya, na kuutangaza Uislamu katika ulimwengu katika nafasi hii.

# WANAHARAKATI WA KIISLAMU NA HAKI ZA BINADAMU

Haiwezekani kwa mtafiti yeyote yule aliye mwadilifu ambaye atatafiti maandiko na sheria za Kiislamu, kukataa namna fikra na sheria za Kiislamu zilivyojishughulisha zaidi na masuala ya haki za binadamu, kiasi ya kuifanya Dini hii kuwa ndio ya mwanzo na inayojishughulisha zaidi na jambo hili kuliko dini nyingine na shule nyingine zikiwepo nchi za Kimagharibi katika zama hizi. Tokea karne kumi nyuma kabla ya kusainiwa maazimio ya haki za binadamu katika nchi za Ulaya, Aya mbalimbali za Qur'ani Tukufu zimesisitiza juu haki za binadamu na kulindwa haki zake za kimada na kiroho, na kuzingatia kwamba namna yoyote ile ya uvunjaji wa haki hizi ni kumfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Dini Yake na Mtume Wake, na hali hiyo inastahili kupata ghadhabu za Mwenyezi Mungu na hasira Zake na adhabu Yake.

Qur'ani Tukufu inazingatia kwamba kuyafanyia uadui maisha ya mtu mmoja yeyote yule ni sawa na kuwafanyia uadui watu wote na kuwatoa uhai wao, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

مِنْ أَجْلِ ذَٰلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 52 1/7/2015 11:52:46 AM

**"Kwa ajili ya hayo tukawaandikia wana wa Israil ya kwamba atakayeua nafsi isiyoua nafsi au kufanya ufisadi katika ardhi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kuiokoa ni kama amewaokoa watu wote." (Qur'ani 5:32).**

Kwa kweli heshima, ni haki ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa kila binadamu kwa vile tu yeye ni binadamu, bila ya kuangalia wasifu mwingine, kama anavyosema: **"Kwa hakika tumemtukuza binadamu…" (Qur'ani)** Na pia Qur'ani inasisitiza juu ya uhuru wa mawazo na itikadi kwa binadamu, inasema: **"Basi anayetaka aamini, na anayetaka akufuru." (Qur'ani)**.

Na hata Mitume ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hawana haki ya kutumia nguvu yeyote ya kulazimisha imani fulani, na kazi yao inabakia kuwa ni kulingania na kufikisha Ujumbe tu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيْطِرٍ

**"Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatenza nguvu." (Qur'ani 88:21-22).**

Na anasema tena Mwenyezi mungu Mtukufu:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَآمَنَ مَنْ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا
أَفَأَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

**"Angelitaka Mola Wako wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?" (Qur'ani 10:99)**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 53 1/7/2015 11:52:46 AM

Na katika kipengele cha kulinda haki za kimada, Qur'ani Tukufu inatoa onyo kali kwa mwenye kunyang'anya kitu katika mali za wengine, kwa mfano kupora mali ya yatima, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا

**"Hakika wanaokula mali ya mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula moto matumboni mwao, na wataingia Motoni." (Qur'ani 4:10).**

Na pia anasema kuhusiana na haki za kiroho:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَبْ بَعْضُكُمْ بَعْضًا

**"Enyi Mlioamini jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi." (Qur'ani 49:12).**

Na kuna mamia ya Hadithi za Mtume (s.a.w.w.), ambazo wanachuoni wamezielezea kwamba ni sheria ya Uislamu iliyowekwa ili kulinda haki za binadamu za kimada na kiroho, kama vile sheria ya kisasi na fidia, na shughuli za kijamii, na ratiba za tabia njema na malezi. Na kuziorodhesha Hadithi zote zinazoelezea haki za binadamu, ni jambo linalohitaji utafiti wa kina, lakini ninalotaka kulijadili hapa, ni nafasi ya wanaharakati wa Kiislamu katika kutetea na kupigania haki za binadamu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 54 1/7/2015 11:52:47 AM

# UKWELI JUU YA KUJISHUGHULISHA NA HAKI ZA BINADAMU:

Wanaharakati wengi wanajifakharisha mbele ya tamaduni za Kimagharibi kwamba Uislamu ulitangulia katika kujishughulisha na haki za binadamu, na kwa hakika hili ni jambo la kweli kwa mujibu wa maandiko matakatifu na mafundisho ya hukumu za kisheria. Ama katika kiwango cha utekelezaji, inapasa kukiri kwamba kuna upungufu na kuzembea, na wengine (wasiokuwa Waislamu) wametutangulia na kutupita kwa masafa ya mbali sana. Inawezekana kuelezea baadhi ya namna sisi (Waislamu) tulivyochelewa katika kadhia ya haki za binadamu, katika maelezo yafuatayo:

**1.** Kuchelewa upatikanaji wa azimio maalumu la kifundi linalohusiana na kadhia ya haki za binadamu. Hii ni kwa sababu mara nyingi maandiko ya Kidini hayaliweki jambo hili kuwa ni lenye kupasa kutekelezwa na watu wote, hii ni kwa mujibu wa wanachuoni wanavyoyatolea tafsiri, na kutofautiana rai zao juu ya utekelezwaji wake. Na hata fatwa za kisheria za wanachuoni zinazohusiana na haki za binadamu mara nyingi zinabainisha hukumu zinazohusiana na Mwislamu binafsi.

Ama hatua za kimaendeleo zilizopigwa katika jamii za watu wa Magharibi, ni kuwepo azimio la kifundi lililo wazi linalohusiana na haki za binadamu, azimio ambalo linatoa ulazima wa utelelezwaji wake katika kiwango cha sehemu maalumu au kimataifa. Kwa mfano, baada ya kutokea mapinduzi katika nchi ya Ufaransa, kikao cha Bunge kilichofanyika tarehe 26, Agosti 1789, kilitangaza haki za binadamu na za raia katika vipengele kumi na saba, vikizungumzia haki na uhuru, na wakati ilipotolewa katiba ya Ufaransa,



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 55 1/7/2015 11:52:47 AM

mwaka 1791, kadhia hii ilikuwa ni sehemu ya katiba hiyo. Na katika katiba ya mwaka 1793, ambayo ilipitishwa na kikao cha Bunge, vilizidishwa vipengele vingine vinavyohusiana na haki za binadamu na za raia, ambazo zilikuwa zinahusiana na masuala ya kiuchumi na mambo ya kijamii. Basi katiba yao hiyo ikawa na vipengele thelathini na tano, miongoni mwa vipengele mia moja na ishirini na nne vya katiba yote.

Na baada ya kuanzishwa Umoja wa Mataifa, mkutano wake mkuu uliofanyika tarehe 10 Disemba, 1948, kwa kauli moja ulitangaza utekelezaji wa haki za binadamu kwa ulimwengu mzima, na azimio hilo lina vipengele thelathini, kisha vikafuatiwa na makubaliano mawili:  La kwanza, linahusiana na haki za kiuchumi na kijamii na kitamaduni, na la pili, ni kuhusiana na haki za raia na kisiasa. Hili la pili lilikuwa ni makubaliano ya hiyari. Maazimio haya yalifanyika tarehe 16 Disemba, 1977.

Ama katika mwelekeo wa Kiislamu, licha ya kuwepo vipengele visivyokubalika katika maazimio ya Umoja wa Mataifa juu ya haki za binadamu, katika mwaka 1979, kulianzishwa fikra ya kutoa maazimio ya Kiislamu juu ya haki za binadamu, fikra iliyoanzishwa na Mkutano wa Nchi za Kiislamu, ambapo mkutano huo wa kumi uliofanywa na mawaziri wa mambo ya nje ulikubaliana juu ya kuundwa kamati ya ushauri inayowahusisha wataalamu wa haki za binadamu, kutengeneza vipengele vinavyohusiana na haki za binadamu katika Uislamu. Suala hilo lilipewa mkutano wa kumi kulisimamia, ambapo mkutano huo ulilikabidhi kwa kamati ya Kisheria. Na katika mkutano wa tatu wa wakuu wa nchi hizo, ilitolewa hati ya suala hilo, lakini mkutano huo nao ukalihawilisha suala hilo kwa kamati nyingine. Na katika mkutano wa kumi na nne wa mawaziri wa mambo ya nje uliofanyika Dhaka, ulikubaliana na utangulizi wake na kipengele chake cha kwanza, na vipengele vilivyobakia vikaachi-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 56 1/7/2015 11:52:47 AM

wa kamati ya tatu, kisha kukafuatiwa na mikutano iliyosisitiza juu ya kadhia hiyo, mpaka pale palipofanywa mkutano mwezi wa Disemba mwaka 1989 katika mji wa Tehran, ambao ulitayarisha hati ya mwisho, ambayo ilikubaliwa na mawaziri wa mambo ya nje katika mkutano wao wa kumi na tisa uliofanyika Cairo. Hivi ndivyo hati ya haki za binadamu ilivyopita katika mikutano kumi ya mawaziri wa mambo ya nje. Ulianzia Fasi, Islamabad, Baghdad, Niyami, Dakka, Sanaa, Amman, Riyadh, Tehran na kumalizikia Cairo. Na mikutano mitatu ya wakuu wa nchi hizo, ulianzia Taif, Darul Baydhaa na kumalizikia Kuweit. Na kulifanyika vikao mbalimbali vya wataalamu. Kizazi hiki kigumu cha kukubali haki za binadamu za Kiislamu kilichukua muda wa miaka kumi. Ama dola hizo za Kiislamu kufikia kiwango cha utekelezaji kivitendo azimio hili, inahitajika miaka mingine kumi!!

**2.** Uchache wa kujishughulisha na kadhia ya haki za binadamu katika hotuba za Kiislamu: Kitu tunachokikuta kikipewa umuhimu mkubwa ni masuala ya Kiakida na Kiibada, na hata masuala ya kisiasa yamepata nafasi ya kuzungumzwa katika hotuba za Kiislamu za zama hizi, lakini suala la haki za binadamu halijafika kiwango kikubwa cha kupewa kipaumbele isipokuwa ni kidogo mno. Mara nyingi huzungumza pale anapotokea mtu na kudai kwamba Uislamu umefumbia macho suala la haki za binadamu, na kujifakharisha namna Uislamu ulivyoliweka suala la haki za binadamu, au huzungumzwa pale wanaharakati wanaponyimwa haki zao, basi hutaka wapatiwe haki zilizokubaliwa katika maazimio ya haki za binadamu.

**3.** Mipaka ya kutetea haki za binadamu iliyowekwa na wanaharakati wa Kiislamu: Kumeasisiwa mashirika na kamati nyingi katika kiwango cha kitaifa na kimataifa zinazoshughulikia haki



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 57 1/7/2015 11:52:47 AM

za binadamu, lakini waanzilishi na wale wenye kuchangia kazi hii wengi wao sio Waislamu. Na kwa upande wa Kiislamu, hakujaanzishwa harakati za kutetea haki za binadamu, isipokuwa katika miaka ya hivi karibuni, kwa ajili ya kukabiliana na dhulma na ugandamizaji unaowasibu wanachama waliojiunga na harakati hizo. Na mara nyingi taasisi hizo za Kiislamu hujishughulisha zaidi na yale yanayowasibu wanachama wake na wala hawawajali watu wengine.

**4.** Ripoti nyingi za uvunjaji wa haki za binadamu zinazotolewa mara kwa mara, mara nyingi zinazonesha uvunjwaji wa haki za binadamu hufanywa na nchi za Kiislamu, hii ni kwa sababu ya kukita uvunjwaji wa haki hizo kwa viwango mbalimbali. Na uvunjwaji wa haki za binadamu katika nchi za Kiislamu, haufanywi tu na watawala, bali baadhi ya mila katika jamii hizo zinabeba uvunjaji wa wazi wa haki za binadamu, kama vile katika mafungamano ya kifamilia na katika mafungamano pamoja na makundi mengine katika jamii.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 58 1/7/2015 11:52:47 AM

# KWA NINI UNAFUMBIWA MACHO UVUNJWAJI WA HAKI ZA BINADAMU?

Kuna masafa yaliyopishana sana kati ya namna Uislamu ulivyojishughulisha mno katika kadhia ya haki za binadamu kupitia sheria, na namna Waislamu, na hasa wanaharakati wa Kiislamu walivyoipuuzia kadhia hii. Basi hutolewa baadhi ya mawazo juu ya kile kilichosababisha kuwepo mtengano huu. Nami ninatoa baadhi ya sababu hizo kama ifuatavyo:

Mazoea ya Kielimu, ni kwamba mafunzo ya Kidini yaliyorithiwa na kuzoeleka, ni yale ya kutetea haki za Mwenyezi Mungu zilizoko kwa waja Wake, katika nyanja ya Kiitikadi na Kiibada. Basi wanachuoni wamejishughulisha sana katika kubainisha itikadi za Kidini na nguzo za ibada, ambapo mambo haya huleta mafungamano kati ya Mwenyezi Mungu na mja Wake, na ni katika mambo yanayomuokoa na kumfaa mja Siku ya Kiyama. Ama kuhusiana na haki za watu kati yao, na ambayo ni sababu ya kupangika maisha yao ya kidunia, kwa kweli jambo hili halijapewa kipaumbele.

Na kwa upande mwingine ni kwamba baadhi ya mafunzo ya Kidini, hayakufahamika vyema na kuhusishwa utekelezwaji wake katika mambo maalumu. Jambo hili limetengeneza aina fulani ya usahaulifu katika masikio ya wafuasi wa Dini juu ya utetezi wa haki za binadamu. Miongoni mwa mafunzo hayo ni suala la subira, ambapo maana yake halisi, ni kutokutetereka na kuwa na msimamo madhubuti mbele ya changamoto mbalimbali, lakini neno hili (subira) limepewa maana ya kusalimu amri na kujidhalilisha. Mafunzo mengine ni neno 'Zuhdi' ambalo maana yake halisi, ni kujiepusha



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 59 1/7/2015 11:52:47 AM

na matamanio ya dunia na kujikita katika kutekeleza mafunzo ya Kiislamu, lakini limepotoshwa maana yake na kuwa na maana ya kutokujali mambo yanayohusiana na maisha.

Pia katika jambo hili, ni ufahamu wa baadhi ya Hadithi ambazo zinaelezea namna ya kuamiliana na watawala, ambazo zinamaanisha kuwa na tahadhari pasitokee fitina, kwa hivyo raia wakubali matendo yote yanayofanywa na kiongozi wao, hata kama mtawala huyo ni dhalimu na mwenye kwenda kinyume na sheria.

Kwa kweli watu wameghafilika na maandiko na mafunzo ya Kidini ambayo yanamlea binadamu Mwislamu katika kushikamana na uhuru wake, heshima yake na haki zake, na kumhimiza kuyapigania mambo haya, na kutokukubali kudhulumiwa na kuvunjiwa haki zake za kimada na kiroho, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَمَنِ اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ

**"Anayekushambulieni, basi nanyi mshambulieni kwa kadiri alivyokushambulieni." (Qur'ani 2:194).**

Na pia Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu Waumini wanaopigana kwa ajili ya kuzirejesha haki zao kwa kusema:

وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ

**"Na ambao wanapofanyiwa jeuri hujitetea." (Qur'ani 42:39).**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 60 1/7/2015 11:52:47 AM

Na imepokewa kutoka kwa Ali (a.s.) akisema: "Haikupotea haki, iliyofuatiliwa na kutafutwa." Na katika dua ya tabia njema iliyopokewa kutoka kwa Imamu Ali ibn Husein Zaynul Abidiin (a.s.), kama ilivyokuja katika ibara ifuatayo: "Na unijaalie nguvu kwa yule aliyenidhulumu, na kauli kwa aliyenifanyia uhasama, na ushindi kwa aliyenifanyia uadui, na unipe nguvu kwa aliyenifanyia vitimbi na uwezo kwa aliyenitimua." Na An-Nawawiy amenakili maneno kutoka kwa Abi Ali Daqqaq katika kitabu chake alichosherehesha Sahihi Muslim, akisema: "Mwenye kuinyamazia haki, huyo ni shetani bubu."

Basi hakuna budi kuelezwa mafunzo haya kwa uwiano, ili kusiwe na mchanganyiko na kasoro katika mafunzo na mwenendo. Na pia katika historia ya Kiislamu kumekuwa na sababu ya kisiasa ambayo imewafanya wanachuoni na wanafikra wasiingie kwenye mikwaruzano na watawala, kama ilivyokuwa katika utawala wa Kiabbasi na wa Kiumayya, na mfano wao ambao walifuata siasa ya ukandamizaji na kuvunja haki nyingi za binadamu, kwani ilikuwa kuzungumzia haki hizo ni sawa na kupinga tawala hizo au kuwaamsha watu juu ya matendo yao.

Mmoja wa watafiti wa zama hizi, alifanya utafiti juu ya yale yaliyojazwa katika vitabu vya historia vya Kiislamu kuhusiana na uvunjwaji wa haki za binadamu. Basi palitengenezwa kitabu kikubwa kilichokuwa kikiitwa '*Mausuatul Adhabi* (Kitabu cha Mateso)', kurasa zake zinafika 3000, ndani yake kuna aina tofauti za uvunjaji wa haki na uporaji, mambo ambayo yanafedhehesha uso na kusababisha mshangao na mshituko.[32]

Hata baada ya kuondoka tawala hizo, ni kwamba bado umma ulitahiniwa na ugonjwa wa kuitukuza historia na kuwatukuza watu wa zama hizo, mpaka ikawa kuwakosoa watawala hao pamoja na

[32] Shalijiy: Ubudi, *Mausuatul Adhabi*.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 61 1/7/2015 11:52:47 AM

siasa zao ni jambo lisilokubaliwa na wengine, kwa hoja kwamba Mwenyezi Mungu amesema:

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**"Hao ni watu waliokwishapita. Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakayoyachuma, wala nyinyi hamtaulizwa yale waliyokuwa wakiyafanya." (Qur'ani 2:134)**

Ni kweli, kujiingiza kwenye mizozo ya kihistoria ni jambo lenye madhara ikiwa mtu atajihusisha katika mizozo na migawanyiko katika umma, lakini pia kukithirisha kuwatukuza watu wa kale, kunawanyima watu kupata mafunzo na mazingatio kwa yale yaliyopita, na huenda makosa yao yakawa ni yenye kufuatwa kisheria. Na pia kuna sababu za kimila na kidesturi ambazo zimekuwa na nguvu sana katika jamii ambazo zinavunja haki za binadamu, ambapo wanaharakati wa Kiislamu wameshindwa kuzikabili, kama ilivyo kuhusiana na kuamilia kubaya na mke na mwanamke kwa ujumla, na pia ugumu katika kuamiliana na watoto, wanafunzi na wafanyakazi. Na sababu nyingine inayowafanya wanaharakati wa Kiislamu kuacha kujishughulisha na haki za binadamu, ni kutokuwepo na ukweli wa tangazo la haki za binadamu unaofanywa na nchi za Magharibi, kwa vile katika baadhi ya vipengele vyake vinakwenda kinyume na sheria za Kiislamu, kama vile uhuru wa kuritadi (kutoka katika Uislamu), usawa kati ya mwanamme na mwanamke katika mirathi na talaka.

Ni jambo la wazi kwamba, baadhi ya nchi za Magharibi pamoja na Marekani, ni mfano wa wazi katika hili, na zina undumilakuwili

katika kaulimbiu yao ya haki za binadamu. Wanaitumia kaulimbiu hii kwa ajili ya maslahi yao na malengo yao, kwani hufumbia jicho upande mmoja unaovunja haki za binadamu kwa vile ni marafiki zao, katika wakati ambao ulimwengu hujaa kauli dhidi ya waasi wanaotaka kuzitawala nchi hizo, na dalili ya wazi ni kule kunyamaza kwao kimya, bali kuchangia unyama na uvunjwaji wa haki za binadamu wanofanyiwa Wapalestina, wanaodhulumiwa haki zao na wazayuni, ukatili ambao unaendelea siku hadi siku, kwa hili linawafanya wasionekane wakweli katika kadhia ya haki za binadamu.

Na kama hali ya kuwarudi katika siasa zao hizi chafu, baadhi ya wanaharakati wa Kiislamu wanaziangalia nchi za Ulaya kwa wasiwasi pindi wanapoelezea haki za binadamu, kama kwamba ni azimio lililochakachuliwa au kama kwamba ni neno la haki, lenye malengo yasio sahihi.

# MTAZAMO WA KUJISHUGHULISHA ZAIDI NA HAKI ZA BINADAMU:

Licha ya kuwepo baadhi ya visingizio hivi na ukubwa wa baadhi ya sababu hizo, lakini haifai kujizuia na hakika mbili zilizo tukufu:

**Ya kwanza:** Nafasi ya haki za binadamu katika sheria ya Kiislamu, na msisitizo mkubwa juu ya kuzichunga na kuzilinda. Maandiko matakatifu ya Kidini hayakutoa onyo kali kama yalivyotoa dhidi ya kuwafanyia makosa na dhulma na kutochunga haki za watu wengine, kama ambavyo, kusimamisha uadilifu kati ya watu, ndio lengo la msingi la sheria za Mwenyezi Mungu na sababu ya kuletwa Mitume, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyosema:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu…" (Qur'ani 57:25).**

Hii inamaanisha kwamba, kuidharau kadhia hii, maana yake ni kupotea lengo la msingi la Dini na kupinga moja kati ya sheria zake muhimu na malengo yake.

**Ya pili:** Mafungamano ya hali ya juu kati ya uchungaji wa haki za binadamu na kiwango cha maendeleo ya kistaarabu ya watu, kwani haiwezekani watu wakaendelea na kuwepo utulivu thabiti na hasa



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 64 1/7/2015 11:52:47 AM

katika zama hizi, ikiwa hakutapatikana heshima ya kuwaheshimu watu wake, kwani mtu mwenye kukandamizwa na kudhulumiwa, katu hawezi kuleta maendeleo ya kweli, na wala hawezi kuzalisha, ambavyo leo ulimwengu hauwaheshimu watu wasiojali haki za binadamu. Basi ni juu yetu kutambua kiwango cha ujinga wa kutochunga haki za binadamu, ambacho jamii zetu nyingi za Kiislamu zinaishi nacho. Kwani kiwango cha ripoti kinachotolewa kutoka katika mashirika yanayojishughulisha na kadhia hii, juu ya hali mbaya ya haki za binadamu katika nchi za Kiislamu, sio zote zina malengo mabaya, licha ya kwamba baadhi ya mashirika hayo yana malengo mengine, lakini ukandamizaji wa haki za binadamu unaotokea, huenda ukawa mkubwa zaidi kuliko huo unaotajwa katika ripoti.

Mambo haya mawili yanawalazimisha wanaharakati wa Kiislamu, kuanza kujishughulisha na kadhia ya haki za binadamu na kujitolea kuzitetea, kwa kusambaza mtazamo wa Kiislamu na mafunzo yake yanayoelezea haki za wengine kwa kupitia mitaala ya masomo, vyombo vya habari, wanapowahutubia watu, kuunda taasisi zinazojishughulisha na haki za binadamu, na kutumia njia mbalimbali zinazonasibiana na sheria.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 65 1/7/2015 11:52:47 AM

# JUMUIYA YA KITAIFA YA HAKI ZA BINADAMU:

Kuanzishwa jumuiya ya kitaifa inayojishughulisha na haki za binadamu katika nchi ya Saudi Arabia, ni hatua kubwa ya kukabiliana na changamoto hii, kwani kikundi cha watu werevu miongoni mwa wananchi wa nchi hii tukufu wameweza kuunda jumuiya hii kwa ajili ya kutetea haki za binadamu na kusimama dhidi ya dhulma, ukandamizaji, utesaji na kutokusamehe, na kwa kushirikiana na mashirika mengine ya kimatifa yenye kujishughulisha na kadhia hii, kama ilivyo katika katiba ya jumuiya hii.

Kwa kuchelewa kuundwa kwa jumuiya hii, au kuwepo baadhi ya maoni kutoka kwa baadhi ya watu kuhusiana na njia ilizozipita ili kuasisiwa kwake, haifai kujizuia kuipongeza na kuihamasisha na kuisaidia ili ifikie malengo yake mazuri iliyojiwekea. Kwa hakika ni tajriba nzuri, ambayo itatuongoza kwenye maendeleo, na kutusaidia kuachana na uvivu na kuvivishwa, mambo ambayo yanaisibu jamii ya Kiislamu katika kadhia ya kujishughulisha na haki za binadamu.

Kwa kufaulu mradi huu, kutaleta kheri nyingi kwa nchi na wananchi na kwa serikali, kwani nchi inayoheshimu haki za binadamu, huingia ndani ya nafsi za wananchi wake, na hufaidika kutokana na utoaji wa nguvu zao na uwezo wao katika maendeleo na kuijenga kwa uwezo wao wote. Na mtu ambaye anapata haki zake za kibinadamu anakuwa na raha nyingi, na kujitolea kwa nia safi kwa ajili ya nchi yake na watu wake. Na serikali ambayo inalinda na kuhami haki za raia wake, inastahiki uungwaji mkono na wananchi wake wa ndani, na kuheshimiwa katika ulimwengu. Na mafanikio haya haya-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 66 1/7/2015 11:52:47 AM

patikani isipokuwa wanachama wa jumuiya hii watakapotoa juhudi zao tukufu, na kusaidiwa na taasisi za kimataifa, na kupata uungwaji mkono wa wananchi kwa kuwasaidia.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 67 1/7/2015 11:52:47 AM

# WAJIBU WA KUTETEA HAKI ZA BINADAMU

Umeelezwa kwamba katika zama za utawala wa al-Muutadhid al-Abbasiy, ambaye alitawala kuanzia mwaka 279 mpaka 289 A.H., kwamba mmoja kati ya makamanda wakubwa alimkopa pesa mtu mmoja aliyekuwa mzee katika mji wa Baghdadi, na baadaye alikataa kumrudishia pesa zake, na kila alipojaribu kupata pesa zake hakufanikiwa, mpaka mtu mmoja akamtaka aende kwa mshona mabusati. Mtu huyo alimwambia yule mzee: "Hakika yeye ndiye mtu peke yake ambaye atakuwezesha kupata pesa zako." Yule mzee alimwendea, na kwa kweli alikuwa anashona mabusati, na alishangazwa naye pale alipomwambia: "Kaa hapa, na kwa haraka nitakupatia haki yako…" Yule mshona mabusati alimtuma mmoja wa wafanyakazi wake aende nyumbani kwa yule kamanda na amwambie amuendee huku akiwa na pesa za mzee. Baada ya muda mfupi yule kamanda akamlipa mzee pesa zake na akamuomba msamaha kama mtoto anavyoomba msamaha kwa baba yake. Na baada ya yule kamanda kuondoka, yule mzee alimuuliza mshona mabusati: "Ni vipi umekuwa na nguvu juu ya watu hawa?"

Mshona mabusati alimjibu: "Mimi nina kisa fulani, kama unavyoniona ni mshonaji mabusati wa kawaida, na wala mimi sina cheo rasmi, lakini nimepata hadhi hii ambayo umeshuhudia matokeo yake, kutokana na kadhia iliyotokea hapa… Usiku mmoja nilikuwa nimekaa kwenye varanda ya nyumba yangu, mara nikamuona kamanda anapita mbele ya nyumba yangu akiwa amepanda farasi, na kwa upande mwingine kulikuwa na mwanamke mzuri akiwa anatembea kwa heshima na upole. Yule kamanda alimpandisha mwanamke juu ya farasi wake kwa nguvu, na akaelekea naye nyumbani kwake, na



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 68 1/7/2015 11:52:47 AM

huku mwanamke akipiga kelele za kutaka usaidizi kwa kusema: Mimi si mzinifu, mimi nimeolewa, na mume wangu amekula kiapo kwamba atanitaliki ikiwa usiku mmoja nitalala nje ya nyumba yake.

Lakini yule kamanda hakushughulika na maneno yake, bali mimi nikateremka kutoka kwenye varanda na nikawakusanya baadhi ya watu, na tukaenda ili kuingilia kadhia hiyo, lakini aliwaamrisha askari watupige. Basi walitupiga na kututawanya… Basi nikarudi nyumbani, lakini sikuonja usingizi hata kitambo kidogo, nikawa nafikiri juu ya yule mwanamke, na namna mume wake atakavyomtaliki iwapo atalala katika nyumba ya kamanda katika usiku huu…

Wakati niko katika kufikiri, mara ikanijia fikra ya kwenda msikitini, ili niadhini kwa ajili ya Swala ya Asubuhi, na kwa hakika yule kamanda atafahamu kwamba asubuhi imeshaingia, hapo atamuacha yule mwanamke aendelee na shughuli zake, na kurudi nyumbani kabla ya kumalizika usiku, kwa hivyo hatotalikiwa. Basi nilikwenda msikitini na nikapanda mnara wa kuadhinia, na nikaanza kuadhini kwa sauti ya juu…, nilipomaliza adhana niliwaona askari wakiwa wamezunguka msikiti, na kunitaka niende nao katika kasri la Khalifa (al-Muutadhid). Alikuwa ananisubiri, kama walivyoniambia..

Nilikwenda kwake. Alikuwa amejawa na hasira, ghafla akanitangulizia suala kwa kusema: Je, huu ndio muda wa adhana? Je, nchi haina sheria? Nilisema: Mwenyezi Mungu aitulize akili ya Amiri, hakika sheria za nchi zimekanyagwa kwa miguu siku ambayo mkubwa ameachwa aharibu utu wa wanawake, na kukawa hakuna wa kumzuia. Kisha nikamueleza Khalifa yale yaliyofanyika. Basi aliamrisha aletwe yule kamanda pamoja na mwanamke, na baada ya kupatikana uthibitisho wa jambo lao, Khalifa aliamrisha auliwe yule kamanda, na akamuacha huru mwanamke na kumpa heshima yake, na akanitaka mimi niadhini kila ninapoona tukio la aina kama hilo…, na kwa vile jambo lilienea kati ya makamanda na viongozi,



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 69 1/7/2015 11:52:47 AM

basi wao wananiogopa, na hivi ndivyo ambavyo mimi nina nguvu juu yao…"

Tumetaja kisa hiki cha kihistoria ili kiwe ni kama utangulizi wa mazungumzo yanayohusiana na majukumu ya kila mtu katika kulinda haki za binadamu. Sisi katika kisa hiki cha kweli, kuhusiana na kitendo kilichofanywa na raia wa kawaida, aliyeona uvunjwaji wa haki za binadamu mbele yake, uliofanywa na mfanyakazi aliyekuwa na cheo kikubwa katika serikali, aliyetumia nafasi yake kuwafanyia uadui watu wengine, raia huyu wa kawaida hakuiruhusu akili yake inyamaze juu ya dhulma ile, na wala hakuipa visingizio nafsi yake ya kwamba ina mipaka maalumu mbele ya kamanda mwenye nguvu na cheo. Bali aliikamua akili yake kwa kufikiria njia inayowezekana kuipigania haki ya mwanamke yule dhaifu na kumtetea. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweza kumuongoza namna ya kuvumbua mbinu kwa sababu ya nia yake safi na ikhlasi yake, mbinu ambayo ilimfungulia njia ya kumkomboa kila mwenye kudhulumiwa na kuitetea haki ya yeyote. Kama ambavyo Muutadhid Abbasiy hakuwa mtawala mwadilifu aliyechaguliwa na watu, lakini hilo halimaanishi kutowezekana kutatua baadhi ya matatizo na kutengeneza baadhi ya yale yaliyoharibika.

Hili ndilo somo muhimu ambalo tunalipata kupitia kisa hiki. Basi ni wajibu kwa kila raia kubeba majukumu yake kuhusiana na haki za binadamu, kwa sababu ni kadhia muhimu mno na tukufu sana, ambayo inastahiki kujishughulisha nayo na kuipigania. Kwani haki za binadamu ndio kitu kinachosimamisha utu. Na kuzivunja inamaanisha kuvunja utu wa mtu na kupora utukufu wake aliopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

# KUTETEA HAKI:

Hali ya maumbile ya mtu kujipenda mwenyewe, ambayo yamewekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya nafsi ya kila mtu, yanamsukuma katika kulinda na kutetea maslahi. Ni jambo ambalo halihitaji mahimizo ya kisheria kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika utekelezaji wa jambo hili, kwa sababu hali ya kimaumbile ya binadamu, inamsukumu kwenye kupigania haki zake. Na amri za Kisunna zilizokuja kuhusiana na jambo hili ni aina ya amri za muongozo tu. Hii ni kwa mujibu wa istilahi za wanachuoni wa elimu ya Usulul Fiqhi, kama ambavyo humsaidia binadamu kujiepusha na masaibu, na kuvumilia matatizo yanayomkabili wakati wa kupigania haki.

Hakika Qur'ani Tukufu, inamhimiza yule mwenye kudhulumiwa haki zake, kupinga na kutangaza waziwazi namna alivyodhulumiwa, ili iwe ni sababu ya kuufedhehesha upande uliomfanyia dhulma na maovu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

لَا يُحِبُّ اللَّهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَنْ ظُلِمَ

**"Mwenyezi Mungu hapendi uovu uenezwe kwa maneno ila kwa mwenye kudhulumiwa." (Qur'ani 4:148).**

Na yule ambaye atajishughulisha katika kupigania haki yake, na kutetea maslahi yake kwa mujibu wa sheria, mtu huyo atakuwa ametekeleza haki yake ya kimaumbile, na wala hakuna lawama yoyote, Mwenyezi Mungu anasema:



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 71 1/7/2015 11:52:47 AM

وَلَمَنِ انْتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَٰئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِنْ سَبِيلٍ

**"Na wanao jitetea baada ya kudhulumiwa, hao hapana njia ya kuwalaumu." (Qur'ani 42:41)**

Na katika *Sahihul Bukhariy*: "Mtu mmoja alikuwa anamdai Mtume (s.a.w.w.), alimuendea kumdai, katika kudai alitumia lugha kali na nzito wakati wa kuzungumza na Mtume (s.a.w.w.). Maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.) wakataka kumuadabisha kutokana na utovu wake wa adabu, Mtume (s.a.w.w.) alisema: 'Mwacheni, kwani mwenye haki anakuwa na lugha yake maalumu.'"[33] Na wala haifai kwa mtu kupitiliza mipaka katika kudai haki yake, kiasi cha kuwadhulumu watu wengine. Kwa kufanya hivyo hapati heshima yoyote kwa watu na wala hatopata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani imepokewa kutoka kwa Imamu Husein ibn Ali (a.s.) kutoka kwa Babu yake (s.a.w.w.) akisema: "Mwenye kushutumu hasifiwi wala halipwi mema."[34] Na kuna riwaya iliyopokewa kutoka kwa Imamu Ja'far (a.s.), akisema: "Hakika Mwenyezi Mungu amemuachia Muumini mambo yake yote, na wala hakumuachia ruhusa ya kuwa dhalili."[35]

Na wajibu wa kupigania haki za binadamu hauishii katika mipaka ya maslahi yanayofungamana na mtu mwenyewe tu, bali maana yake ni kubeba majukumu ya kutetea haki yoyote ya binadamu yeyote yenye kukandamizwa, kiasi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu, anawahimiza Waumini kupigana kwa ajili ya kuwaokoa wanyonge kutokana na ukandamizaji wanaofanyiwa, anasema:

---

33 Al-Bukhariy: Muhammad ibn Ismail, *Sahihul Bukhariy*, Hadithi Na. 2401.

34 Al-Muttaqiy al-Hindiy: Ali, *Kanzul ummal*, Hadithi Na. 9287.

35 At-Tusiy: Muhammad ibn Hasan, *Tahdhibul Ahkam*, Jz. 6, Uk. 179.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 72 1/7/2015 11:52:47 AM

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ

**"Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa, wanaume na wanawake na watoto…" (Qur'ani 4:75).**

Qurtubiy amesema kuhusiana na Aya hii: "Mwenyezi Mungu amewajibisha Jihadi kwa ajili ya kulinyanyua neno Lake na kuidhihirisha Dini Yake na kuwaokoa Waumini wanyonge miongoni mwa waja Wake, na hata kama jambo hilo litapoteza roho. Na pia kuwakomboa mateka ni wajibu kwa Waislamu, ama kwa kupigana au kwa kutumia mali. Amewajibisha hayo kwa vile kufanya hivyo ni jambo hafifu zaidi kuliko hao mateka. Malik amesema: Ni wajibu kwa watu kutoa fidia ya kuwakomboa mateka kwa mali zao zote, na hili halina khitilafu yoyote, katika kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo: **"Na ya wale wanaoonewa…"** amewaunganisha katika Jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa maana: **"Na katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa…"** kwani kwa hakika kuwakomboa wanaoonewa ni miongoni mwa njia za Mwenyezi Mungu."[36]

Mtu kunyamazia uvunjwaji wa haki za wengine na huku akiwa na uwezo wa kuzitetea, hiyo inazingatiwa sawa na kushiriki katika dhulma na kuunga mkono hali ya ufisadi na madhara yake kwa ujumla. Kutokana na hali hii, Ibn Abbas amepokea kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Naapa kwa Nguvu Zangu na Utukufu Wangu, nitamlipizia kisasi dhalimu kwa haraka na kwa kumsubiria, na nitamlipizia kisasi mwenye kumuona mdhulumiwa akidhulumiwa na huku akiwa na uwezo wa kumtetea."[37]

---

36 Qurtubiy: Muhammad ibn Ahmad, *Tafsir Qurtubiy*: Jz.5, Uk. 180.

37 Al-Muttaqiy al-Hindiy: Ali, Kanzul ummal, Hadithi Nal 7641.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 73 1/7/2015 11:52:47 AM

Na pia imepokewa kutoka kwake Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume Wake, Daud (a.s.): Hakuna mja atakayemsaidia mdhulumiwa, au atakayetembea pamoja naye katika kutafuta haki yake, isipokuwa Mwenyezi Mungu ataidhibiti miguu yake katika siku ambayo miguu itateleza."[38] Na Imamu Ali (a.s.) aliwausia watoto wake, Hasan na Husein (a.s.) kwa kusema: "Na kuweni mahasimu kwa madhalimu na wasaidizi kwa mwenye kudhulumiwa."[39] Na kutoka kwa Sahli ibn Huneyfi, kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.), amesema: "Ambaye atamuona Muumini akidhalilishwa mbele yake na huku akiwa na uwezo wa kumnusuru, lakini asimnusuru, basi Mwenyezi Mungu atamdhalilisha mtu huyo mbele za watu Siku ya Kiyama."[40]

Basi uvunjaji wa haki ya mtu yeyote katika jamii, ni kuiweka jamii yote katika maangamizi, na kunyamaza kwao juu ya uvunjwaji huo na kutokuwajibika kwa hilo, ni mambo yanayovunja mustakabali wenye heshima kwa jamii yote. Haya ndiyo aliyoeleza Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema: "Hakika watu wanapomuona dhalimu, na wasimshike mkono wake (wasimzuie), basi Mwenyezi Mungu hukaribia kuwajumuisha katika adhabu kutoka Kwake."[41] Na katika Hadithi nyingine ya Mtume (s.a.w.w.) anasema: "Ni vipi Mwenyezi Mungu atautukuza umma ambao hautetei haki ya mtu wao dhaifu kutoka kwa mtu wao aliye na nguvu."[42]

Haki za binadamu zimethibiti kwa binadamu, kwa sababu ya ubinadamu wake, bila ya kuangalia sifa nyingine ya pili, kama vile jinsia, kabila, dini au nasaba. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa heshima kwa wanadamu wote kwa ujumla, bila ya kuhusish-

---

38 Kitabu kilichotangulia, Hadithi Na. 43467.
39 Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*: Barua Na. 47.
40 Ibn Hanbal: Ahmad, *Musnad Imami Ahmad ibn Hanbal*, Haditni Na. 12081.
41 Al-Muttaqiy al-Hindiy: Ali, *Kanzul ummal*, Hadithi Na. 5543.
42 Kitabu kilichotangulia, Hadithi Na. 5547.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 74 1/7/2015 11:52:47 AM

wa, amesema: **"Kwa hakika tumemtukuza binadamu."** (Qur'ani 17:70). Na pia amesema: **"Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa."** (Qur'ani 95:4). Na Aya mbalimbali za Qur'ani zinasisitiza ya [43] kwamba lengo la sheria za Mwenyezi Mungu ni kusimamisha uadilifu kati ya watu na kutetea haki zao, bila ya kuangalia kikundi maalumu miongoni mwa watu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ
وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu." (Qur'ani 57:25).** Na pia anasema: **"Na semeni na watu kwa uzuri." (Qur'ani 2:83).**

Na msisitizo wa kuheshimu haki za kila binadamu, umekuja katika maandiko ya Kidini, ambayo yanaonya juu ya kuvunja haki za watu wenye kukhalifu Dini (wasio Waislamu), na wale waliokuwa wakiishi katika himaya ya dola ya Kiislamu, kama ilivyopokewa katika *Sunan Abi Daudi* kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema:

"Tambueni kwamba, mwenye kumdhulumu asiye Mwislamu ambaye anaishi katika dola ya Kiislamu kwa mkataba maalumu, au akampunguzia haki zake au akamkalifisha zaidi ya uwezo wake au akachukua kitu kutoka kwake bila ya ridhaa ya nafsi yake, basi mimi nitakuwa hasimu wake Siku ya Kiyama."

43 Sajistaniy: Abu Daudi Sulayman ibn Ash-athi, Sunanu Abi Daud, Hadithi Na.3052.

# ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU NA HATUA ZA UTEKELEZAJI

Hatua ya kwanza katika kuhakikisha kunapatikana haki za binadamu na kutetewa, ni kizitambua haki hizo na kueneza elimu yake. Hii ni kwa sababu watu wengi katika jamii zetu hawatambui haki zao na zile zilizo wajibu kuwafanyia wengine, basi hawatafuti kile kilicho chao na wala hawatekelezi kile wanachowajibika kuwafanyia wengine, sababu yake ni ujinga na kukosa maarifa.

Kwa hakika maarifa ya kutambua haki sio sehemu ya mipangilio ya maisha yetu na mafunzo yetu katika nyanja tofauti, kwani tunaendesha maisha yetu ya kijamii na kisiasa kwa kubahatisha na kwa kufuata hali ya maisha ilivyo, bila ya kuzingatia kwamba hali hii itapelekea uvunjaji wa haki za binadamu na kutokuheshimu utukufu wake! Hakuna mtaala wa kimasomo katika taasisi za kielimu ambao utamwezesha mwanafunzi kujua haki zake! Na huenda mfanyakazi asitambue haki zinazohusiana na kazi yake.

Na katika mfumo wa kindoa, wanandoa wanakutana bila ya kutambua mfumo wa haki za mafungamano ya kindoa. Na kwa upande wa kisiasa, watu hawajui haki zao kama wananchi, na katika kuamiliana na taasisi yoyote ile miongoni mwa taasisi za serikali, hawazipitii kanuni zinazohusiana na taasisi kadhaa. Bila ya shaka, kuna taratibu na kanuni zanazohusiana na kila taasisi, bila ya kuangalia ukamili au upungufu wa kanuni hizo, lakini tatizo kwenye jamii zetu lipo kwenye ukosefu wa ratiba ya kueleweshwa mambo yanayohusina na haki.

Ama katika nchi zilizoendelea, kueleweshwa na kuelimishwa haki ni sehemu ya ratiba za elimu, na katika ratiba za vyombo vya



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 76 1/7/2015 11:52:48 AM

habari, na katika kuanzisha familia, na katika mafungamano ya ajira, na katika aina yoyote ya muamala kati ya pande mbili. Kwa mfano katika nchi hizo zilizoendelea, askari wa barabarani anapokukuta na kosa la barabarani, hukuambia jambo ambalo utachagua kufanya kwa mujibu wa kanuni ili uamiliane nalo. Na wakati unaposimamishwa kwa ajili ya kuhojiwa, hukutajia haki zako, na ni haki yako kutaka jambo fulani na kukataa jambo fulani. Na mfanyakazi hajiungi na taasisi kwa ajili ya kufanya kazi, ila baada ya kusoma taratibu na kanuni za makubaliano, kisha husaini baada ya kukubaliana na vipengele vilivyomo, na hivi ndivyo ilivyo katika nyanja mbalimbali.

Kwa hakika tuna haja kufanya juhudi kubwa ya kueneza elimu juu ya haki katika jamii zetu, kwa kusomesha mikataba ya haki za binadamu, na kuzipitia taratibu na kanuni za nchi, na kujua mipaka na kanuni za mafungamano yetu ya kijamii. Na katika mafunzo yetu ya Kiislamu, kuna mahimizo makubwa juu ya haki za binadamu na taratibu za mafungamano ya kijamii. Hakika katika milango ya Kifiqhi ya Kiislamu kuna utajiri wa misingi madhubuti ya haki za kila upande miongoni mwa watu. Kuna haki kati ya mtawala na raia wake, kati ya mkuu wa familia na wanafamilia wake na kati ya makundi ya kijamii wao kwa wao. Lakini maarifa haya ya Kiislamu ya haki, yanahitaji kuagaliwa upya, na kuelezwa kwa njia nzuri, ili yaendane na lugha ya kisasa na maendeleo ya maarifa ya binadamu katika kadhia hii.

Na mara nyingi katika kuelezwa haki katika hotuba zetu za Kidini zinalenga upande mmoja, kiasi cha kusisitiza haki upande mmoja na kujisahaulisha upande mwingine, jambo ambalo linapalilia mfumo wa ukandamizaji, chini ya hatari ya khofu inayotokana na ugaidi. Kwa mfano, inasisitizwa sana juu ya haki za mwalimu bila ya kubainishwa haki za mwanafunzi, na msisitizo juu ya haki za



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 77 1/7/2015 11:52:48 AM

wazazi wawili, na huku kughafilika juu ya haki za mtoto, na kuzikuza haki za mume na kuzipuuzia haki za mke, na kusisitiza juu ya haki za mtawala na kuacha haki za raia. Huu ni mfumo usio sawa, ni mfumo ambao husaidia kuwepo haki za binadamu, bali unahimiza kuzivunja. Katika hali ambayo tunamkuta Imamu Ali (a.s.) wakati alipokuwa Khalifa, mara nyingi hotuba zake na barua zake alizokuwa akiwaandikia magavana katika majimbo, zikizungumzia haki zenye kulingana kati ya mtawala na raia.

Imekuja mwanzoni mwa hotuba yake maneno yafuatayo: "Enyi watu! Kwa hakika mimi nina haki juu yenu na nyinyi mna haki juu yangu. Haki yenu juu yangu ni kuwapeni nasaha, na kuwarahisishia ruzuku zenu, na kuwaelimisheni ili msiwe wajinga, na kuwaadabisheni ili mjue. Ama haki yangu juu yenu ni kuitekeleza bai'a (kiapo cha utiifu), na nasaha mbele ya macho yangu na mbali nayo, na kuniitika niwaitapo, na kutii ninapowaamrisha."[44]

Na wakati Makhawariji walipotangaza upinzani wao kwake, alikimbilia kutaja haki za upinzani, na akazungumza mbele ya watu. Imekuja katika kitabu cha historia cha Tabariy, akisema: "Siku moja Ali alisimama mbele ya watu na kuwahutubia, mtu mmoja aliyekuwa upande wa msikiti alisema: Hakuna serikali, isipokuwa ya Mwenyezi Mungu. Na mwingine naye akasimama na kusema maneno kama hayo, kisha wakafuatiliwa na watu wengi wakiwa wanasema maneno kama hayo. Ali alisema: Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, ni neno la haki lililokusudiwa batili! Ama nyinyi mna mambo matatu kwetu ikiwa mtasuhubiana nasi: Hatutowazuilia misikiti ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutaja Jina Lake humo, na hatutokunyimeni mali iwapo mikono yenu itakuwa pamoja na mikono yetu (hamtotufanyia uadui), na wala hatutowapiga vita mpaka pale mtakapotuanza kutupiga."[45]

---

44 Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*; Khutba: Barua Na. 3 4.
45 Tabariy: Muhammad ibn Jarir, *Tarikhu Tabariy*, Jz. 4, Uk. 53.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 78 1/7/2015 11:52:48 AM

Hivi ndivyo ambavyo Imamu Ali (a.s.) anavyotangaza haki zao na kuwahakikishia kuzitekeleza. Kwa upande wa usalama, hatowafanyia uadui iwapo hawatafanya uasi, na kwa upande wa kiuchumi, hatowanyima haki yao kutoka katika Benki Kuu, na kuhusiana na mambo ya kijamii, hatowazuilia kuhudhuria Swala za jamaa pamoja na Waislamu wengine.

Na kuhusiana na kadhia hii, Imamu Ali ibn Husein (a.s.) ameandika waraka wa haki ambao unazungumzia juu ya haki hamsini, ambazo ni haki zinazozungumzia pande mbilimbili, kwani amezungumzia haki za mtawala na raia, haki za wazazi na mtoto, haki za mshitaki na mshitakiwa, haki za mwalimu na wanafunzi, haki za Waislamu na wasiokuwa waislamu…, kwa hakika waraka huo ni miongoni mwa mirathi yetu ya Kiislamu iliyo bora mno.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 79 1/7/2015 11:52:48 AM

# KUTENDA KWA AJILI YA HAKI ZA BINADAMU:

Mafanikio ambayo wameyapata jamii nyingine katika nyanja ya haki za binadamu, si jambo lililotokea kati ya asubuhi na jioni, na wala haikutokea mara moja, na wala haikuwa kwa urahisi na wepesi. Kwa kweli mataifa hayo yaliishi katika dhulma kubwa ya ukandamizaji wa kanisa na dhulma ya kisiasa. Basi kukajitokeza fikra za kuwa huru na kuboresha maisha, fikra ambazo zilizaliwa kutoka katika tumbo la ukandamizaji wa hali ya juu, na zilichukua muda mrefu na juhudi za hali ya juu na kujitoa muhanga, lakini baadaye zilizaa matunda ya kupatikana mikataba ya haki za binadamu, na kuleta mafanikio yake katika nchi hizo.

Na wakati nchi zetu zinapotaka kuwafikia hao waliotangulia, basi hazina budi kutoa juhudi nyingi sana na kazi yenye kuendelea, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunapatikana neema hiyo. Na katika mafunzo yetu ya Kiislamu kuna hazina kubwa ya elimu na mafunzo ambayo yanaweza kutuwezesha kuanza harakati kwa nguvu, na katika hali ambayo tunafaidika na uzoefu wa mataifa mengine, na kujua kasoro ambazo tunapaswa kuziepuka. Kwa hakika sisi tunahitaji kufanya kazi ya kutetea haki za binadamu katika nyanja tatu:

**Kwanza: Kanuni na Sheria:**

Katika nyanja ya kanuni na sheria: Sheria za mifumo ya kisiasa inayotegemewa iwe inawafikiana na mikataba ya Kiislamu na ya kimataifa juu ya haki za binadamu, na iangaliwe na kufutiliwa mbali mifumo inayogandamiza haki yoyote, au kusababisha uvunjaji wake. Hii ndio kazi kubwa ya baraza la kutunga sheria, kama vile baraza

la mashauriano na kikao cha bunge, ambayo yanapaswa yaamiliane na haki za binadamu kama haki ya msingi na lango la mwanzo, na baadaye sheria zote na kanuni ziwe chini ya kivuli chake.

Na wanafikra pamoja na walinganiaji wa maendeleo katika umma wana wajibu wa kulipatia kipaumbele suala la haki za binadamu kuliko kitu kingine chochote. Na mashirika ya kutetea haki za binadamu ni juu yao kujishughulisha na ufuatiliaji wa sheria na siasa zinazofuatwa na namna ya kuafikiana kwake na haki za binadamu, badala ya kujishughulisha zaidi katika mambo madogo madogo, ambayo ni miongoni mwa mipango ya kanuni za kisiasa.

**Pili: Utekelezaji wa Serikali:**

Ni juu ya Serikali na wafanyakazi wake kutekeleza haki za binadamu, kwani kiwango kikubwa cha uvunjwaji wa haki za binadamu hufanywa na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Serikali. Huwa hawachungi utukufu wa ajira, na hutumia vibaya nafasi zao na vyeo walivyonavyo, na hufaidika kutokana na baadhi ya kasoro kwenye kanuni na sharia. Kwa hivyo hakuna budi kuwepo taasisi za kusimamia, kuchunguza, ofisi ya malalamiko na vyombo vya habari, ili kuwe na nguvu ya uzuiaji na ubanaji kwa lengo la kutetea haki za raia. Mtu yeyote miongoni mwa wafanyakazi wa Serikali, akihisi kwamba anamiliki kila kitu na ana kinga kamili, ndio huwa sababu ya kuvunja haki za watu na kuwadhulumu yale yenye manufaa na wao. Na wafanyakazi waovu ndio wanaoendeleza hali hii, kwani huinyamazia na kuikubali, katika hali ambayo walipaswa kuibainisha kwa viongozi wa juu, na wawabebeshe majukumu ya ufumbuzi, huenda kiongozi wa juu akawa hana habari juu ya hali hii ya uonevu, kama ambavyo huenda ikadhaniwa kwamba yeye haridhiki nayo.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 81 1/7/2015 11:52:48 AM

Kwa hakika kuenea baadhi ya fikra zisizo sahihi, kunawafanya watu wengi washindwe kutetea haki zao na kueleza dhulma wanayofanyiwa, kwani huchukulia dhana ya kutokuwepo umuhimu wowote wa kufuatilia, na kwamba si serikali inajua kila kinachofanyika, na mfanyakazi huyu ana nguvu, na kupeleka malalamiko huenda kukazidisha mambo kuwa magumu zaidi na kusababisha matatizo mapya. Katika kukabiliana na fikra hizi zisizo sahihi, inapasa kueneza elimu ya uwajibikaji kwa raia, serikali na haki za binadamu, ijulikane kwamba, mwananchi anayedhulumiwa, kisha akapeleka malalamiko yake, basi raia huyo anakuwa anapigania maslahi ya serikali na nchi, hii ni kwa sababu utendaji mbaya wa mfanyakazi yeyote hauisaidii serikali, bali unaidhuru na kuichafua.

Baadhi ya watu wanatosheka na kufanya udanganyifu na kuwatumia wafanyakazi wa serikali katika vikao, bila ya kuwajibika katika kutatua makosa, hiyo ndio sifa ya wale wasiwajibika katika nafasi zao za kidini na kinchi.

**Tatu: Katika Nyanja ya Kijamii:**

Ni katika yale yenye mafungamano na jamii. Kuna uvunjaji wa kufedhehesha wa haki za binadamu katika nyanja ya kijamii. Katika mafungamano ya watu wao kwa wao, mfano wake, ni ukatili wa kifamilia, kama vile kuamiliana na wake na watoto, katika hali ambayo baadhi ya baba hufanya ubabe wa kinyama kwa watoto wao, na kama ambavyo baadhi ya waume huwadhulumu wake zao haki za kibinadamu na za Kisheria, pia katika hali ya kuamiliana na wafanyakazi.

Na katika mafungamano kati ya makundi ya watu katika jamii, hutokea ukandamizaji, kiasi cha kuhitajika kuwepo juhudi kubwa za kutetea haki za binadamu, kwa kueneza elimu na uelewa katika



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 82 1/7/2015 11:52:48 AM

jamii na utambuzi wa haki, na msisitizo juu ya kuchunga maslahi ya watu wengine na kuheshimu mawazo yao na mambo yao binafsi, na kuunda kamati na taasisi za kijamii kwa ajili ya kuleta maelewano, na kusuluhisha matatizo na uchupaji mipaka.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 83 1/7/2015 11:52:48 AM

# KATI YA HAKI NA WAJIBU

Kwa kuzingatia kwamba binadamu ni sehemu katika jamii yake, basi mafungamano yake ni ya pande mbili. Hii ina maana kuwepo wajibu wa kubadilisha haki anazopaswa kuwafanyia wengine na zile anazostahiki kufanyiwa. Na kiasili, haki na wajibu ni mambo yenye maana moja, ambayo ni kuthibiti, imekuja katika kitabu *'Lisanul Arabi'* maelezo yafuatayo:

*Haqqa l-amru yahiqqu wayuhiqqu haqqa wahuquuqa: Swara haqqa wathabata.* Amesema al-Azhariy: Maanau wajaba yajibu wujuuba. Na katika Qur'ani Mwenyezi Mungu amesema: **Qaala ladhiy haqqa alayhil qauli** (Amesema yule ambaye imemthibitikia kauli) ikimaanisha, thabata. Na kauli yake Mwenyezi Mungu: **"Walakin haqqatkalimatul adhabi alal kafiriin"** (Lakini imewathibitikia kauli ya adhabu juu ya makafiri.) ikimaanisha, imewajibikia na imewathibitikia."[46] Na pia imekuja katika kitabu '*Lisanul Arabi'* kuhusu maana ya *Wajib* na *Wujub.* Husemwa: *Wajaba shay-u yajibu wajuba idhaa thabatawalazima."*[47]

Na mtafiti al-Asfahaniy amesema: Ama neno 'Haki' lina maana nyingi katika lugha, na inadhaniwa kwamba maana zote zinarudi katika maana moja. Na zile maana ambazo zinaonekana kuwa hazilingani, ni kutokana na kutoelewa vizuri katika sura ya nje, kwani maana ya ndani ni kuthibiti. Kwa hivyo maana ya asili ya neno 'Haki' ni kuthibiti, na maana yake ya wasifu ni chenye kuthibiti. Kwa mtazamo huu, Mwenyezi Mungu Mtukufu hujulikana kwa jina la Haki (***Haqq***), kwa kuthibiti Kwake kuliko bora zaidi, ambako hakuchanganyiki na kasoro. Na maneno ya ukweli hujulikana kuwa

---

46 Ibn Mandhuri: Muhammad ibn Mukrim, *Lisanul Arabi*, Jz. 2, Uk. 680.

47 Kitabu kilichotangulia, Jz. 6, uk. 878.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 84 1/7/2015 11:52:48 AM

ni haki kutokana na uhakika wake, kama Mwenyezi Mungu anavyosema: **"Na Mwenyezi Mungu huithibitisha haki." "Na imekuwa ni haki (imethibiti) Kwetu kuwanusuru Waumini." "Bila ya shaka kauli imekwisha thibiti juu ya wengi katika wao." "Tukio la haki (lililothibiti)." "Na imekuwa haki juu yangu (imethibiti) ya kwamba nisiseme isipokuwa ukweli"**[48]

Kutokana na maelezo haya, ni kwamba haki na wajibu ni maneno yenye maana moja, na katika utafiti wetu huu, ni kwamba haki ni mambo yaliyothibiti kwa binadamu kuwatendea watu wengine, au kwa wengine kumtendea binadamu, na wajibu ni yale yaliyothibiti kwa binadamu kuwatendea wengine, au wengine kumtendea binadamu, basi haki ni wajibu na wajibu ni haki, na tofauti ni kwa mujibu wa utekelezaji wa binadamu au kutekelezewa.

---

[48] Al-Asfahaniy: Sheikh Muhammad Husein, *Hashiyatu kitabil Makasib*, Jz. 1, Uk. 38.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 85 1/7/2015 11:52:48 AM

## HAKI SAWA:

Mfumo wa maisha ya binadamu katika jamii ni kupata haki anazostahiki, na kutekeleza wajibu wake unaompasa. Na pindi patakapopatikana kasoro yoyote ile, basi itapelekea misuguano katika maisha ya mtu binafsi na ya kijamii. Kwa mfano, katika maisha ya kifamilia, kuna haki za kila upande kati ya wanandoa wawili, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ

**"Nao wanawake wanayo haki kwa mujibu wa Sheria, kama ile haki iliyo juu yao (waume)." (Qur'ani 2:228).**

Basi kila mmoja atakapojilazimisha kutekeleza haki za mwenzake, wataishi katika hali ya raha na starehe. Ama ikiwa upande mmoja utaacha kutekeleza wajibu wake kwa upande wa pili, basi hapo patapatikana misuguano ya kifamilia na kukosekana maelewano, jambo ambalo linaondosha raha ya maisha na kuacha kutekeleza majukumu ya kijamii.

Na kwa upande wa kisiasa, pia nako kuna haki za kupokezana kati ya kiongozi na raia, kati ya mtawala na watawaliwa. Kwa kuchunga haki ya kila upande kunaleta amani na utulivu, na kutoa fursa ya maendeleo ya nchi. Ama mtawala mwenye kuzikandamiza haki za raia, au raia kuchupa mipaka dhidi ya haki za serikali, kunasababisha fitna, fujo na uharibifu.

Hivi ndivyo hali ilivyo katika nyanja zote za maisha ya kijamii na mafungamano ya kibinadamu, kwani hakuna mafungamano kati ya pande mbili, ikiwa ni upande mmoja tu ndio ulio na wajibu wa



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 86 1/7/2015 11:52:48 AM

kutekeleza haki za upande mwingine, na upande mwingine usihusike na hilo. Hata kuhusiana na Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ni Muumbaji, aliyetukuka kwa waja Wake, amemuahidi malipo mema mtekelezaji wa haki Zake miongoni mwa waja Wake.

Imamu Ali (a.s.) ameuelezea ukweli huu wakati alipokuwa akiwahutubia raia wake mwanzoni mwa Ukhalifa wake kwa kusema:

> "Kwa hakika Mwenyezi Mungu amenifanya mimi niwe na haki ya kutawalia mambo yenu, na nyinyi mna haki juu yangu mfano wa ile niliyokuwa nayo mimi juu yenu. Basi haki ni kitu chenye upana mkubwa katika kuielezea, na ni finyu sana katika kutenda usawa. Haimuwii mtu ila pia itakuwa kinyume na yeye, wala haimpitii kinyume naye ila itampitia kwa faida yake. Lau ingekuwa inamuwia yeyote na wala isiwe dhidi yake, hivyo ingekuwa khasa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu wala si kwa viumbe Wake. Kwa sababu ya uwezo Wake juu ya waja Wake, na kwa uadilifu Wake katika kila lipitalo katika maamuzi yake. Lakini Yeye ameifanya haki Yake juu ya waja ni wamtii, na amejaalia malipo yao juu yake ni kuwazidishia thawabu, ikiwa ni fadhila kutoka Kwake, na kutoa wasaa kwa kuwa Yeye ni Mstahiki wa kuzidisha. Halafu Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia katika haki Zake, haki iliyo wajibu kwa baadhi ya watu juu ya wengine, akaifanya sawa katika hali yake. Baadhi ya haki hizi zinazalisha haki zingine, wala baadhi haziwi wajibu ila kwa sababu ya nyingine."[49]

Hakika huu ni msisitizo wa namna ya utekelezaji haki, kwa mtawala kuekeleza haki za raia, na raia kutekeleza haki za mtawala. Huu ndio msingi wa uthabiti katika nyanja zote za mafungamano kati ya pande mbili, kwa kila upande kuekeleza haki za upande wa mwingine.

[49] Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*: Barua Na. 216.

# WAJIBU KWANZA:

Ikiwa binadamu ana wajibu juu ya wengine, kwa kiwango alichonacho yeye cha haki, basi jambo la kwanza la kujenga mafungamano sahihi yenye tija na mwingine, inapasa kuanza na kumtekelezea haki zake za wajibu, jambo ambalo litamshawishi mwingine na kumlazimu na yeye kufanya kama hivyo. Kwa kufanya hivi, mafungamano ya dhati yatasimama. Hii ina maana kwamba, binadamu anatakiwa afikirie yale yanayompasa kuwatendea wengine kabla ya kufikiria yale yaliyo wajibu kufanyiwa yeye, na kutekeleza wajibu wake kabla ya kutaka kufanyiwa yale yaliyo haki kwake. Lakini tatizo la watu wengi ni kujitia hamnazo na kujisahaulisha yale yaliyo wajibu kuyatenda, na badala yake wanatafuta yale yaliyo ya wajibu kufanyiwa wao. Na hii ndio hali anayoielezea Imamu Ali (a.s.) pale aliposema: "Basi haki ni kitu chenye upana mkubwa katika kuielezea, na ni finyu sana katika kutenda usawa." Basi kila mtu huizungumza haki vizuri kwa ufasaha na kuisifu na kuiweka wazi pindi inapokuwa iko upande wake. Haki ni kitu kipana zaidi katika kuelezwa na kubainishwa, ama katika ngazi ya utekelezaji, watu wengi wanashindwa kufanya hivyo. Basi binadamu inampasa aanze na nafsi yake, ajilazimishe kutenda haki za wengine kabla ya kuwataka wengine wamtekelezee haki zake.

Binadamu ni mwenye kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuhusiana na wajibu unaomlazimu kuutekeleza. Basi haki za watu ni sehemu ya wajibu usiotengana na haki za Mwenyezi Mungu, kama Imamu Ali (a.s.) anavyosema: "Halafu Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia katika haki Zake, haki iliyo wajibu kwa baadhi ya watu juu ya wengine." Bali imepokewa Hadithi nyingine kutoka kwake (a.s.) akisema: "Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia haki za waja



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 88 1/7/2015 11:52:48 AM

Wake kuwa ni zenye kutangulizwa juu ya haki Zake, basi mwenye kutekeleza haki za waja wa Mwenyezi Mungu, jambo hilo litampelekea kutekeleza haki za Mwenyezi Mungu."[50]

Na ili mtu asalimike na kuwajibishwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, inampasa awatekelezee watu haki zao. Pindi mtu atakapoharakia kutekeleza haki za mtu mwingine, jambo hili litamthibitishia kutekelezewa haki zake, kwani baadhi ya haki zinawajibisha kutekelezwa haki nyingine, na wala baadhi yake hazina wajibu wa kutekelezwa isipokuwa baada ya kutekelezwa nyingine. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Imamu Ali (a.s.), ambapo jambo hili hujenga msukumo wa kikanuni na wa kibinadamu kwa upande wa pili kulazimika kutekeleza haki za binadamu mwingine.

Binadamu kutekeleza haki zilizo wajibu kwake, ni kutokana na uwezo wake na kwa mujibu wa maamuzi yake. Ama watu wengine kumtekelezea haki zake zimo mikononi mwao, pindi ikiwa hamiliki maamuzi ya kuwaamulia wengine na matakwa yao, basi yeye anamiliki maamuzi yake na matakwa yake, basi yeye awe wa kwanza kutekeleza haki za wengine.

[50] Al-Aamudiy Tamiymiy: Abdulwahid, *Ghurarul Hikam*, Harful Jiim, Na. 64.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 89 1/7/2015 11:52:48 AM

# UBINAFSI:

Watu wengi wamevuka mipaka katika kuziangalia nafsi zao, siku zote wanaona haki iko ule upande walioko wao tu, na daima huzungumzia juu ya wajibu ulioko kwa wengine, bila ya kuangalia wajibu na haki zilizoko juu yao, kama kwamba haki inazunguka pamoja nao popote wazungukapo. Kwa mfano, mdai kumsisitiza mdaiwa juu ya kuharakisha kulipa deni analomdai, na uharamu wa kuchelewa na kutoa muda mara kwa mara. Ama pindi anapokuwa anadaiwa, huwa anasisitiza juu ya mwenye kudai kuvuta subira na kumsomea Aya: **"Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike."** Na hulaumu ung'ang'anizi wa kudai na kuwabana wadaiwa!!

Na wakati atakapofika katika chakula akiwa amechelewa na huku kuna waliomtangulia, hapo huzungumza juu ya haraka isiyopendeza, na hulaumu juu ya kutokuwa na uvumilivu. Ama pindi anapofika mapema na wengine kuchelewa, hulaumu juu kutokuchunga wakati, na kutoa wito wa kuuchunga, kwa vile tu wengine wamechelewa!! Na wakati anapoitoa gari yake kwenye kona na kutaka kuingia kwenye barabara kuu, huwalaumu madereva kutokana na mwendo wao wa kasi na kutotoa fursa kwa mwenye kutaka kuingia kwenye barabara kuu. Ama pindi anapokuwa yeye anaendesha gari yake kwenye barabara kuu, na kumuona anayetoka kwenye kona, atamkabili kwa kumpigia honi yenye maudhi ya gari yake, akidhihirisha kukerwa kwake kutokana na wengine kutokuwa na uvumilivu!!

Hivi ndivyo tunavyoshuhudia misimamo mingi na utekelezaji, misimamo ambayo inatokana na suala la ubinafsi, na kuielezea haki na wajibu kwa mujibu wa matakwa binafsi. Ni mara nyingi tumeona wanamapinduzi wanaopinga serikali za kidikteta, na kunyanyua



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 90 1/7/2015 11:52:48 AM

kaulimbiu ya kutaka uhuru na uadilifu, lakini pindi wanaposhika hatamu za utawala, kipaumbele chao kinakuwa ni kudhibiti utawala na kuleta usalama na utulivu na kuacha fikra ya uhuru na uadilifu, kutokana na kutofautiana misimamo yao na mawazo yao wanayoyaangalia, yana athari katika aidiolojia zao.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 91 1/7/2015 11:52:48 AM

# KUZINGATIA UTEKELEZAJI HAKI:

Ni kwa nini watu wengi wanajisahaulisha kutekeleza haki zinazowapasa kuzitekeleza?

**1.** Kuna ujinga na utelezaji hafifu wa haki, katika hali ambayo wengi hawajui yale yaliyo wajibu kuwafanyia wengine. Mafungamano na maingiliano katika nchi zetu yanakwenda bila ya mipangilio, na kwa mujibu wa mila na ada, ambazo zimeshika hatamu. Kwa mfano, katika maisha ya mke na mume, mume anakuwa katika nafasi ya utawala, hapo haki za mke zinapotezwa na kutozingatiwa, na katika kazi, mkuu wa kazi hazingatii haki za mwajiriwa, na hivi ndivyo hali ilivyo kati ya baba na watoto na kati ya mwalimu na wanafunzi wake…

Kuna haja kubwa ya kutolewa elimu juu ya haki, ambayo itambainishia mtu yale yaliyo wajibu kuyatenda na kutendewa, na kufahamishwa juu ya ulazima wa kuanza kutekeleza yale yaliyo wajibu kwake kutenda. Na wala haina maana kwa mtu kujisahaulisha haki anazostahiki kutendewa, au kutozifuatilia na kunyamaza kimya, bali ina maana kwamba, kutafuta haki zake isiwe ni mbadala wa kutekeleza wajibu wake, na wala mtu asiwape watu wengine majukumu yake huku akiacha nafsi yake kuyatekeleza, bali aanze kuyatekeleza yeye mwenyewe, kisha ndipo awatafute wengine wamsaidie.

**2.** Kitu kingine kinahusiana na malezi ya kiroho na ujenzi wa tabia nzuri ya binadamu, kwa kujikumbusha maelekezo ya mafunzo matakatifu, na hayo yawe ndio kipimo cha msimamo wake na matendo yake. Na kwa upande wa pili, kwa mtu kukubali haki zilizoko juu yake, inamaanisha ubebaji na utekelezaji wa maju-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 92 1/7/2015 11:52:48 AM

kumu yake, na kule kutafuta haki zake anazostahiki kufanyiwa, ni kuwabebesha wengine majukumu.

Imepokewa Hadithi kutoka kwa Imamu Ja'far (a.s.) akisema: "Mwenyezi Mungu hakuabudiwa ibada iliyo bora zaidi, kuliko kutekeleza haki ya Muumini." Na kutoka kwa Imamu Hasan Askariy (a.s.) amesema: "Mtambuzi zaidi wa haki za ndugu zake, na yule mwenye kutekeleza zaidi haki zao, ni mwenye shani (hadhi) kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu." [51]

**3.** Na mara nyingi mtu hujisahaulisha na haki za watu wake wa karibu, kwa misingi kwamba yeye ni kiongozi wao na kwa sababu ya nafasi aliyonayo kwao, kama kwamba hali hiyo inampa ruhusa ya kutowatekelezea haki zao. Kwa kweli hili ni kosa kubwa, kwani kuchunga haki za jamaa wa karibu ni jambo lililo bora zaidi, kwa sababu wao ni watu walio karibu zaidi naye. Na atakapozoea kuwadhulumu haki zao, basi daima wataishi pamoja naye maisha mabaya, kwa hivyo Imamu Ali (a.s.) amesema: "Na watu wako (jamaa zako) wasiwe ni watu waovu zaidi kwako (usiwafanyie utovu wa adabu)."[52]

Pia katika hali ya kuamiliana na marafiki, kudhulumiwa haki zao inatokana na hali ya maingiliano pamoja nao. Hali hii husababisha kuvunjika kwa urafiki, Imamu Ali (a.s.) anasema: "Wala usiipoteze haki ya nduguyo kutegemea (uhusiano) uliopo kati yako na yeye, kwa kuwa si nduguyo uliyempotezea haki yake."[53]

---

[51] Al-Majlisiy: Muhammad Baqir, *Biharul-Anwar*, Jz. 72, Uk. 117.

[52] Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*, Barua Na. 31.

[53] Kitabu kilichotangulia.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 93 1/7/2015 11:52:48 AM

# UTUKUFU WA MAISHA NA TABIA YA DHULMA

Maisha ya binadamu yeyote hupatikana kwa mujibu wa maamuzi ya Mwenyezi Mungu na uendeshaji Wake, kwa hivyo, jaribio lolote la kutaka kuyatoa maisha ya mtu, ni kupingana na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Jambo hilo husababisha kwenda kinyume na mpangilio wa kikanuni na kitamaduni. Kila mfumo ambao haulindi maisha ya binadamu, huo ni mfumo usiokubalika kwa mujibu wa mpangilio wa Mwenyezi Mungu, na kinyume chake, ni kwamba mfumo wenye kulinda maisha ya binadamu, huo ni mfumo unaokubaliana na matakwa ya Mwenyezi Mungu na maumbile ya binadamu ambaye amepewa uhai.

Kwa hivyo, kujiua ni kosa kubwa kwa mujibu wa sheria za kidini na kwa mujibu wa kanuni za kimataifa, bali sheria za Kiislamu zimetofautiana na sheria nyingine kwa kuweka mikakati madhubuti ya kulinda uhai. Zimeharamisha kutoa mimba katika kipindi chochote ambacho kichanga kitakuwa kimeshaumbwa, kwa sababu tayari amekwishakuwepo, basi inapasa kutambuliwa na haifai kufanyiwa uadui.

Na wanachuoni wametoa fatwa ya kwamba haifai kwa daktari kuchomoa mashine za kitabibu za kusaidia mapigo ya moyo alizomuwekea mgonjwa wake hata kama ubongo utakuwa umeshakufa, ikawa maisha ya mgonjwa huyo ni kama maisha ya mmea ambayo hayadumu isipokuwa kwa mashine hizo, hii yote ni kuilinda nafsi tukufu katika Uislamu. Na ni juu ya daktari asitegemee ombi la mgonjwa au jamaa wa karibu wa mgonjwa kuchomoa mashine hizo, na pindi atakapozichomoa, huchukuliwa kuwa ni muuwaji.[54]

[54] Sistaniy: Sayyid Ali al-Husainy, *Al-fiqhu lilmughtaribin*, Mas-ala Na. 352.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 94 1/7/2015 11:52:48 AM

Kama ambavyo wanachuoni walivyotoa fatwa ya mtu aliye baleghe kujidhuru mwenyewe, na ni wajibu juu yake kuacha kufanya hivyo, na kuilinda nafsi yake dhidi ya madhara.

Mtazamo sahihi juu ya maisha ni ule wajibu wa kuyalinda, kwani maisha ni kitu kitakatifu katika Uislamu, pindi tunapofikiria kwa makini kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ
فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا

**"Mwenye kuuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama kwamba amewauwa watu wote." (Qur'ani 5:32 ).**

Tunaikuta Aya Tukufu ikifahamisha kwamba, maisha ya binadamu ni hakika moja, na kumfanyia uadui mtu yeyote ni sawa na kuwafanyia uadui watu wote, kwa hivyo, inapasa kujiepusha na fikra na matendo yanayopelekea mauaji hata kama mlengwa ni mtu wa mbali, kwani ni wajibu kila mtu kuhisi kwamba amefanyiwa uadui. Ibn Ashuri anasema katika tafsiri yake: "Maana ya tashbihi katika kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo: **"Basi ni kama kwamba amewauwa watu wote,"** ni kuhimizwa watu wote juu ya kumuadhibu muuwaji wa mtu, na kumshika popote alipo, na kukatazwa kumficha. Kila mwenye kuhutubiwa na Aya hii atende kwa mujibu wa uwezo wake, na kwa kadiri ya nafasi yake katika nchi. Kwa mfano mkuu wa nchi, ni kwa raia wote, basi makusudio ya tashbihi hii ni kukhofisha mauaji."[55]

Na wala hapa haifai kupinga sheria ya Kiislamu ya kuruhusu kuuliwa muuwaji, kwa sababu mauwaji yamewekewa sheria kali

[55] Ibn Ashuri: Muhammad Twahir, *Tahriru wa-tanwir*, Jz. 5, 89.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 95 1/7/2015 11:52:48 AM

kwa lengo la kulinda maisha ya wengine, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَاةٌ يَا أُولِي الأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

**"Na mna uhai katika kulipiza kisasi, enyi wenye akili." (Qur'ani 2:179).**

Katika hali ya mgongano wa mafunzo mema, basi hutangulizwa yale yaliyo bora zaidi. Huenda kulinda uhai wa muuwaji ikawa ni jambo muhimu, lakini lililo muhimu zaidi ni kulinda maisha ya watu wote. Licha ya sheria hii, Uislamu umetoa nafasi ya kubatilisha adhabu ya kifo kwa muuwaji, iwapo ndugu wa mtu aliyeuliwa watamsamehe muuwaji, bali Uislamu unahimiza jambo hili, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ

**"Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu." (Qur'ani 42:40).**



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 96 1/7/2015 11:52:48 AM

# DAMU NI MSTARI MWEKUNDU:

Miongoni mwa mafunzo ambayo Uislamu umejaribu kuyapandikiza katika nafsi za watu, ili iwe ndio msingi wa ustaarabu madhubuti, ni utukufu wa uhai na wajibu wa kuulinda, na maandiko mengi ya Kidini yamesisitiza mafunzo haya, kwani yametahadharisha mno dhidi ya kuufanyia uadui uhai wa watu wengine. Katika Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), inaeleza kwamba kosa lolote analolifanya mja, kuna matarajio ya kusamehewa, lakini atakapofanya ujasiri wa kumwaga damu ya mtu asiye na hatia, ni kwamba jambo hili halina msamaha. Kutoka kwa Ibn Umar, kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mja hatoacha kuwa katika wasaa wa dini yake, ikiwa hajamwaga damu kwa njia ya haramu."[56]

Na pia katika hadithi nyingine kutoka kwake (s.a.w.w.), inaeleza kwamba umwagaji wa damu ndio jambo la mwanzo litakalohukumiwa katika uwanja wa Siku ya Kiyama. Kutoka kwa Ibn Masoud, amesema Mtume (s.a.w.w.): "Jambo la mwanzo litakalohukumiwa kati ya watu Siku ya Kiyama, ni umwagaji damu."[57] Na mfano wa Hadithi hii pia imepokewa katika kitabu '*Wasailu Shi'ah'* kutoka kwa Imamu al-Baqir (a.s.).[58] Na kutoka kwa Ibn Umar, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Tahadharini funda la damu lisimzuie mtu kuingia Peponi."[59]

Pia maandiko ya Kidini yanaeleza kwamba mwenye kuongoza mauwaji anakuwa ni mshiriki katika kosa hilo. Kutoka kwa Ibn Abbas, Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mwenye kushiriki katika damu

[56] Al-Hindiy: Ali Muttaqiy, *Kanzul Ummal*, Hadithi Na. 39907.
[57] Al-Qshayriy Nisaburiy, Muslim ibn Hujjaj, *Sahihi Muslim*, Hadithiu Na. 1678.
[58] Hurrul Amiliy: Muhammada ibn Hasan, *Wasailu Shi'ah*, Hadithi Na. 35026.
[59] Al-Hindiy: Ali Muttaqiy, *Kanzul Ummal*, Hadithi Na. 39922.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 97 1/7/2015 11:52:48 AM

(mauwaji) hata kwa neno moja, atakuja Siku ya Kiyama akiwa ameandikwa kati ya macho yake: 'Mwenye kukata tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu.'"[60] Hakika dunia imeumbwa kwa ajili ya binadamu, na wala haitakuwa na thamani ikiwa maisha ya binadamu hayataheshimiwa.

Na kuna tukio lililotokea wakati wa zama za Mtume (s.a.w.w.), tukio ambalo linabainisha namna Uislamu unavyojishughulisha na uhai. Ni kwamba siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimkuta mtu aliyeuawa. Mtume (s.a.w.w.) alikasirika sana, kwa hivyo akawataka Waislamu wakusanyike msikitini, na baada ya kukusanyika alipanda mimbari na kuwahutubia kwa kusema: "Enyi watu, inakuwaje mtu auwawe na asijulikane aliyemuuwa? Naapa kwa Mwenyezi Mungu, lau kama viumbe wa mbinguni na ardhini watashirikiana katika damu ya Mwislamu mmoja asiye na makosa, au wakaridhika na mauwaji yake, basi itakuwa ni haki kwa Mwenyezi Mungu kuwatupa wote kifudifudi katika Moto wa Jahannam."[61]

Na imepokewa katika Hadithi kwamba baada ya Mtume (s.a.w.w.) kumaliza ibada ya matendo ya Mina, alisimama mbele ya watu na kuwahutubia kwa kusema: "Enyi watu, ni siku gani iliyotukufu zaidi?' Waislamu walisema: 'Ni siku hii.' Alisema: 'Ni mwezi gani uliomtukufu zaidi?' Walisema: 'Ni mwezi huu.' Alisema: 'Ni nchi gani iliyotukufu zaidi?' Walisema: 'Ni nchi hii.' Alisema: 'Basi damu yenu na mali zenu zina utukufu kama ilivyo na utukufu siku yenu hii na mwezi wenu huu na nchi yenu hii."[62]

Na mwenye kufuatilia maisha ya Mtume (s.a.w.w.) atagundua kwamba kulikuwa na ulindaji na tahadhari kubwa dhidi ya umwagaji wa damu. Wanahistoria wamehesabu vita 83 vilivyotokea ka-

[60] Kitabu kilichotangulia, Hadithi Na. 39935.
[61] Al-Majlisiy: Muhammad Baqir, *Biharul An-wari*, Jz. 72, Uk. 150.
[62] Bukhariy: Muhammad ibn Ismail, *Sahihil Bukhariy*, Hadithi Na. 67.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 98 1/7/2015 11:52:48 AM

tika zama za Mtume (s.a.w.w.). Licha ya wingi wa vita hivyo, idadi ya waliouwawa hawakuzidi watu 1400 miongoni mwa Waislamu, Mayahudi na washirikina, katika wakati ambao katika zama hizo watu wengi walikuwa wakishiriki vita, kama ambavyo katika zama hizi vita huchukua roho za mamilioni ya watu. Hii inadhihirisha hali ya unyama inayotawala akili za watu wa zama hizi. Basi mfumo wa maisha ya Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa ni kuonesha kivitendo thamani ya uhai. Kutokana na utukufu wa uhai na kutoa fursa ya kuishi kwa wema, Mtume (s.a.w.w.) aliwaacha huru mateka kwa kuwaambia: "Nendeni, kwa hakika nyinyi mko huru." Na hivi pia ndivyo ilivyokuwa mwenendo wa Imamu Ali (a.s.), ambaye alikuwa akikubali udhuru na kutokuchukua hatua wakati wa shaka, kwa lengo la kulinda uhai wa watu wengine.

# MAFUNZO YALIYOPOTEA:

Mafunzo ya kuheshimu uhai yameghibu katika akili za Waislamu wengi wa zama hizi, katika hali ambayo tunashuhudia nchi zilizoendelea zimenufaika na mafunzo ya kujali uhai, mafunzo waliyoyarithi kutoka kwenye mafunzo ya Mitume, ikawa wanaasisi mifumo na kanuni zenye kuheshimu uhai wa binadamu, mpaka ikawa ni sehemu ya mafunzo ya nchi za Ulaya. Licha ya unyama wanaoufanya kwa watu wengine, ila wao wanawaheshimu raia wao, kwa mfano, pindi raia wa Marekani anaposibiwa na tatizo, taasisi zote za kiserikali hujishughulisha naye, na vyombo vyote vya habari hueleza habari zake. Hali hii pia iko kwa wazayuni (mayahudi). Ni watu wenye kuheshimiwa ulimwenguni, hii ni kwa sababu ya kujiheshimu wenyewe. Makubaliano ya kubadilishana wafungwa na Hizbullahi huko Lebanon ni dalili tosha juu ya hilo. Ni kwamba mazungumzo yao yalichukua miaka mingi na kushiriki taasisi mbalimbali za kimataifa katika mazungumzo hayo. Na Israili ilikubali kuachana na misimamo yake mingi kwa ajili ya kuachiwa huru mateka mmoja na kurejeshwa miili ya watu watatu, jambo ambalo lilimfanya katibu mkuu wa Hizbullahi, Sayyid Hasan Nasrullahi kubainisha kwa uwazi pale aliposema: "Licha ya uadui tunaoishi pamoja na Israil na kutambua makosa yao, lakini inatupasa tujue namna wanavyowaheshimu raia wao."

Katika wakati ambao watu wengine wanaishi katika utamaduni wa kuheshimu uhai wa wengine, tulio wengi miongoni mwetu sisi Waislamu tunaishi katika utamaduni wa kuudhulumu uhai wa wengine, utamaduni ambao umepenya katika ufahamu wetu na kuwa ndio mwenendo wetu katika mambo mengi tunayoyafanya kwa ku-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 100 1/7/2015 11:52:49 AM

tokujali. Kwa mfano wa karibu juu ya hili, ni uendeshaji mbaya wa gari katika barabara kuu na kutokuchunga kanuni za barabarani, kwani kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1424A.H. idadi ya ajali za magari katika nchi ya Saudia Arabia zilifikia 300,000, katika hizo watu 4,000 walipoteza maisha, na watu 4,000 walijeruhiwa, na watu 30,000 walikuwa ni miongoni mwa majeruhi na waliopata ulemavu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 101 1/7/2015 11:52:49 AM

# HARAKATI ZA KIGAIDI:

Ikiwa hatuwezi kujitetea kutokana na ukubwa wa ajali za barabarani, isipokuwa kutokujali maisha ya wengine, basi tunaziweka wapi shughuli za kigaidi ambazo zinawalenga watu wasio na hatia katika hali ya uwendawazimu wa kuuwa watu? Hii inaonesha ujinga wa hali ya juu walionao watu, kwa hivyo inapasa kuharakisha kutatua tatizo hili kwa kuzidisha mtazamo mpya wa kielimu, ambao utasisitiza juu ya utukufu wa uhai wa mtu ambao haustahiki kudhulumiwa kwa anuani yoyote ile. Je, usia wa Mtume (s.a.w.w.) kwa wapiganaji juu ya kutowashambulia wazee, wanawake, watoto na mazao wakati wa vita, haukuwa mfano bora wa kuigwa? Kwa hakika ilikuwa ni msingi wa maisha ya binadamu, kama anavyosema Imamu Ali (a.s.): "Watu wako wa aina mbili, ama ni ndugu yako katika Dini, au ni mfano wako katika maumbile."[63]

Kile ambacho kilishuhudia mji wa Riyadhi siku ya Jumatano, tarehe 2, Mfunguo Sita mwaka 1425A.H. mlipuko uliolenga jengo la serikali ambalo ndani yake lilikuwa na makao makuu ya usalama wa barabarani, kikosi maalumu cha mambo ya dharura, na idara ya upelelezi ya makosa ya jinai, kinabainisha wazi namna watu waliotenda kosa hilo walivyokosa akili, na kuwa kwao mbali na mafunzo ya Kiislamu. Kwa hivyo sisi tunalaani matukio yote ya kigaidi yanayotokea hapa Saudi Arabia na yanayotokea pahala popote, kama yale yaliyotokea Basra, Karbala na Najaf, ambayo yalipoteza roho za mamia ya watu huko Karbala. Na yale yaliotokea kabla ya haya huko Morocco, katika kisiwa cha Bali huko Indonesia na matukio mengineo ya kigaidi yenye kufedhehesha. Na jambo la kutisha zaidi ni mlipuko uliolipua treni huko Madrid Hispania. Mwanzoni serikali ya Hispania ilitangaza kwamba, mlipuko huo hauna mafungamano

[63] Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*: Hotuba Na .53, Uk. 427.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 102 1/7/2015 11:52:49 AM

yoyote na Waislamu, na ulitekelezwa na waasi wa ITA wanaotaka kujitenga, lakini kundi la magaidi lenye kujinasibisha na Uislamu lilitoa taarifa kwamba linahusika na mlipuko huo, kana kwamba linajifakharisha na kosa hilo.

Umma unahitaji mafunzo mapya ya kumzindua Mwislamu, huenda tukaweza kutibu majaraha ambayo yameletwa na mafunzo ya ukandamizaji wa uhai, na hapo tutaweza kuchora ubao wa maadili mema ya sura ya Uislamu wa kiuhakika, ambao umechafuliwa mbele ya watu wengine na watu wenye akili mbovu, mpaka ugaidi umekuwa ni alama ya wazi miongoni mwa alama za Uislamu kwa mujibu wa mtazamo wao.

Ni haki ya kila mtu kupinga mfumo wa siasa anaouona una kasoro, lakini hiyo haimpi haki ya kufanya jambo lolote lile, bali njia yake ya kufikia lengo iwe ni njia ya haki, kwani kuna njia nyingi za kiistarabu ambazo zinampa mtu fursa na haki ya kuwa mpinzani, bali njia hizo ndizo zenye kuleta tija zaidi. Uzoefu na historia vimeonesha kwamba shughuli za kigaidi sio njia bora ya kufikia katika malengo ya kisiasa, na uzoefu wa wanaharakati za Kiislamu katika nchi ya Algeria na Misri ni dalili tosha. Kwa hivyo njia ya kigaidi haikubaliki, kwa sababu inapingana na heshima ya uhai wa mtu na wala haiendani na msamiati wowote katika misamiati ya mafunzo ya Kiislamu.

# DHULMA JUU YA UHAI:

Dini hii Tukufu ambayo inauheshimu uhai, na kuzingatia kwamba kuudhulumu ni kosa kubwa sana, basi ni vipi tabia ya kuudhulumu uhai imetawala kwa baadhi ya wafuasi wake? Na ni vipi imekuwa ndio nguo ya kosa lenye kufedhehesha katika kuudhulumu uhai?

Gazeti moja la Kisaudia liliripoti kwamba kijana mmoja kutoka Indonesia aliyekuwa akiitwa Ruusuliy Sadiy, aliyekuwa na umri wa miaka 26, alikwenda kufanya ibada ya Hijja mwaka 1423A.H., alijirusha kutoka katika ghorofa ya tisa ya hoteli katika barabara ya Ummul Quraa katika mji wa Makka, akiwa ameacha ujumbe wenye maana ya kwamba alisikia kuhusiana na ubora wa mtu mwenye kufa katika mji wa Makka, ni kwamba mtu huyo ataingia Peponi, basi aliamua asipitwe na fursa hii adhimu, alimuaga mke wake kwa kumuambia: "Kwa heri, tutaonana Peponi!!"[64]

Na katika tukio jingine, askari wa Msikiti Mtukufu wa Makka alimkamata hujaji mmoja kutoka Ulaya, kwa sababu ya kumchoma kisu mgongoni hujaji kutoka Yemen, kwa madai kwamba yule hujaji anayetoka Yemen ni Masihi Dajjali! Alieleza kwamba, kabla ya kuelekea kwake Makka aliona kwenye ndoto kwamba atafanikiwa kumuona Masihi Dajjali katika maeneo ya Hijja, akiwa na ndevu ndefu na jicho zuri, wasifu huo ndio aliokuwa nao Hujaji kutoka Yemen aliyejeruhiwa. Kwa hivyo alikuwa akimfuatilia wakati wa kutufu na kisha kumshambulia huku akisema: "Hakika huyu ni Masihi Dajjali… Masihi Dajjali." Ilielezwa kwamba hujaji huyo kutoka Ulaya umri wake ulikuwa kwenye miaka ishirini na alikuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Kiislamu kulichoko Madina![65]

[64] Ukadhi: Gazeti la kila siku, linalotolewa na taasisi ya Ukadh, tarehe 4|12|1423A.H.

[65] *Al-Watan*: Gazeti la kila siku la Saudi Arabia, tarehe 23, Februari, 2002 A.D.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 104 1/7/2015 11:52:49 AM

Kama ambavyo pia vyombo vya habari vilitangaza ya kwamba askari wa Ujerumani alimkamata mhamiaji wa Kituruki aliyekuwa na umri wa miaka 59, ambaye aliwauwa Waturuki wawili kwa kuwapiga risasi baada ya Swala ya Alfajiri katika msikiti, kwenye kitongoji cha Galzanakirshin, Magharibi mwa Ujerumani, muuwaji alikiri kosa kwa madai kwamba hao watu wawili aliowauwa walikuwa wakitamka matamshi yaliyokuwa yakishusha heshima yake na kugusa heshima ya mke wake. Ilikuwa inajulikana namna muuwaji alivyokuwa akishikamana na dini yake na kutekeleza Swala na kufunga safari ya kwenda kufanya ibada katika mji Mtukufu wa Makka.[66]

Je si jambo la kutisha kufanywa vitendo hivi na watu wanaoishi katika mazingira ya Kidini? Je, hiyo haiashirii juu ya kuwepo kasoro katika mafunzo wanayoyapokea? Ni sawa kwamba hali hizi ni za nadra, lakini kinaporudiwa inabidi kipengele cha tahadhari kitupeleke kwenye uchunguzi na utafiti wa kile kinachosababisha haya.

Na katika mwenendo huu, kunafanyika kosa la uadui na mauwaji chini ya anuani ya kulinda heshima na kosa la heshima, nayo ni kwa baba au kaka au ndugu mdogo wa kiume au mke kumuua mwanamke wakati anapomtuhumu katika mwenendo wake wa kitabia (hata anapomdhania kufanya uzinifu), uadui huu umekithiri sana katika nchi ya Jordan, kwa sababu kanuni za huko zinasahilisha kosa hili. Kwa kweli wanawake wengi wamepoteza uhai wao kwa namna mbaya na ya kufedhehesha kwa kupitia mikono ya ndugu zao wa karibu kwa sababu ya kudhaniwa tu!! Na misururu ya watu huenda kumpongeza na kumuunga mkono muuwaji. Kila mwaka wanawake wasiopungua 25 huuwawa kwa namna hii katika nchi ya Jordan.

Shirika la kimataifa la kutetea haki za binadamu limesema katika ripoti yake ya mwaka 1999 kuhusiana na Pakistan: Kila mwaka mamia ya wanawake wanauwawa kwa anuani ya kifo cha kulinda

[66] *Al-Hayatu*: Gazeti la kila siku, linalotolewa London, siku ya Jumatatu, 27|1|2004 A.D.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 105 1/7/2015 11:52:49 AM

heshima, na ni nadra kwa wauwaji kufikishwa kwenye vyombo vya sharia. Mnamo tarehe 6 Januari 1999 msichana aliyekuwa akiitwa Ghazala alichomwa moto, na ikajulikana kwamba kaka yake ndiye aliyemchoma mpaka akafariki katika mji wa Jawhar Aabad katika jimbo la Panjab, kwa sababu familia yake ilikuwa inamshutumu ya kwamba alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na mmoja wa majirani, imeelezwa kwamba mwili wake uliokuwa umeungua usiokuwa na nguo, ulibakia njiani kwa muda wa saa mbili, kwa sababu watu wote walikataa kujiingiza katika kadhia hiyo.[67]

Na sasa hivi kunafanyika vitendo vya kujilipua na kigaidi ambavyo vinawalenga watu wasio na hatia miongoni mwa wanaume, wanawake na watoto chini ya anuani ya Jihadi na kupambana dhidi ya makafiri na wale wanaowaunga mkono, hii ikiwa ni matokeo ya mafunzo ya kudhulumu uhai, na kwa masikitiko makubwa zaidi hufanywa kwa jina la Dini!

---

[67] Shirika la kimataifa la kutetea haki za binadamu, ripoti Na 33 ASA, 2,99, iliomo kwenye tofutti *amnesty-arabic.org*



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 106 1/7/2015 11:52:49 AM

# KUKATAZA MAOVU KWA UPOLE NA KWA AJILI YA KULETA MANUFAA

Uislamu unaheshimu uhuru wa mtu na kulipa umuhimu mkubwa jambo hili katika sheria zake na mafunzo yake. Uhuru kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislamu, ni jambo takatifu, haifai kulikosa, na wala haifai kwa mtu kupindukia mipaka katika uhuru wake, na kugeuka kuwa mtumwa wa wengine. Imamu Ali (a.s.) amesema: "Usiwe mtumwa wa mwingine, na ilihali Mwenyezi Mungu amekufanya huru."[68] Na wala haifai kwa wengine kuuhujumu uhuru wa watu wengine: "Tokea lini mmewafanya watu watumwa na ilihali mama zao wamewazaa wakiwa huru."

Na wala hakuna vipengele maalumu vya uhuru wa binadamu, bali inahusisha kila kipengele katika nyanja za maisha yake. Uhuru uko katika kuchagua dini, itikadi na mrengo fulani, uhuru katika harakati za kiuchumi, kiasi ambacho wanachuoni wamekuja na kanuni katika kanuni za muamala, ambayo wameiita 'Kanuni ya Kutawalia.' Kanuni hiyo inasema: "Watu wametawalishwa juu mali zao." Uhuru huu uko katika kila jambo lilioko chini ya uendeshaji wa binadamu mwenyewe.

Licha ya Uislamu kukiri juu ya uhuru huo kwa namna ambayo dini nyingine wala tamaduni nyingine hazijaufikia, isipokuwa kuna baadhi ya wajibu ambao kwa mara ya kwanza binadamu huenda akadhani unagongana na uhuru wa binadamu. Huenda baadhi ya watu wakauliza: Wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya uko kwenye nafasi gani, licha ya Uislamu kutoa hakikisho la uhuru wa binadamu?!

[68] Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*, Barua Na.31.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 107 1/7/2015 11:52:49 AM

Dhahiri ya uamrishaji mema na ukatazaji mabaya ni mambo yanayoingilia uhuru wa wengine, kwani unakuwa unaamrisha kitu ambacho wengine wamekiacha, na kukataza kitu ambacho wanakifanya kwa maamuzi yao na kwa kukipenda. Na lau kama walikuwa ni wenye kutenzwa nguvu kusingekuwa na sababu ya kuamrisha na kukataza.

Na hata daraja lililo dhaifu zaidi la kuamrisha mema na kukataza mabaya, kiuhalisia wake linaonekana ni kuingilia uhuru wa mtu, kwani daraja la kwanza la kuamrisha mema na kukataza mabaya ni kuchukia moyoni, ama la pili ni kutumia ulimi, na la tatu ni kutumia mkono. Haya ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema: "Yeyote mwenye kuona uovu, basi aukataze kwa mkono wake, asipoweza aukataze kwa ulimi wake, asipoweza auchukie moyoni mwake, na huo ni udhaifu mkubwa wa imani."[69] Kidhahiri daraja hizi tatu zinaingilia uhuru wa binadamu. Basi ni vipi tunafahamu wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya ndani ya ufahamu wetu wa uhuru wa binadamu?!

Kuna umuhimu wa kufahamu ili kuondosha mawazo yasiyo sahihi ambayo yapo kwa baadhi ya watu ambao wameacha wajibu huu wa kuamrisha mema kwa sababu ya ufahamu wao usio sahihi, na kudhania kwamba ni wajibu unaopingana na uhuru wa watu wengine. Pindi unapowauliza baadhi ya watu wengine, kwa nini huamrishi mema, au kukataza maovu? Jawabu lake huwa ni kama lifuatavyo: Tufanye nini na ilihali watu wanatumia uhuru wao? Na hata wale wanaotenda maovu na maasi wakati unapowaamrisha au kuwakataza kitu, jawabu lao linakuwa kama lifuatavyo: Mimi ni mtu huru, nafanya nilitakalo! Na baadhi yao hukuambia kwa ulimi mkali: "Wewe siye uliyeuwasha moto wangu, basi niache na mambo yangu."

[69] Qushayri: Muslim ibn Hajjaj, *Sahihu Muslim*, Hadithi Na. 78.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 108 1/7/2015 11:52:49 AM

Maneno yao haya yote ni kuonesha namna walivyochanganyikiwa kuliko kukubwa… Ni kwa nini? Ni kwa sababu uhuru wa binadamu haumaanishi kutoka nje ya mzunguko wa hukumu za Kiislamu. Kama ambavyo Uislamu unaheshimu uhuru wa binadamu, pia unawaamrisha wale waliobaleghe kutekeleza wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya, wajibu ambao ni miongoni mwa nguzo zenye umuhimu, huenda umuhimu wake unazidi nguzo nyingine, kama vile Swala, Funga, Hijja, Zaka…

Kutokana na maneno haya, Imamu Ali (a.s.) anasema maneno muhimu na yenye mazingatio: "Na matendo mema yote na Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, si lolote mbele ya kuamrisha mema na kukataza maovu ila ni kama tone katika bahari kuu."[70] Na katika Hadithi nyingine kutoka kwake (a.s.) anasema: "Kuamrisha mema ni amali bora zaidi ya viumbe."[71] Na katika Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) anasema: "Kuamrisha mema na kukataza mabaya ni njia ya Mitume na mwenendo wa watu wema. Ni nguzo kubwa ambayo kwayo husimamishwa nguzo nyingine, na kuyapa usalama madhehebu (Ushia), na kulifanya halali chumo, na kuzuia dhulma, na kuiimarisha nchi, na kusalimika na maadui na jambo (Uislamu) kuweza kusimama barabara."[72]

Je, Kuamrisha mema na kukataza maovu kunakinzana na uhuru wa binadamu au laa?

**Jawabu:** Ni kwamba hakuna kukinzana wala kupingana, kwa sababu Uislamu unaweka wajibu katika mipaka isiopingana na uhuru wa binadamu, bali ni kinyume ya hayo, kwani jambo hili linachunga uhuru wa binadamu na kutoa dhamana ya maridhawa kwa binadamu… Na malengo na makusudio ya wajibu huu wa kuam-

[70] Sharifu Radhiy: *Nahjul Balaghah*, Hwkima Na. 374.

[71] Al-Aamudiy at-Tamiymiy: Abdul Wahid, *Ghurarul Hikam*, Hadithi Na. 1198.

[72] Hurrul Amiliy: Muhammad ibn Hasan, *Wasailu Shi'ah*, Jz. 16, uk. 119.

risha mema na kukataza mabaya ambayo Uislamu umeyaweka ni kama yafuatayo:

**Kwanza: Kutaka Kumnufaisha Binadamu:**

Wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya unalenga kumkinga binadamu dhidi ya maovu na mambo ya hatari yenye kungamiza ambayo huenda akatumbukia ndani yake, ikiwa hakutanababahishwa. Pindi binadamu anayetembea barabarani akitanababahishwa kuhusiana na uwepo wa shimo, hiyo ni kwa ajili ya manufaa yake ili asitumbukie humo na kudhurika. Si jambo liingialo akilini wakati huo kuambiwa kwamba umeingilia uhuru wake. Pia pindi unapomnasihi mtu asile chakula chenye sumu, si mantiki wakati huo kukuambia kwamba yeye yuko huru na wewe huna haki ya kuingilia mambo yake. Hiyo ni kwa sababu wewe unamtakia manufaa, lakini ni haki yake awe na matumaini juu ya amri yako au katazo lako, na sio akatae msingi wa suala la kuamrisha mema na kukataza mabaya. Kwa sababu Uislamu unawataka wafuasi wake waishi katika hali ya kutakiana manufaa, na kueneza upendo katika nyoyo zao wa kupendana wao kwa wao, basi mmoja amuamrishe mwenzake yale yaliyo na manufaa kwake, na kumkataza yale yaliyo na madhara kwake. “Mpendelee ndugu yako yale unayoyapenda wewe, na chukia kwake yale unayoyachukia kwako.” Huo ndio ulinganio wa kwenye kheri, ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka watu wa umma wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kuutekeleza:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 110 1/7/2015 11:52:49 AM

**"Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unaoamrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio waliofanikiwa." (Qur'ani; 3:104).**

**Pili: Kuonesha Upendo wa Dhati kwa Binadamu:**

Ni namna gani inapasa tuwaangalie watenda maovu na maasi ambao ni wajibu waamrishwe wema na kukatazwa mabaya? Baadhi ya watu wanayaangalia maovu na watenda maovu kwa kutowajali na kushika msimamo wa kuyaangalia tu yale yanayofanyika! Hii ni kutokana na sababu zifuatazo:

**Kwanza:** Ni kuwepo aina fulani ya ubinafsi kwa kutokujali manufaa ya wengine.

**Pili:** Huo ni msimamo asiouridhia Mwenyezi Mungu Mtukufu, bali msimamo huo ni kumuasi Mwenyezi Mungu, kwani kuridhika na maasi na kuyanyamazia, ni kumuasi Mwenyezi Mungu, kisha natija ya hayo yote ni kuyadhuru maslahi ya jamii, kwani kuendelea kuwepo maasi bila ya kubadilishwa, ina maana ya kuwaweka wanajamii katika maangamizi.

Na baadhi ya watu huchukua misimamo mbalimbali juu ya watenda maasi, ambayo ni ya kuwaadhibu na kuwatesa. Msimamo huu ni wa hatari sana, kwa sababu Uislamu unatutaka tuwaangalie watenda uovu kwa jicho la huruma na upole, kwani mtenda uovu ni mtu mgonjwa katika nafsi yake na roho yake, na sio katika mwili wake. Je inafaa kwa mtu pindi anapomuona mgojwa amchukie na kumkasirikia? Na je, ni juu ya daktari amuadhibu mgonjwa, au ni juu yake amuonee huruma kutokana na hali yake na kufikiria namna ya kumtibu?

Wakati wa zama za Mtume (s.a.w.w.) kulitokea tukio lifuatalo: Alipelekwa mlevi, basi Mtume (s.a.w.w.) aliwaamuru Maswahaba



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 111 1/7/2015 11:52:49 AM

zake wamwadhibu kwa mujibu wa sharia. Kisha wakawa wanasema: "Je, humuonei haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa kufanya hivi? Baada ya Mtume (s.a.w.w.) kuondoka, ikawa watu wanamwapiza na kumtusi, msemaji akawa anasema: "Ewe Mola Wangu mdhalilishe! Ewe Mola Wangu mlaani! Mtume (s.a.w.w.) akasema: Msiseme hivi, msiwe shetani kwa ndugu yenu, lakini semeni: Ewe Mola Wangu, msamehe na muongoe."[73]

Na wakati ilipokuwa kusudio la nasaha na kuamrisha mema na kukataza maovu, kuwa ni tiba ya maradhi ya mtenda maasi, basi hakuna budi kutibiwa kwa njia yenye madhara madogo zaidi, na kuigusa shakhsia yake. Kumlaani na kumtukana, kamwe hakutotibu tatizo, huenda ikawa ni sababu ya kuendelea kufanya maovu… Ama kumlingania kwa lengo la kumuongoa na kumtakia wema, na kwa kutumia hekima na mawaidha mazuri wakati wa kuzungumza naye, huenda kukawa na tija kubwa katika moyo wake na kubadili tabia yake. Kwa hivyo inawapasa wale wenye kulingania mema na wenye kutoa nasaha kufikiri njia na namna inayonasibiana, kama vile kuzungumza naye kwa maneno yenye kuvutia, na kutogusia maasi na dhambi anazozitenda, ili huyu mtengenezaji aweze kupata upendo wake kwanza, kisha baada ya hapo ampe angalizo, au amtanabahishe juu ya kosa na dhambi anayoifanya, hii ndio njia ya kutumiwa na wenye kutengeneza.

**Tatu: Kutomfedhehesha Mtu kwa Watu Wengine:**

Ni juu ya mtu mwenye kutengeneza jamii kuacha kumfedhehesha mtenda dhambi na kuitangaza dhambi yake. Kuamrisha mema na kukataza mabaya ni wajibu. Ama kumfedhehesha mtu ni jambo lililo haramu, na mwenye kufanya hivi anakuwa miongoni mwa wale aliowaeleza Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya hii:

[73] Kandahalawiy: Muhammad Yousuf, *Hayatus Swahaba*, Jz. 3, uk. 512.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 112 1/7/2015 11:52:49 AM

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ آمَنُوا
لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ
لَا تَعْلَمُونَ

**"Hakika wale ambao wanapenda kueneza uchafu kwa walioamini watapata adhabu chungu duniani na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." (Qur'ani 24:19).**

Na ikiwa mwenye kufedhehesha akishtaki hatakuwa na ushahidi unaothibitisha madai yake na tuhuma zake anazomtuhumu mtu fulani ya kwamba anatenda dhambi, basi hapo itafaa kwa mwenye kutuhumiwa kulipeleka shauri lake kwa hakimu wa kisheria ili huyo msingiziaji aadhibiwe adhabu ya kutuhumu, na hata kwa hakimu wa kisheria haipasi kumsingizia mtu makosa ikiwa hana ushahidi.

Ama yule mwenye kutenda maasi dhahiri shahiri mbele ya watu, itakuwa amejifedhehesha mwenyewe, na kwa hivyo hana haki ya kuheshimiwa, kwani hakuna yeyote aliyemvunjia heshima, bali amejivunjia heshima mwenyewe. Kuna tofauti kubwa kati ya mtu anayetenda dhambi kutokana na udhaifu fulani unaojitokeza, na yule ambaye anakusudia kufanya maasi mbele za watu. Huyu wa pili inafaa kutomheshimu, kwani yeye mwenyewe hakujiheshimu.

Ama huyu mtu wa kwanza inafaa asaidiwe ili aachane na udhaifu alionao, na hatua muhimu kwenye jambo hili ni kumfichia uovu wake, kwani kubakia kuwa ni mwenye kutajwa vizuri na watu ni hatua yenye manufaa ya kuweza kuacha maasi yake. Ni kama kwamba tumempa fursa njema ya maisha yenye heshima baada ya kuwa heshima yake imechafuka. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: "Mwenye kusitiri uovu wa Muumini, ni kama kwamba amem-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 113 1/7/2015 11:52:49 AM

fufua mtoto wa kike aliyezikwa akiwa hai."[74]

Na Imamu Hasan (a.s.) amesema kuhusiana na haki ya rafiki: "Pindi anapokuona na kosa hulirekebisha na akikuona na jambo jema hulihesabu." Na kwa upande mwingine, hakuna mtu asiyekuwa na mambo ya aibu au makosa, basi yule atakayeona mambo ya aibu ya ndugu yake, haifai kufurahi, kwani yeye hajui ni kosa gani atakalolitenda baadaye. Imamu Ali (a.s.) anasema: "Usifurahike kwa kosa la mtu mwingine, kwani hujui, kwani wewe humiliki kutenda wema siku zote."[75]

Kwa vile binadamu hamiliki hali ya kutotenda maasi (si maasumu), basi ni juu yake asimfedheheshe mtu mwingine. Na asipofanya hivyo, basi Mwenyezi Mungu atamfedhehesha, na je mtu anapenda afedheheke? Mtume (s.a.w.w.) anasema: "Usichunguze makosa ya Waumini, kwani mwenye kuchunguza makosa ya Waumini, Mwenyezi Mungu atamfichulia makosa yake. Basi ambaye Mwenyezi Mungu atamfichulia makosa yake, atamfedhehesha hata kama ni ndani ya nyumba yake."[76]

Ilitokezea kwa baadhi ya watu waliokuwa na tabia ya kudhihirisha aibu za watu, na wala nasaha za kuwataka waachane na tabia hiyo hazikuwasaidia, mpaka pale ilipowajia siku ambayo Mwenyezi Mungu aliwafedhehesha mbele ya watu kutokana na aibu walizokuwa wakizifanya ndani ya nyumba zao. Hiyo ni kutokana na kauli za wake zao ambao husema aibu zao na makosa yao wakati wanapogombana.

Kuna mtu alimwambia Mtume (s.a.w.w.): "Napenda Mwenyezi Mungu anisitiri aibu zangu." Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Zisitiri

[74] Al-Hindiy: Ali Muttaqiy, *Kanzul Ummal*: Jz. 2, Uk. 249, Hadithi Na. 6388

[75] Al-Amudiy Tamiymiy: Abdul Wahid, *Ghurarul Hikam*, Faslu ya 75, Hadithi Na. 144.

[76] Al-Majlisiy: Muhammad Baqir, *Biharul An-war*, Jz. 72, Uk.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 114 1/7/2015 11:52:49 AM

aibu za ndugu zako, Mwenyezi Mungu atazisitiri aibu zako."[77] Bali hata huko Akhera Mwenyezi Mungu atazisitiri aibu za wakosaji kwa sababu ya kuzisitiri aibu za ndugu zao hapa duniani, Mtume (s.a.w.w. amesema: "Mwenye kumsitiria ndugu yake uovu aliouona akiufanya, basi Mwenyezi Mungu atamsitiri duniani na Akhera."[78]

Hakika kuamrisha mema na kukataza mabaya sio tu kuzungumzia juu ya makosa anayoyafanya mkosaji, bali ni mapenzi ya dhati ya yule mwenye kutaka kuleta manufaa kwa ajili ya kubadilisha hali ya mtu kuwa nzuri zaidi.  Basi njia yake iwe ni kutumia maneno mazuri na taratibu zenye kupendeza na kulingania kwa wema, kwani hizi ndizo njia zenye kuleta mabadiliko na ndizo zinazokubalika kisheria.

## ANAWALINGANIA WAKOSAJI:

Miongoni mwa visa vizuri, kilichotokea kuhusiana na hilo, ni kisa cha mwanachuoni mchamungu aliyejulikana kwa jina la Marufu al-Karkhiy, ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa Imamu Ridha (a.s.), kisa ambacho amekieleza ibn Jawziy katika kitabu chake kiitwacho *Swafwatus Swafwati:* "Marufu alikuwa amekaa katika fukwe ya Dajla, mara wakapita vijana wakiwa katika mashua wakipiga ngoma na kunywa ulevi. Ibrahim al-Atwrash ambaye alikuwa pamoja naye, alimwambia kuhusu wale vijana: Je, huwaoni watu hawa wakimuasi Mwenyezi Mungu Mtukufu? Basi waombee laana, basi alinyanyua mikono yake na kusema: 'Ewe Mola Wangu, nakuomba uwafurahishe katika Pepo kama ulivyowafurahisha katika dunia.' Watu waliokuwa na Marufu walishangazwa kutokana na maombi haya. Marufu aliwabainishia kwa kusema: 'Iwapo Mwe-

---

[77] Rishahriy: Muhammadiy, *Mizanul Hikma*, Jz. 7, Uk. 145.

[78] Kitabu kilichotangulia, Uk. 145.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 115 1/7/2015 11:52:49 AM

nyezi Mungu atawafurahisha huko Akhera, basi atawasamehe hapa duniani, na hilo halitokudhuruni chochote.'''[79]

Huu ndio mtazamo anaotakiwa kuwa nao Muumini juu ya watenda maovu. Na hivi ndivyo alivyokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hata pamoja na Washirikina, kwani kila ambapo washirikina walizidisha vitimbi na ubishi, yeye hakuzidisha isipokuwa subira na uvumilivu, na kunyenyea kwa kwa Mola Wake kwa kuwaombea dua ili awaongoe kwa vile wao hawajui! Na historia haijatunukulia kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliwahi kuwaombea balaa washirikina.

Swahaba wa Mtume (s.a.w.w.), Abdullahi ibn Masoud amesema: "Kama kwamba ninamuangalia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akimsimulia Nabii miongoni mwa Manabii kuhusiana na kupigwa na watu wake mpaka wakamtoa damu, na huku anaifuta damu yake usoni na akisema: Ewe Mola Wangu wasamehe watu wangu, kwani wao hawajui."

Na Kadhi Iyadh amesema katika kitabu kijulikanacho kwa jina la *Shifau*: Wakati yalipovunjika meno yake ya mbele, na uso wake kupasuka katika vita vya Uhudi, Maswahaba wake walikasirishwa sana na jambo hilo, wakasema: Lau ungewaombea maangamizi? Mtume (s.a.w.w.) akawajibu kwa kusema: "Hakika mimi sikuletwa ili niwe ni mwenye kulaani, lakini nimeletwa ili niwe mlinganiaji na mwenye rehema. Ewe Mola Wangu, waongoe watu wangu. Ewe Mola Wangu, waongowe watu wangu, kwani wao hawajui."[80]

Ama kuhusiana na Imamu Husein (a.s.), imepokewa kutoka kwake kwamba alionekana akilia katika uwanja wa Karbala, mmoja wa wafuasi wake alimuuliza: Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, unalia kwa yale ambayo Mwenyezi Mungu amekuteremshia?

[79] Answariy Sha'araniy: Abdulwahhab, ibn Ahmad, *Mukhtasw Kitabi Swafwatis Swafwati*
[80] Qazwiniy: Hasan Murtadha, Rasulul Akram, *Madrasatul Akhlaq*, Uk. 186.

Imamu (a.s.) alisema: "Hapana, hakika mimi nawalilia watu hawa, kwani wataniua mimi, na wataingia Motoni kwa sababu yangu."

Ama wale wenye mtazamo finyu, wanakuwa na hisia za uadui hata na baadhi ya ndugu zao wa karibu, wakiwakuta na kasoro yoyote huwagombeza, na wanapotenda uovu huutangaza kwa watu. Lau kama wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya, ungetekelezwa kwa mujibu wa mipaka yake na kanuni zake, basi usingekuwa na mgongano wowote na uhuru wa binadamu, bali ungenyanyua kiwango cha uelewa wa binadamu wa kujua uhuru wake, na ungekuwa ni sababu ya kurekebisha matatizo ya kijamii na kuyaondoa, na mwisho kufikia kilele cha ubora ambao utaleta manufaa na furaha kwa wote.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 117 1/7/2015 11:52:49 AM

# TANGAZO LA KIMATAIFA LA HAKI ZA BINADAMU

Kwa mujibu wa azimio la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa Na. A217 (D-3), lililotolewa tarehe 10 Disemba 1948, ambapo Mkutano huo ulitangaza tangazo la Kimataifa la haki za binadamu, maelezo kamili ya hati ya azimio hilo tunayabainisha katika kurasa zifuatazo. Baada ya tukio hili la kihistoria, Mkutano huo Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ulizitaka nchi zote wanachama kulitangaza azimio hilo, kulichapisha, kulisambaza, kulisoma na kulitolea maelezo hasa katika mashule na vyuo vingine vya elimu, bila ya ubaguzi wowote unaosababishwa na siasa za nchi au kieneo.

## UTANGULIZI:

Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa walikiri kwamba heshima ya binadamu na haki zao asili yake ni uhuru, uadilifu na amani katika ulimwengu.

Kujisahaulisha na kudharau haki za binadamu kumepelekea maudhi katika nafsi ya binadamu, na kitu ambacho wanakitazamia wanadamu ni kuishi katika ulimwengu unaojali uhuru wa kila mtu katika mazungumzo na imani, na awe huru kutokana na woga na umasikini. Basi imekuwa ni jambo muhimu sana kuwepo kanuni ambazo zitamzuia mtu asimfanyie uadui na dhulma mtu mwingine.

Kwa hivyo mataifa wanachama wa Umoja wa Mataifa, walipitisha azimio ambalo wanaamini kwamba msingi wa heshima ya mtu ni kupatiwa haki zake, na kuwepo usawa kati wa wanaume na wa-



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 118 1/7/2015 11:52:49 AM

nawake, na kuamini kwamba jambo hili ndilo linaloleta maendeleo ya kijamii na kuboresha hali ya maisha. Basi nchi wanachama waliahidi kusaidiana na Umoja wa Mataifa juu ya kuchunga haki za binadamu na uhuru na kuziheshimu.

Na kwa mujibu wa mtazamo wa kimataifa ni kwamba haki hizi na uhuru huu una umuhimu mkubwa wa kutekeleza azimio hili, basi Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ulikubaliana kulitangaza azimio hili la haki za binadamu na kuyataka mataifa yote kuliweka azimio hili mbele ya macho yao, kwa njia ya mafunzo katika mashule, na kuchukua hatua stahiki kitaifa na kimataifa. Vipengele vya azimio hilo ni kama vifuatavyo:

## KIPENGELE CHA 1

Watu wote wanazaliwa wakiwa hai wakiwa na haki na heshima sawa, na wamepewa akili na mawazo, basi ni juu yao kuamiliana wao kwa wao kwa roho ya udugu.

## KIPENGELE CHA 2

Kila mtu anastahiki kupata haki na uhuru uliomo katika azimio hili, bila ya ubaguzi wowote, kama vile ubaguzi wa kikabila au rangi au jinsia au lugha au dini au mawazo ya kisiasa au kwa mtazamo wowote ule, au uasili wa kinchi au kijamii au utajiri au uzawa au jambo jingine, bila ya kuwepo tofauti kati wanaume na wanawake, na zaidi ya hayo yaliyotangulia, kusiwe na ubaguzi wowote ambao msingi wake ni mfumo wa kisiasa au kikanuni au kwa nchi au eneo ambalo mtu anahusika nalo, ni sawa ikiwa nchi hiyo au eneo hilo linajitegemea au linatawaliwa, au halina mamlaka kamili, au likawa mamlaka yake yako kwa yeyote yule awaye.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 119 1/7/2015 11:52:49 AM

## KIPENGELE CHA 3

Kila mtu ana haki ya kuishi, kuwa huru na kupata usalama wa nafsi yake.

## KIPENGELE CHA 4

Haifai kumfanya mtumwa mtu yeyote, na ni marufuku kufanya utumwa na pia aina yoyote ya biashara ya utumwa.

## KIPENGELE CHA 5

Mtu yeyote asiadhibiwe au kuamiliwa vibaya na kinyama au kuvunjiwa heshima.

## KIPENGELE CHA 6

Kila mtu atakayeikuta haki popote, basi anapaswa aitambue kikanuni.

## KIPENGELE CHA 7

Watu wote wako sawa mbele ya haki, na wana haki ya kupatiwa ulinzi wa kutosha bila ya ubaguzi, kama ambavyo wana haki ya kutetewa dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote ambao utakwenda kinyume na azimio hili, na bila ya kuhimiza juu ya ubaguzi huu.

## KIPENGELE CHA 8

Kila mtu ana haki ya kwenda kwenye mahakama ya nchi yake ili kulalamika juu ya muamala wa kidhuluma dhidi ya haki zake za kimsingi ambazo amepewa kwa mujibu wa kanuni.

## KIPENGELE CHA 9

Haifai kumshika mtu yeyote au kumzuilia au kumhamisha kinyume cha sheria.

## KIPENGELE CHA 10

Kila mtu ana haki kamili sawa na watu wengine, kwa kupelekwa shauri lake mbele ya mahakama iliyo huru na yenye kutenda haki, ili ahukumiwe kiadilifu na kwa uwazi kwa lengo la kujua na kubainisha haki zake na kila tuhuma ya kijinai inayomkabili.

## KIPENGELE CHA 11

**1.** Kila mtu mwenye kutuhumiwa kutokana na kosa fulani, yuko huru mpaka pale litakapothibiti kosa lake kwa mujibu wa kanuni kwenye mahakama ya wazi ambayo imempa fursa muhimu za kujitetea.

**2.** Mtu asitiwe makosani kwa sababu ya kutenda jambo au kujizuia kutenda jambo, isipokuwa jambo hilo litazingatiwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa kanuni za kinchi au kimataifa wakati wa kulitenda, na pia asiadhibiwe adhabu kali zaidi kuliko ile anayostahili kuadhibiwa wakati wa kutenda kosa.

## KIPENGELE CHA 12

Mtu yeyote hana haki ya kuingilia bila ya sheria maisha ya mtu binafsi au familia yake au makazi yake, barua zake au mambo yenye kubeba heshima yake na umaarufu wake, na kila mtu ana haki ya kuichunga kanuni mfano wa hii ya kuingilia mambo ya wengine.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 121 1/7/2015 11:52:49 AM

## KIPENGELE CHA 13

**1.** Kila mtu ana uhuru wa kutembea na kuchagua mahala pa kuishi ndani ya mipaka ya kila nchi.

**2.** Kila mtu ana haki ya kusafiri kutoka katika nchi yake, kama alivyo na haki ya kurudi humo.

## KIPENGELE CHA 14

**1.** Kila mtu ana haki ya kukimbilia nchi nyingine, kujaribu kukimbilia huko kwa lengo la kukimbia machafuko.

**2.** Hatonufaika na haki hii yule mwenye kukimbia kuhukumiwa kutokana na makosa, isipokuwa makosa ya kisiasa au mambo yenye kupingana na malengo ya Umoja wa Mataifa na misingi yake.

## KIPENGELE CHA 15

**1.** Kila mtu ana haki ya kuwa raia wa nchi fulani.

**2.** Haifai kumnyima mtu uraia wake kinyume cha sheria, au kukataa haki yake ya kuubadilisha.

## KIPENGELE CHA 16

**1.** Mwanamme na mwanamke wanapofikia umri wa kubaleghe, wana haki ya kufunga ndoa na kuasisi familia bila ya kikwazo

cha jinsia au dini, na wana haki sawa katika ndoa na wakati wa kuifunga na wakati wa kuvunjika kwake.

**2.** Haitofaa kufungwa kwa ndoa isipokuwa baada ya kupatikana makubaliano kamili ya pande mbili, hakuna kulazimisha katika hili.

**3.** Familia ni muundo wa kimaumbile wa jamii, kwa hivyo ina haki ya kulindwa na jamii na serikali.

## KIPENGELE CHA 17

**1.** Kila mtu ana haki ya kumiliki akiwa peke yake au kwa kushirikiana na mwenzake.

**2.** Haifai kumzuilia mtu mali yake bila ya sheria.

## KIPENGELE CHA 18

Kila mtu ana haki ya uhuru wa kufikiri na malengo na dini, na haki hii inajumuisha uhuru wa kubadili dini yake au imani yake, na haki ya kuzitangaza kwa kuzifunza, kuzitekeleza na kuzifanyia maonesho na kuzichunga, ni sawa kama atafanya kwa hali ya siri au akiwa na wenzake.

## KIPENGELE CHA 19

Kila mtu ana haki ya kuwa na rai na mawazo, na haki hii inajumuisha uhuru wa kujiunga na raia bila kuingiliwa na yeyote, na kupokea habari na fikra na kuzitangaza kwa njia yoyote ile iwayo bila kuwepo vikwazo vya kijiografia.

## KIPENGELE CHA 20

**1.** Kila mtu ana haki ya uhuru wa kushiriki katika jumuia na vikundi vya kutafuta amani.

**2.** Haifai kumzuia yeyote kujiunga na jumuia fulani.

## KIPENGELE CHA 21

**1.** Kila mtu ana haki ya kushiriki katika uendeshaji wa mambo ya nchi yake, ikiwa ni moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi wanaochaguliwa kwa uchaguzi ulio huru.

**2.** Kila mtu ana haki kama aliyonayo mwenzake ya kupata ajira katika nchi.

**3.** Matakwa ya wananchi ndio chanzo cha kupatikana serikali, matakwa haya yatapatikana kwa njia ya uchaguzi ulio wa haki kwa kila kipindi, ambao utafanyika kwa njia ya siri na kuwepo usawa kwa wote unaotoa uhuru wa kupiga kura.

## KIPENGELE CHA 22

Kila mtu kwa sifa yake ya kuwa sehemu katika jamii, ana haki ya dhamana ya kijamii, na kupata uhakikisho kutokana na nguvu za kitaifa na usaidizi wa kimataifa, kwa mujibu wa taratibu za kila nchi na kanuni za haki za kiuchumi na kijamii na kimalezi ambazo hana budi kizipata ili kulinda heshima yake na kukuza uhuru wa shakhsia yake.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 124 1/7/2015 11:52:49 AM

## KIPENGELE CHA 23

**1.** Kila mtu ana haki ya kufanya kazi, na ana uhuru wa kuichagua kwa mujibu wa sharti za kiadilifu zenye kukubalika, kama ambavyo alivyo na haki ya kuangaliwa asikose kazi.

**2.** Kila mtu bila ya ubaguzi, ana haki ya kupata malipo yanayolingana na kazi.

**3.** Kila mtu anayefanya kazi ana haki ya kupata malipo kwa uadilifu, anapoumwa ahakikishiwe malipo ya ziada inapowezekana, ili aishi maisha ya heshima pamoja na familia yake, na mambo mengine yenye kulinda haki za kijamii.

**4.** Kila mtu ana haki ya kuanzisha na kujiunga katika vikundi vyenye kutetea maslahi yake.

## KIPENGELE CHA 24

Kila mtu ana haki ya kustarehe, na kuwa na wakati wa faragha, hasa katika kuainisha wakati wa kazi unaokubalika kiakili na wakati wa mapunziko wa kazi.

## KIPENGELE CHA 25

**1.** Kila mtu ana haki ya kuwa na kiwango cha maisha kitakacho muhakikishia afya na starehe zake pamoja na familia yake, ambayo ni kupata chakula, mavazi, makazi na matibabu, na pia huduma za msingi za kijamii, na ana haki ya kuhakikishiwa maisha yake wakati asipokuwa na kazi, anapokuwa mgonjwa,

mlemavu, mjane na uzee, na hali nyinginezo za kukosa njia ya kuishi zilizo nje ya uwezo wake.

**2.** Mama na mtoto wana haki maalumu ya kusaidiwa na kuangaliwa, na kila mtoto ana haki ya kulindwa kijamii, ikiwa mtoto huyo amepatikana kwa njia za kisheria (mtoto wa halali) au kwa njia zisizo za kisheria.

## KIPENGELE CHA 26

**1.** Kila mtu ana haki ya kusoma, na kwa uchache ni wajibu elimu ya awali na ya msingi iwe ni bure, na ilimu ya msingi iwe ni ya lazima, na inapasa kwenye elimu kujumuishwe fani na amali, na kukubaliwa kusoma elimu ya juu iwe ni kwa usawa kwa wote kwa mujibu wa uwezo (wa kielimu).

**2.** Ni wajibu malezi yalenge kukuza kikamilifu shakhsia ya binadamu, na kutilia nguvu heshima ya binadamu na misingi ya uhuru, na kukuza maelewano na urafiki kati ya mataifa yote na jumuia za kikabila na kidini, na kwa Umoja wa Mataifa kuzidisha juhudi kubwa za kuhifadhi amani.

1) Haki ya kwanza ya kuchagua aina ya malezi ni ya wazazi.

## KIPENGELE CHA 27

**1.** Kila mtu ana haki ya kushiriki kwa uhuru katika maisha ya kitamaduni ya kijamii na kunufaika na pia kuchangia katika maendeleo ya kisayansi na kunufaika nayo.

**2.** Kila mtu ana haki ya kulinda hatimiliki ya fani au vitu vya kimada vinavyotokana na uzalishaji wake wa kisayansi au kifasihi au kifani.

# KIPENGELE CHA 28

Kila mtu ana haki ya kufaidika kikamilifu na mfumo wa kijamii wa kimataifa, ambao unamhakikishia haki na uhuru kama ulivyoelezwa katika mkataba huu.

# KIPENGELE CHA 29

**1.** Kila mtu ana haki katika jamii aliomo kwa kupata uhuru ulio kamili.

**2.** Mtu atalazimika kutekeleza haki yake na uhuru wake kwa mujibu wa masharti yanayokubaliwa na kanuni tu, kwa lengo la kutoa dhamana ya haki za mwingine na uhuru wake na heshima yake, na kuhakikisha kunakuwepo uadilifu katika mfumo wa kijamii na manufaa kwa wote na tabia njema katika jamii ya kidemokrasia.

**3.** Kwa vyovyote vile, haifai kutekeleza haki hizi katika hali ya kukinzana na malengo ya Umoja wa Mataifa na kanuni zake.

# KIPENGELE CHA 30

Katika azimio hili, hakuna kipengele kinachofaa kutafsiriwa ya kwamba kinaipa fursa nchi au kikundi cha watu au mtu binafsi haki yoyote ya kufanya jambo lenye malengo ya kuvunja haki na uhuru uliomo humu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 127 1/7/2015 11:52:50 AM

# TANGAZO LA HAKI ZA MTOTO

Ilitangazwa mbele ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa azimio Na. 1386 (D-14), tarehe 20 Novemba, 1959.

## UTANGULIZI:

Wakati mataifa wanachama wa Umoja wa Mataifa walipoingia katika mikataba, walisisitiza kwa mara nyingine juu ya imani za haki za binadamu na heshima ya shakhsia ya kibinadamu na nafasi yake, na kuazimia kutilia nguvu maendeleo ya kijamii na kunyanyua hali ya maisha katika hali ya uhuru mpana zaidi. Kwa hivyo Umoja wa Mataifa ukatangaza tangazo la haki za binadamu, ya kwamba kila mmoja apate haki zote na uhuru uliokubaliwa katika tangazo hilo, bila ya ubaguzi wowote wa kikabila, rangi, jinsia lugha, dini, mtazamo wa kisiasa au usio wa kisiasa, au uzalendo wa kinchi au kijamii au utajiri au nasaba au aina yotote ile.

Na kwa vile mtoto ana mahitaji maalumu kutokana na kutokumea mwili wake na akili yake, na hasa kuhitaji kanuni zitakazomtetea, ikiwa ni kabla au baada ya kuzaliwa. Kutokana na umuhimu huu wa kipekee, kulitolewa tangazo la haki za mtoto lililotolewa huko Jeniva mnamo mwaka 1924. Ilizingatiwa kwamba hilo ni azimio la kimataifa la haki za binadamu, na kutangaza kuwepo chombo maalumu cha Umoja wa Mataifa kitakachoshughulikia masuala ya watoto. Basi kikao cha hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa kikatangaza rasmi, ‘Haki za Mtoto.’ Hii ni kwa ajili ya kumfanya afurahikie na kuneemeka vyema na hali yake ya utoto kwa manufaa yake na kwa jamii, kwa kupata haki na uhuru kama ulivyoainishwa katika tangazo



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 128 1/7/2015 11:52:50 AM

hili, na kuwataka wazazi, wanaume, wanawake, taasisi za misaada, serikali za mitaa na serikali kuu, zote kwa pamoja kutambua haki hizi na kufanya juhudi za kuzilinda kwa kuweka sheria kwa mujibu wa vipengele vifuatavyo:

## KIPENGELE CHA 1:

Inapasa kwa mtoto apate haki zake zote kama zilivyoelezwa katika azimio hili, na kila mtoto apatiwe haki hizi bila ya ubaguzi wa kikabila, rangi, jinsia, dini, mtazamo wa kisiasa au usio wa kisiasa, uasili wa kinchi, kiutaifa, uwezo wa kimali, nasaba au jambo jingine linalomhusu yeye au familia yake.

## KIPENGELE CHA 2

Inapasa kwa mtoto apatiwe himaya maalumu, na apatiwe kila fursa kwa mujibu wa sheria na isiyokuwa ya kisheria ya kumuwezesha kukua kimwili, kiakili, kitabia, kiroho na kijamii, ukuaji wa kawaida ulio salama katika mazingira ya uhuru na heshima. Basi maslahi yake ya hali ya juu ni kwa jambo hili kutungiwa sheria.

## KIPENGELE CHA 3

Mtoto tangu kuzaliwa kwake ana haki ya kupewa jina na kuwa na utaifa.

## KIPENGELE CHA 4

Inapasa kwa mtoto kupatiwa dhamana ya kijamii, na kuweza kukua katika afya njema, basi kwa lengo hili inapasa kwa mtoto pamoja

na mama yake kupewa uangalizi maalumu kabla ya kuzaa na baada ya kuzaa. Na kwa mtoto ana haki ya kupewa huduma ya kutosha ya chakula, makazi, kucheza na huduma za kiafya.

## KIPENGELE CHA 5

Mtoto mlemavu wa mwili au akili au kijamii, inapaswa apewe matibabu, malezi na uangalizi maalumu ambao unalingana na hali yake.

## KIPENGELE CHA 5

Ili mtoto aweze kunufaika na utu wake na kukua kikamilifu, anahitaji mapenzi na maelekezo, hayo yatawezekana kwa kupata uangalizi wa wazazi wake ikiwa ni katika wajibu wao, hayo ikiwa anapata mapenzi na utulivu wa kiroho na kimwili na kutoka kwao, hapo haitofaa kutenganishwa nao, ama ikiwa ni kinyume chake, hapo itafaa kwa mtoto mdogo atenganishwe na mama yake. Na ni wajibu kwa jamii na serikali kuu kutoa uangalizi maalumu kwa watoto wenye kukoseshwa haki zao kutoka kwa familia na wale wenye kukosa namna ya kuishi. Na inapendekezwa kutolewa msaada wa serikali na usio wa serikali kwa ajili ya kuwasaidia watoto walioko katika familia yenye idadi kubwa ya watu.

## KIPENGELE CHA 6

Mtoto ana haki ya kupata elimu, ambayo kwa uchache inapasa iwe ni bure na ya lazima katika ngazi za awali, na ikusudiwe kunyanyua kiwango cha elimu ya mtoto na kumuwezesha kupata fursa ya kukuza uwezo wake na kipaji chake, na kujihisi kwamba ana jukumu la kielimu na kijamii, ili awe ni mtu mwenye manufaa katika jamii. Na



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 130 1/7/2015 11:52:50 AM

manufaa makubwa ya mtoto yanapasaswa yatekelezwe na wahusika kwa kumuelimisha na kumuelekeza. Majukumu haya yanaanza kwa wazazi wake kwa kiwango kikubwa. Ni wajibu kwa mtoto apatiwe fursa ya kutosha ya kucheza na kustarehe, ambapo mawili haya yawe yanamuelekeza kwenye elimu, na ni wajibu wa jamii na serikali kuweza kurahisisha haki hizi.

## KIPENGELE CHA 8

Ni wajibu mtoto katika mazingira yote, awe katika watu wanaomjali kwa kumhami na kumsaidia.

## KIPENGELE CHA 9

Ni wajibu mtoto aepushwe na aina zote za kutelekezwa, kufanyiwa ukali na kutumikishwa, na kwa namna yeyote ile haifai kutumiwa kibiashara, na wala haifai kumtumikisha mtoto kabla ya kufikia umri wa kubaleghe, na haifai kwa vyovyote vile kufanyishwa kazi au kuachiwa kufanya kazi yoyote ile inayoidhuru afya yake au elimu yake, kukwaza ukuaji wake wa kimwili au kiakili au kitabia.

## KIPENGELE CHA 10

Ni wajibu mtoto apewe himaya zote dhidi ya kuamiliwa kwa muamala wenye kumbagua kirangi au dini au aina yoyote ile ya ubaguzi, na alelewe katika namna ya kueleweshwa, kusamehewa, na urafiki kati ya mataifa, amani, udugu wa kimataifa, na kutambua kikamilifu wajibu wa kutoa nguvu zake na vipawa vyake kwa ajili ya kuwatumikia binadamu wenzake.

# WARAKA WA HAKI ZA BINADAMU KATIKA UISLAMU

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.**

Kila sifa njema inamstahikia Mwenyezi Mungu, na Rehema na Amani zimwendee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

Wanachama wa Umoja wa Nchi za Kiislamu, ambao wanaamini yakwamba Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote ndiye Muumbaji wa kila kitu, na ndiye Mpaji wa kila neema, Ambaye amemuumba binadamu katika umbile lililokamilika, na kumtukuza na kumfanya kuwa Khalifa katika ardhi na kumfanya kuwa ndiye muimarishaji wake (ardhi) na mtengenezaji, na amembebesha majukumu ya Mwenyezi Mungu, na amemtiishia vyote vilivyomo mbinguni na ardhini.

Na hali ya kuamini Ujumbe wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.), ambaye Mwenyezi Mungu amemleta kwa ajili ya kuongoa watu akiwa na Dini ya Haki, ambaye ni Rehema kwa walimwengu wote na mkombozi wa wenye kuonewa, na mvunjaji wa matwaghuti na wenye kujifanya waungu. Mtume ambaye alitangaza usawa kwa wanadamu wote. Hakuna ubora wa mtu juu ya mwingine isipokuwa kwa uchamungu, na alibatilisha matabaka na kuchukiana kati ya watu, ambao wameumbwa na Mwenyezi Mungu kutokana na nafsi moja.

Na kwa mujibu wa itikadi yenye ukhalisia, ambayo ndio iliyolisimamisha jengo la Uislamu, akida ambayo imewataka watu wasimuabudu mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na wala wasimshirikishe na kitu chochote, na wala wengine wasiwafanye



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 132 1/7/2015 11:52:50 AM

waungu badala ya Mwenyezi Mungu. Akida ambayo ndio iliyoweka msingi wa uhakika wa uhuru wa binadamu na utukufu wake, na kutangaza wazi kwamba binadamu asimwabudu binadamu mwenzake.

Na kwa mujibu wa yale yaliyoletwa na Sheria za Kudumu za Kiislamu, ambazo zimeeleza bayana juu ya kulinda Dini, nafsi, akili, utu, mali, na kizazi. Sheria ambazo ni za kipekee ambazo zimekusanya mambo yote, kwani zimekusanya kati ya mambo ya kiroho na kimwili, na kuzungumzia kati ya akili na moyo, na kutofautisha kati ya mawazo na ukalisia, na kupima kati ya haki na wajibu, na kueleza kati ya heshima ya mtu binafsi na maslahi ya wengi, na kusimamisha hukumu za uadilifu kati ya watu wenye kikinzana, Basi hakuna kuchupa mipaka wala kula hasara.

Na kwa kuzingatia kazi ya kistaarabu na kihistoria ya umma wa Kiislamu ambao Mwenyezi Mungu ameufanya kuwa ni umma bora. Umma ambao umewarithisha wanadamu ustaarabu wa kimataifa ambao ni wa kati na kati, ustaarabu ambao umeiunganisha dunia na mbingu, na kuifungamanisha dunia na akhera, na kukusanya kati ya imani na elimu. Basi kinachotarajiwa kwa umma huu katika zama hizi ni kuwaongoa wanadamu waliozama katika fikara tofauti, na kutoa ufumbuzi wa matatizo ya ustaarabu wa kimada uliopo.

Na kuchangia katika juhudi za kibinadamu zinazohusiana na haki za binadamu ambazo zinalenga katika kumhami kutokana na kutumikishwa na kuonewa, na kulenga katika kuhakikisha uhuru wake na haki zake katika maisha ya heshima ambayo yanawafikiana na Sheria za Kiislamu.

Hali ya kuamini kwamba, binadamu amekata masafa makubwa ya elimu ya kimada, ni kwamba anahitaji mno mambo ya kiimani katika maendeleo yake na utambuzi wa nafsi yake ambao utalinda haki zake.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 133 1/7/2015 11:52:50 AM

Na kuzingatia kwamba, haki za kimsingi na uhuru katika Uislamu ni sehemu ya Dini ya Waislamu. Hakuna yeyote aliye na haki ya kutozitekeleza zote au baadhi yake, au kizikataa au kuzidharau hukumu hizi za Mwenyezi Mungu ambazo ameziteremsha katika Kitabu Chake, na kufikishwa na Mtume Wake wa mwisho, na kuzikamilisha katika Ujumbe wa mbinguni, na ikawa kuchunga haki hizo ni miongoni mwa ibada, na kuzidharau au kwenda kinyume nazo ni kuipinga Dini, na kila mtu ana majukumu yeye binafsi, na umma pia una majukumu.

Nchi wanachama wa Nchi za Kiislamu (O.I.C.) ulitangaza vipengele vifuatavyo:

# KIPENGELE CHA 1

a. Binadamu wote ni familia moja, wamekusanywa na ibada ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja na kwamba wote ni watoto wa Adamu (a.s.), na asili ya watu wote ni kuheshimiwa kutokana na ubinadamu wao, na kwa mujibu wa majukumu yao. Hakuna ubaguzi wowote wa kikabila, rangi, lugha, upahala, utaifa, mwelekeo wa kisiasa au nafasi ya kijamii au jingine lolote lile.

b. Viumbe vyote ni waja wa Mwenyezi Mungu, na anayependwa zaid na Yeye ni yule mwenye kufanya ibada vizuri zaidi, na ni kwamba hakuna ubora kwa yeyote kati yao, isipokuwa kwa mwenye kumcha Mwenyezi Mungu.

# KIPENGELE CHA 2

a. Uhai ni haki anayostahiki kila binadamu, na ni juu ya watu na jamii na nchi kuilinda haki hii dhidi ya hujuma, na wala haifai kuitoa roho bila ya Sheria inayokubalika.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 134 1/7/2015 11:52:50 AM

b. Ni wajibu wa Kisheria kulinda kuendelea kwa maisha ya binadamu mpaka pale anapotaka Mwenyezi Mungu, basi haifai kutoa mimba bila ya kuwepo haja kubwa kwa mujibu wa Sheria. Basi haifai kuzuia kuoa na kuzuia kuzaa bila ya sababu ya Kisheria.

## KIPENGELE CHA 3

a. Wakati wa vita au mizozo ya kisilaha, haifai kumuua asiyeshiriki katika vita, kama vile mzee, mwanamke na mtoto mdogo. Na majeruhi ana haki ya kutibiwa, na mateka alishwe, apewe makazi na mavazi, na ni haramu kuwafedhehi waliouwawa. Na inafaa kubadilishana mateka na wanafamilia kukutana na watu wao ambao wametenganishwa na vita.

b. Haifai kukata miti, na wala mazao na wanyama wasiharibiwe, na wala majengo ya maadui yasivunjwe kwa kupigwa mabomu au kung'olewa au kwa njia nyingine, isipokuwa kwa ulazima wa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria.

## KIPENGELE CHA 4

Kila mtu ana heshima yake baada ya kifo chake na kulindwa utu wake, na ni juu ya nchi na jamii kuulinda mwili wake na kuuzika.

## KIPENGELE CHA 5

Familia ndio msingi wa kujenga jamii, na ndoa ndio msingi wa familia:

a. Wanaume na wanawake wana haki ya kuowana, basi haifai kuwekewa vizuizi vya kikabila, rangi au utaifa katika kunufaika kwao na haki hii.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 135 1/7/2015 11:52:50 AM

b. Ni juu ya jamii na nchi kuondosha vikwazo vya ndoa, na warahisishe kufana kwake na kuilinda familia na kuihami.

## KIPENGELE CHA 6

a. Mwanamke yuko sawa na mwanamume katika heshima ya utu, ana haki za kufanyiwa kama vile alivyo na wajibu wa kufanya, ana haki ya kupata maendeleo, na ana haki ya kumiliki mali na haki ya kuihifadhi kwa jina lake na kwa nasaba yake.

b. Ni jukumu la mume kuihudumia familia na ana majukumu ya kuishughulikia kwa mujibu wa usimamizi wa mwanamume kama ulivyoelezwa katika Sheria za Kiislamu.

## KIPENGELE CHA 7

a. Baada ya mtoto kuzaliwa ana haki kwa wazazi wake, jamii, na serikali katika kumlea na kumchunga katika mambo ya kimada na kimalezi, kama ilivyo wajibu mama yake kuangaliwa na kupewa huduma maalumu.

b. Baba wana haki ya kuchagua aina ya malezi wanayoyataka kwa watoto wao, pamoja na kuchunga maslahi yao na mustakabali wao kwa mujibu wa mafunzo na Sheria za Kiislamu.

c. Baba wana haki ya ubaba kwa watoto wao, na ndugu wa karibu wana haki kwa jamaa zao kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu.

## KIPENGELE CHA 8

Kila mtu ana haki ya kustarehe na jinsia yake, na haifai kumzuilia jinsia yake kwa njia ya dhulma.

## KIPENGELE CHA 9

Kila mtu ana haki ya kustarehe ya utu wake kisheria, katika kutekeleza yaliyo wajibu kuyafanya na yale anayostahiki kufanyiwa, na pindi anapokosa au kupungua utu wake, basi msimamizi wake atafanya kwa niaba yake.

## KIPENGELE CHA 10

a. Kutafuta elimu ni wajibu, na kufundisha ni wajibu wa nchi, basi ni juu yake kuhakikisha kwamba imeweka miundo ya msingi wake na kuiweka elimu katika fani mbalimbali, ili kuleta ufanisi wa jamii, na kumpa mtu fursa ya kuweza kutambua Dini ya Kiislamu na ukweli juu ya ulimwengu na kudhalilishwa kwake (ulimwengu) kwa ajili ya manufaa ya wanadamu.

b. Ni haki ya kila binadadamu katika taasisi ya elimu na makundi mbalimbali kama vile familia, shule, vyuo vikuu na vyombo ya habari kumlea binadamu katika mafunzo ya kidini na kidunia, malezi yaliyo kamili na ya kiadilifu, kiasi cha kuweza kumea utu wake na imani yake juu ya Mwenyezi Mungu, kuwa na nguvu na kuheshimu kwake haki na wajibu na kuzitetea.

## KIPENGELE CHA 11

Kwa vile binadamu anatakiwa afuate Uislamu ambao ni Dini ya maumbile, basi haifai kufanyiwa aina yoyote ile ya kutenzwa nguvu ili aiche Dini hii na aingie dini nyingine, au kukufuru. Kama ambavyo haifai kutumia fursa ya ufakiri wake au ujinga wake ili abadili Dini yake.

## KIPENGELE CHA 12

a. Mtu anazaliwa akiwa huru, na hakuna yeyote mwenye haki ya kumfanya mtumwa au kumdhalilisha au kumtenza nguvu au kumtumikisha, na wala hakuna utumwa isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu tu.

b. Ukoloni ni jambo la haramu kabisa, nao ni aina mbaya sana ya utumwa, na mataifa yanayosibiwa na hali hii wana haki kamili ya kujikomboa kutokana nao na kuamua mustakabali, na ni juu ya nchi na mataifa kuwasaidia kuutokomeza ili kusafisha kila aina ya ukoloni na utekaji, na mataifa yote yana haki ya kutawalia utajiri wake na mali zake asili.

## KIPENGELE CHA 13

Kila mtu ana haki ya kusafiri na kuchagua mahali pa kuishi, ikiwa ni ndani ya nchi yake au nje ya nchi. Na wakati wa masaibu, ana haki ya kukimbilia nchi nyingine, na ni kwa nchi aliyokwenda ni juu yake kumpeleka sehemu yenye amani, hii ni pale itakapokuwa ukimbizi huo hautokani na kitendo kinachokhalifu Sheria za Kiislamu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 138 1/7/2015 11:52:50 AM

## KIPENGELE CHA 14

Kazi ni haki ambayo nchi inatakiwa impatie kila mwenye uwezo, na mtu ana haki ya kuchagua kazi inayolingana naye ambayo italeta maslahi yake na maslahi ya jamii. Na mfanyakazi ana haki ya kupewa dhamana ya amani na usalama, na wala haifai kufanyishwa kazi asiyoiweza au kumtumikisha au kumdhuru. Na ni juu yake kupewa ujira wa kazi yake pasi na kucheleweshwa, na ni haki yake kupewa mapumziko na marupurupu anayostahiki. Naye anatakiwa afanye kazi kwa ikhlasi na kwa uzuri. Pindi wafanyakazi watakapozozana na wajiri, ni juu ya serikali kuingilia ili kuondosha dhulma na kuleta haki kwa uadilifu bila ya kuegemea upande mmoja.

## KIPENGELE CHA 15

Binadamu ana haki ya kufanya biashara yenye kuruhusiwa kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu, bila ya kuzuia bidhaa au kughushi au kumdhuru mwingine.

## KIPENGELE CHA 16

a. Kila binadamu ana haki ya kumiliki kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu (ikiwa ni mtu binafsi au kwa kushirikiana na mwingine), kama vile alivyo na haki ya kutumia anachokimiliki katika njia ambayo hakimdhuru yeye au mwingine miongoni mwa mtu au jamii, na wala haifai kupora mali, isipokuwa kwa ajili ya maslahi ya umma na kulipwa mara moja kwa uadilifu.

b. Kwa njia yoyote ile haifai kutaifisha mali, isipokuwa kwa mujibu wa sheria.

## KIPENGELE CHA 17

Kila mtu ana haki ya kunufaika na kazi ya uzalishaji wake wa kielimu au kifasihi au fani au kitekinolojia, na kila mwenye kuchangia katika uzalishaji huo, ana haki ya kulindiwa maslahi yake ya kifasihi na mali inayotokana nayo, kwa msingi uzalishaji huu uwe haupingani na Sheria za Kiislamu au itikadi au tabia.

## KIPENGELE CHA 18

a. Kila mtu katika jamii yake na nchi yake ana haki ya kupata uangalizi wa kiafya na kijamii, na kupatiwa kila mahitaji ya kijamii ambayo anayahitaji, hii ni kwa mujibu wa uwezo uliopo.

b. Nchi ina haki ya kumpatia kila mtu maisha mazuri yenye kumtosheleza yeye na wanafamilia wake, ambayo ni chakula, mavazi, makazi, elimu, matibabu na mahitajio mengine ya kimsingi.

## KIPENGELE CHA 19

a. Kila mtu ana haki ya kuishi kwa amani yeye na watu wake na mali yake.

b. Binadamu ana haki ya kuwa huru katika harakati zake maalumu za maisha yake, nyumbani kwake, familia yake, mali yake na mawasiliano yake, na wala haifai kumpeleleza au kumchunguza au kumchafulia jina lake. Na ni wajibu juu ya serikali kumtetea dhidi ya kila uingiliaji wa kidhulma, hayo yote ni kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.

c. Nyumba ina heshima yake katika kila hali, haifai kuivunja, au kuipora, au kuwatimua wakaazi wake, na wala haifai kuingia pasi na idhini ya wenyewe, au kuingia kwa namna isiokubalika kisheria.

## KIPENGELE CHA 20

a. Asili ya majukumu ni ya mtu binafsi, na wala haifai kutoa adhabu isipokuwa kwa mujibu wa maandiko matakatifu.

b. Mtuhumiwa hana kosa mpaka pale litakapothibitishwa kosa lake na mahakama ya kiadilifu, ambayo itampa fursa zote za kujitetea.

## KIPENGELE CHA 21

Haifai kumkamata mtu kinyume na Sheria ya Kiislamu, au kumzuilia uhuru wake, au kumfukuza au kumtesa, au kumuadhibu kimwili au nafsi, au aina yoyote ile ya muamala wenye udhalili au mgumu au wenye kupingana na heshima ya binadamu. Kama ambavyo haifai kwa mtu yeyote kufanyiwa majaribio ya kiafya au kisayansi bila ya ridhaa yake, kwa sharti afya yake na uhai wake usije ukadhurika, kama ambavyo haifai kutunga sheria maalumu ambazo zinazihusu vyombo vya utendaji.

## KIPENGELE CHA 22

a. Kila mtu ana haki ya kuwa na uhuru wa fikra za mawazo na kuyafikisha kwa njia yoyote ile ndani ya Sheria za Kiislamu.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 141 1/7/2015 11:52:50 AM

b. Kila mtu ana haki ya kulingania kwenye kheri na kuamrisha mema na kukataza mabaya, na ana haki ya kushirikiana na mwingine miongoni mwa watu katika kutekeleza haki hii, haya yote ni kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu, na ni juu ya serikali na jamii kutoa msaada unaohitajika.

c. Vyombo vya habari ni jambo muhimu sana lenye kustawisha jamii. Ni haramu kuvitumia vibaya, na kutumia kwa matumizi yoyote yenye kupelekea kuiharibu jamii, kwa kuiparaganyisha au kuidhuru au kuleta mtingishiko wa imani.

d. Haifai kuibua mambo yenye kuleta chuki za kibaguzi au kikabila, au chochote ambacho kitaleta ubaguzi wa aina yoyote.

## KIPENGELE CHA 23

a. Watu wote wako sawa mbele ya Sheria, ambapo mtawala na raia ni sawa.

b. Ni haki kwa watu wote kwenda mahakamani.

## KIPENGELE CHA 24

a) Uhuru wa jamii ni wajibu unaotoa dhamana ya kimsingi ya binadamu, na uongozi ni amana, basi ni haramu kabisa kuutumia vibaya.

c. Kila mtu ana haki ya kushiriki katika uendesahaji wa mambo ya umma ya nchi yake, kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kama vile alivyo na haki ya kuongoza mambo ya umma kwa mujibu wa sheria.

## KIPENGELE CHA 25

Kila haki na uhuru iliyothibitishwa katika azimio hili, ni kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu.

## KIPENGELE CHA 26

Sheria za Kiislamu ndio marejeo peke yake kwa ajili ya kutoa tafsiri au maelezo ya kipengele chochote kati ya vipengele vya azimio hili.

## KIPENGELE CHA 27

Nchi wanachama wa Umoja wa nchi za Kiislamu zina wajibu wa kuchukua hatua zote za lazima, kwa lengo la kutekeleza azimio hili.

## VITABU VYA MAREJEO

**1.** Qur'ani Tukufu.

**2.** Ibn Hanbal: Imamu Ahmad, *Musnad Imami Ahmad ibn Hanbal*, Toleo la kwanza, 1998A.D., Alamul Kutubi, Beiruti.

**3.** Ibn Aashur: Muhammad Tahir, *Tahrir wat-Tanwiyri*, toleo la mwanzo, 2000A.D., Muassasatu Tarikh, Beiruti.

**4.** Ibn Qudama: *Al-Mughniy*, toleo la pili, 1992A.D., Hijru litwabaa, Cairo.

**5.** Ibn Mandhur: Muhammad ibn Mukrim ibn Ali, *Lisanul Arabil Muhit*, 1988A.D., Darul Jail, Daru Lisanul Arabi, Beiruti.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 143 1/7/2015 11:52:50 AM

**6.** Al-Asfahaniy: Sheikh Muhammad Husein, *Hashiyatu Kitabil Makasib*, toleo la kwanza, 1418A.H., Darul Mustafa liihyai turathi, Qum.

**7.** Al-Alusiy al-Baghdadiy: Sayyid Muhammad Shukriy, *Ruhul Maaniy fi tafsiril Qur'ani*, toleo la mwaka 1985A.D., Saru Ihtai Turathil Arabiy, Beiruti.

**8.** Al-Amidiy Tamimiy: Abdul Wahid, *Ghurarul Hikam wa Durarul Kalam*, Toleo la kwanza, 1987A.D. Muassasul A'lamiy Lilmatbuatiy, Beiruti.

**9.** Al-Aminiy: Abdul Husein, *Al-Ghadir*, Muassasul A'lamiy Lilmatbuatiy, Beiruti-Lebnon, Toleo la kwanza, 1994A.D.

**10.** Al-Answariy Sha'raniy: Abdul Wahhab ibn Ahmad, *Mukhtaswar Kitabi Swaf-watu Swaf-wa*, Matbuatu Nahdha al-Hadithiya, Makkatul Mukarrama, 1967A.D.

**11.** Baqiy: Imaduddin, *Taqriyratu darsu Ayatullahi al-Muntadhariy, biun-wani Huquqil insane am Huquqil insanil Muumini?* Annaz-atu al-insaniya wal Islam, Qum, 1434A.H., www.montazeri.w.s.

**12.** Al-Bukhariy: Muhammad ibn Ismail, *Sahihul Bukhariy*, 1999A.D, Darul Kutubil Alamiya, Beiruti.

**13.** Hurrul Amiliy: Muhammad ibn Hasan, *Wasailu Shi'ah*, Toleo la kwanza 1993A.D., Muassasatu Ahlul bayt (a.s.) Liihyai Turathi, Beiruti.

**14.** *Al-Hayatu*: Gazeti la kila siku linalotolewa London, Jumanne, 27|1|2004A.D. – 5,Dhul Hijja 1424A.H. Na. 14915.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 144 1/7/2015 11:52:50 AM

**15.** Rishahriy: Muhammadiy, *Mizanul Hikma*, Markazun Nashri, Maktabul I'lamil Islamiy, Qum.

**16.** Sajistaniy: Sulayman ibn Ash-ath, *Sunanu Abi Daudi*, Toleo la kwanza 1988A.D., Darul Jinani, Beiruti.

**17.** Sistaniy: Ali Huseyniy, *Fiqhu lil-Mughtaribin*, Toleo la lwanza 1998A.D.

**18.** Sharifu Radhiy: Ali ibn Husein, *Nahjul Balaghah*, Tahqiqu Subhu Swalih, Toleo la kwanza 1967, Darul Kutubi, Beiruti Lebnon.

**19.** Shansuddin: Muhammad Mahdiy, *Jihadul Umma*, Toleo la kwanza 1997, Darul Ilmi lilimalayiin, Beiruti.

**20.** Shiraziy: Nasir Makarim, *Ta'liqati alal-Ur-watul Wuth-qaa,* Toleo la pili 1413A.D., Madrasatu Amiril Muuminin, Qum.

**21.** Tabatabai: Sayyid Muhammad Husein, *al-Mizanu fi Tafsiril Qur'ani*, Toleo la kwanza 1991A.D., Muassasatul A'lamiy, Beirut.

**22.** Tabarriy: Muhammad ibn Jarir, *Tarikh Tabariy*, Muassasatul A'lamiy Lilmatbuati, Beirut.

**23.** Tusiy: Muhammad ibn Hasan, *Tahdhibul Ahkami, Tahqiqu Hasan al-Musawiy*, Toleo la pili 1959A.D., Daruul Kutubil Islamiyya, Najaf al-Ashraf.

**24.** Abudi Shalijiy, *Mausuatul Adhabi*, Toleo la pili 1999A.D., Darul Arabiya lilmausuati, Beirut.

**25.** *Ukadh: Sahifatu yaumiyya,* Saudia, linatolewa na taasisi ya ukadh lisahafati wannashri, 4|12| 1432A.H.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 145 1/7/2015 11:52:50 AM

**26.** Fadhlullahi: Muhammad Husein, *Tafsiru fi Wahyil Qur'ani*, Toleo la pili 1998A.D., Darul Malak, Beirut.

**27.** Qurtubiy: Muhammad ibn Ahmad, *Tafsirul Qurtubiy*, Toleo la kwanza 2000A.D, Darul Kutubil Ilmiyya, Beirut.

**28.** Qazwiniy: Hasan Mutradha, *Rasulul Akram Madrasatul Akhlaq*, Darul Bayanil Arabiy, Toleo la kwanza 1991A.D.

**29.** Qushayriy Nisaburiy, Muslim ibn Hajjaj, *Sahihu Muslim bisharhin Nawawiy*, Daru Turathil Arabiy, Beirut.

**30.** Kandahalwiy: Muhammad Yusuf, *Hayatu Swahaba*, Matba-atu Darul fikriy, Toleo la kwanza 1974A.D, Lebanon-Beirut.

**31.** Al-Kulayniy: Muhammad ibn Yaqub, *al-Kafiy*, Toleo la pili al-Muswahaha 1985A.D, Darul Adh-wai, Beirut.

**32.** Kayaliy: Abdul Wahhab, *Muassasatu Siyasa*, Toleo la pili 1990A.D, Muassasatul Arabiya liddirasatu wannashri, Beirut.

**33.** Lalandi: Andariya, *Muassasatu Landi al-falsafiyya*, Toleo la kwanza 19976A.D., Manshuratu Uweydati, Beirut, Paris.

**34.** Al-Majlisiy: Muhammad Baqir, *Biharul An-wari*, Toleo la pili 1983A.D, Daru Turathil Arabiy, Beirut.

**35.** Al-Muhsiniy: Muhammad Asif, *Hududu Sharia-Almuharramati*, Toleo la pili.

**36.** *Munaddhamatul Afwi Dawliy*, Azimio Na.33, ASA 99\20, Tovuti: www.ns-news service, text, Arabic.org pakis-asa_33_20_99.htm,99asa.

**37.** Al-Musawiy: Sharif Radhiy, *Nahjul Balaghah*, Tahqiq Duktur Swubhu Swalih, Toleo la kwanza 1967A.D, Darul Kitabi, Beirut, Lebnon.

**38.** Al-Hindi: Ali Muttaqiy: *Kanzul Ummal*, Muassasatu Risala, Toleo la tano 1985A.D., Beirut.

**39.** *Hay-atul Ighathatil Islamiyya al-Alamiyya*, Maktabul Ahsai, 100 Suali wajawabi fil amalili khayriy, Toleo la kwanza 1423A.H.

**40.** Wizaratul Awqafi Washuunil Islamiyya, *Muassasatul Fiqhiyya*, Toleo la nne 1993, Kuweit.

**41.** Al-Watan: *Swahifatu Yaumiyya Sudiyya*, 23 Februari, 2002A.D.



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 147 1/7/2015 11:52:50 AM

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 148 1/7/2015 11:52:50 AM

24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 149 1/7/2015 11:52:51 AM

52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?

80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali (as)
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 151 1/7/2015 11:52:51 AM

108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) - (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) - (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l’Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi

134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur’an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur’an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur’ani – Majibu na Maelezo

162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye

189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Tawhiid Na Shirki katika Qur’ani Tukufu
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Kishia (Al- Muraja’aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali (as) na Mambo ya Umma
214. Imam Ali (as) na Mfumo wa Usawa



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 155 1/7/2015 11:52:51 AM

215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
227. Yafaayo kijamii
228. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
229. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
230. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
231. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya Kiislamu
232. Imam Mahdi Na Bishara Ya Matumaini
233. Jihadi
234. Majanga Na Jukumu La Jamii
235. Muhadhara wa Maulamaa
236. Mashairi ya Kijamii
237. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
238. Mwanamke Katika Harakati za Mageuzi
239. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
240. Yusuf Mkweli



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 156 1/7/2015 11:52:51 AM

241. Hotuba za Kiislamu juu ya Haki za Binadamu
242. Ugaidi wa Kifikra katika Medani ya Kidini
243. Imam Mahdi (as) – Imam wa zama hizi na Kiongozi wa Dunia
244. Imam Mahdi (as) ni Tumaini la Mataifa
245. Imam Husein (as) ni Utu na Kadhia
246. Talaka Tatu
247. Uswalihina Dhahiri na Batini yake
248. Upotofu ndani ya kitabu cha mitaala kwa Shule za Sekondari juu ya Uislamu
249. Imam Husein (as) ni Kielelezo cha kujitoa Muhanga na Fidia
250. Uislamu wa Shia

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Ya Muhammadi (s.a.w.w) Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique



46_14_Haki za Binadamu _7_Jan_2015.indd 157 1/7/2015 11:52:51 AM